# Nipashe

Jumanne Novemba 15, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581130

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



Nipashe
TESA
Jumanne Novemba 15, 2022
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 17
Msisimko wasichana mashujaa wafugaji walipovunja mwiko

Ukurasa 16
Utajiri uliojificha ndani ya haki miliki: Huanzia kuzisajili, zitambulike, zilindwe

Ukurasa 19
COP 27 kufanyika Misri hakuna tija kama waharibifu hawatatoa fedha kuinusuru Afrika

SAYANSI NA SABATO KASIKA

AJALI YA NDEGE BUKOBA

Fahamu asili, kazi kisanduku cheusi kumbe si cheusi, tena hakiungui

MARA ndege inapopata ajali kama ilivyotokea Bukoba hivi karibuni, kimbilio ni kisanduku cheusi ambacho kina taarifa za mwenendo wa safari zote za ndege hadi siku ilipoanguka.

Kisanduku cheusi au black box watu wengi hawakifahamu ni kama siri ya wahandisi wabunifu wa ndege waliyoiweka ili kupata taarifa iwapo itapata matatizo.

Ajali iliyotokea mkoani Kagera, ndege ya Precision Air, alianguka ndani ya Ziwa Victoria na kuua watu 19, uchanguzi wake umeanza na kisanduku cheusi kikitarajiwa kujibu maswali ya chanzo.

Mhandisi wa ndege mstaafu, Gideon Mgusi, anazungumza na Nipashe kuelezea maana ya black box na jinsi inavyofanya kazi ya kubainisha chanzo cha misukosuko inayoiangusha ndege.

Anasema ni kifaa ndani ya ndege kinachonasa na kutunza taarifa mbalimbali za mwenendo wa ndege wakati wote inapokuwa angani na kwamba kina kitu au 'memory card au hard disc' ya kompyuta inayorekodi kila kitu, kuanzia siku ilipoanza kupaa.

"Kwa kawaida katika ndege kubwa kama Airbus na Boeing kuna vifaa viwili vya kunasa taarifa. Hivi ndivyo kwa ujumla wake huitwa black box. Cha kwanza kinanasa sauti na kelele zote ndani ya chumba cha marubani," anasema Mhandishi Mgusi.

Kina uwezo wa kutunza sauti miaka yote hata saa mbili baada ya ajali na kwamba mazungumzo yote kati ya marubani wenyewe, na minara ya kuongozea ndege (control towers) au rubani na abiria wake anasema.

"Kifupi, sauti au kelele zozote ndani ya chumba cha marubani hunaswa na kutunzwa. Hata ukivuta nyuma kiti mikwaruzo hunaswa. Kuna kinasa sauti ndani ya chumba hicho kikiitwa Cockpit Voice Recorder (CVR) japo kisanduku hicho hakiko ndani ya chumba hicho," anasema.

Kifaa kingine huitwa Flight Data Recorder (FDR) ambacho hunasa na kutunza taarifa za aina nyingi na mbalimbali na kwamba ndicho chenye 'memory card au hard disc' zinazorekodi mambo mengine mengi mno.

Mfano, kasi ya ndege angani, kulinganisha na hewa ilipo ndege, mwendokasi, muda unaotumika, uwezo wa injini inapofanya kazi, kiasi cha joto, mwelekeo wa inapokwenda.

Anaongeza kuwa: "Kwa kifupi, FDR ni kama mpelelezi wa kila kinachofanyika ndani ya ndege. Kulingana na aina zake, ina uwezo wa kuhifadhi data kulingana na muda kuanzia saa tano, 10 hadi 25 tangu ilipozimwa na kurudi nyuma."

HISTORIA BLACK BOX

Mugusi anasema kifaa hicho kilianzishwa miaka 69 iliyopita nchini Australia na kwamba kwa kipindi cha miaka miwili kati ya 1952 na 1954, ndege ya kwanza aina ya Jet ikiitwa Comet ilipata ajali na kuua takriban abiria 110.

"Idara ya Usafiri wa Anga ya Australia ilikutana na ndipo mtaalamu Dk. David Warren, akapendekeza kuwekwa chombo cha kurekodi sauti. Hiki kilikuwa kama kinasa sauti 'tape recorder' iliyowekwa ndani ya chumba cha rubani," anasema.

Anaongeza kuwa tangu wakati huo, kifaa hicho kimefanyiwa marekebisho na maboresho mengi hadi kuwa na uwezo mkubwa na weledi katika zama hizi.

"Tunaposema kifaa hiki au black box tunaaminisha vyote viwili, yaani CVR na FDR. Wakati mwingine vinakuwa ndani ya mkusanyiko mmoja ingawa vinafanya kazi tofauti na vinawekwa maeneo tofauti pia," anasema.

Gedeon Mgusi (kulia) akitengeneza ndege. PICHA: MPIGAPICHA WETU

INAENDELEA UK.18

UKURASA 13


SUPA JACKPOT

TZS.1,051,207,683

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Mzee** auawa kikatili, muuaji akutwa akila nyama ya mtu

UKURASA 3



Henry Shekifu Philip Marmo Vian Nchimbi

# Waliokatwa CCM watoa ya moyoni

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akiongoza kikao cha dharura cha Baraza la Mawaziri kilichofanyika Ikulu Chamwino, Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Ripoti ajali ya ndege mwezi ujao

UKURASA 2



## Baba, mwanawe jela kwa dhuluma ghorofa la ndoa

UKURASA 7

MICHEZO MGUNDA AWAVALIA NJUGA KIBU, KYOMBO UK.32 KABWELA UK.7

# Waliotemwa CCM wafunguka

**Na Waandishi Wetu**

WALIOTEMWA kwenye kinyang'anyiro cha nafasi ya wenyeviti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ngazi ya mikoa na jumuiya zake, wamesema wanakubaliana na uamuzi, baadhi wakisema Mungu ndiye hupanga viongozi.

Pia wamesema wataendelea kuwa na imani thabiti na msimamo wa kukitetea chama hicho bila kuchoka.

Kati ya waliotemwa katika kinyang'anyiro hicho ni waliowahi kuwa wabunge, James Lembeli na Henry Shekifu na waziri wa zamani, Philip Marmo.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, aliyeomba kuteuliwa kugombea nafasi ya Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Lembeli alisema, hajapokea matokeo rasmi kutoka mawasiliano ya chama hicho zaidi ya kuona kwenye mitandao ya kijamii.

"Nimeona kwenye mitandao ya kijamii orodha ya majina ya waliopitishwa na ambao hawajapitishwa kugombea nafasi hiyo. Jina langu liwepo au lisiwepo nitaendelea kuwa Lembeli, imani na msimamo wangu utakuwa ule ule," alisema na kuongeza:

"Kuna mtu kaja hapa kunipa pole baada ya kuona mtandaoni namuuliza ya nini, mimi kwenye kugombea kuna mambo mawili upate fursa na kuwaongoza wana CCM na Watanzania kwa ujumla, fursa ninayo maana nimeshawahi kuwa kiongozi na hadi sasa nawawakilisha Watanzania kwenye bodi moja duniani."

**SHINYANGA**

Jana Katibu wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Donald Magesa, alitaja majina ya wagombea wa nafasi ya mwenyekiti yaliyopitishwa na Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, akiwataja waliopitishwa ni Mabala Mlolwa ambaye anatetea kiti chake kwa awamu nyingine, akichuana na Costantine Nkuba na Eneza Kanuya.

**TANGA**

Mkoani Tanga, Henry Shekifu aliyejitosa kwenye kinyang'anyiro hicho kwa mara ya tatu mfululizo na jina lake halikurudi.

Katibu wa CCM mkoani humo, Suleiman Charasi, alisema majina ya wagombea yaliyorudi katika nafasi ya Mwenyekiti ni Mathias Mkingwa, Derrick Kazoba na Rajabu Abdallah (aliyekuwa ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Pangani).

**SINGIDA**

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida, Alhaj Juma Kilimbah ni kati ya wanachama watano ambao majina yao yalikatwa kutetea nafasi hiyo.

Kilimbah aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida kipindi cha 2017 hadi 2022, hajateuliwa na Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa (NEC) kutetea nafasi hiyo.

Katibu wa CCM Mkoa wa Singida, Lucy Boniface, akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu, alisema kati ya wagombea wanane walioomba kuteuliwa kuwania nafasi ya Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida walioteuliwa na NEC ni watatu pekee.

Aliwataja walioteuliwa kuwa ni Yusuph Mwandami, (Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Singida), Martha Mlata (mbunge mstaafu) na Amani Ray ambaye ni mkandarasi.

Baadhi ya wanachama ambao ambao hawakuteuliwa na NEC ni pamoja na Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa, Kilimbah, Katibu Mkuu mstaafu wa Jumuiya ya Wazazi Taifa, Erasto Sima.

Uteuzi wa wagombea wa nafasi za ngazi ya mkoa na Jumuiya za CCM ulifanywa Novemba 13, mwaka huu na kikao cha NEC chini ya Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia Suluhu Hassan.

**KILIMANJARO**

Mwenyekiti wa sasa wa chama hicho mkoani hapo, Patrick Boisafi ni miongoni mwa majina yaliyorudi huku akichuana na Golden Swai na Alphonce Temba.

Boisafi anatetea nafasi hiyo kwa awamu ya pili mfululizo.

Akizungumza kwa njia ya simu, Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, alisema wagombea wawili, Swai na Temba ni mara yao ya kwanza.

**DODOMA**

Katibu wa CCM Mkoa wa Dodoma, Pili Agustino, alitaja walioteuliwa nafasi ya Mwenyekiti kuwa ni Godwin Mkanwa (anayetetea nafasi yake), Adam Kimbisa (aliwahi kuwa Mwenyekiti mwaka 2012 hadi 2017 na Mbunge mstaafu wa Bunge la Afrika Mashariki) na Brigdea Jenerali Augustine Gailanga.

Nafasi ya NEC ni Ismail Jama, Dayana Ngurumo, Ahid Senene, Felista Bura, Donald Mejitii na Nicolaus Haule.

**ZANZIBAR**

Wagombea uwenyeviti wa zamani majina yaliyorudi na mikoa yao ya kichama kwenye mabano ni Talib Ali Talib (Mjini), Muhamed Rajab (Magharib), Iddi Khamis Ali (Kaskazini Unguja), Mberwa Hamad Mberwa (Kusini Pemba) na Yussuf Ali Juma (Kusini Pemba)

**MANYARA**

Simon Lulu ni miongoni mwa walioteuliwa kugombea nafasi ya Mwenyekiti Mkoa wa Manyara akitetea nafasi hiyo kwa mara nyingine, huku akichuana na Mkuu wa wilaya wa zamani, Peter Toima na Fraiten Kwahhison.

Majina ya wagombea ambayo hayakurudi ni Omary Kwaang' na waziri wa zamani, Philip Marmo.

**GEITA**

Walioteuliwa ni Said Karidushi (anayetetea kiti chake), Daud Sunzu, Kasendamila Nabaya na Wanselho Siwale. Kwenye nafasi ya ujumbe wa NEC, waliopitishwa ni Adeline Kabakame, Lameck Mgasha na Evarist Gervas (anayetetea kiti hicho).

**UVCCM**

Vian Nchimbi aliyekuwa anawania nafasi ya Mwenyekiti wa UVCCM alisema vijana wote waliojitokeza kuwania nafasi hiyo, wana sifa zote za kuongoza, hivyo ni muhimu kukubali kuwa ni nafasi inayowaniwa na ni mmoja tu anayetakiwa.

Nchimbi ambaye ni Meneja Miradi wa Kampuni tanzu ya CCM iitwayo Jitegemee Trading akiwa tawi la Dodoma, anasema uamuzi uliofanywa na vikao vya chama ni uamuzi wa wanaCCM wote.

"Pamoja na kwamba tunafanya uchaguzi wa viongozi, lakini Mungu ndiye anayeamua ni nani awe kiongozi na kwa wakati gani, hivyo wale ambao wapependekezwa ni uamuzi wa Mungu pia," alisema Nchimbi.

Alisema anawatakia heri wote waliopendekezwa, kwa kuwa lengo la vikao ni kuhakikisha jumuiya hiyo inasonge mbele na kufika salama kule inakokwenda na kwamba mchato mzima ulienda vizuri.

Japhary Kubecha aliyekuwa anawania nafasi hiyo ndani ya UVCCM, alisema amepokea kwa moyo mkunjufu uamuzi wa vikao vya chama kupendekeza majina mengine ya vijana wanaowania nafasi ya mwenyekiti wa UVCCM taifa huku jina lake likikatwa.

Anasema alikuwa miongoni mwa wanachama 200 waliojitokeza kuwania nafasi hiyo, akisisitiza si busara kulazimisha kuteuliwa.

"Niwapongeza viongozi wa chama chetu kwa busara, hekima, maarifa ya kiuongozi ambavyo wametumia kuteua majina hayo, kwani wanatambua hitaji la kisiasa na hali ya kisiasa tulionayo kwa sasa," anlisema Japhary.

***Imeandikwa na Marco Maduhu (SHINYANGA), Thobias Mwanakatwe (SINGIDA), Hamida Kamchalla, (TANGA), Mary Mosha (MOSHI), Augusta Njoji (DODOMA), Rahma Suleiman (ZANZIBAR), Sabato Kasika (DAR) na Jaliwason Jasson, (MANYARA)**


ANATAFUTWA



JINA: RICHARD WASONGA

Mtajwa hapo juu anatafutwa na Polisi kufuatia taarifa zilizoko kwenye Jalada namba AR/RB/10649/2022

Yeyote atakayemuona au mwenye taarifa ya mahali alipo anaombwa azitoe kituo chochote cha Polisi kwa kutumia RB Namba: AR/RB/10649/2022 au kwa kupiga simu +255 784 812 851 au +255 683 233 721.

117146602


# Ripoti ajali ya ndege mwezi ujao

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BARAZA la Mawaziri limeagiza wataalamu wa ndani na nje ya nchi kushirikiana kufanya uchunguzi wa kujua chanzo cha ajali ya ndege ya Precision Air aina ya ATR42-500 yenye namba ya usajili PW494.

Kadhalika, taarifa ya awali ya uchunguzi itatolewa kwa siku 14 baada ya ajali, ya pili itatolewa baada ya siku 30 na nyingine ndani ya miezi 12.

Ajali hiyo ilitokea Novemba 6, mwaka huu na ilisababisha vifo vya watu 19 na majeruhi 26 baada ya kutumbukia kwenye Ziwa Victoria wakati ikitaka kutua Uwanja wa Bukoba.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo baada ya Baraza hilo lililoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kumaliza kikao chake, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema limepokea taarifa ya awali ya ajali ya ndege hiyo na hatua zilizochukuliwa baada ya ajali.

"Kikao cha Baraza la Mawaziri kimeelekeza wataalamu wa ndani kushirikiana na wa nje ya nchi kufanya uchunguzi wa ajali hii ili kupata chanzo na kutoa mapendekezo ya hatua zinazotakiwa kuchukuliwa baada ya ajali kutokea," alisema.

Hata hivyo, alisema maeneo ya uchunguzi yote yanaainishwa na timu za wachunguzi, taratibu zote za kimataifa ambazo zinaelekeza maeneo yanayopaswa kufanyiwa uchunguzi zinazingatiwa.

Msigwa alisema, Baraza limetoa maelekezo hayo kwa kuzingatia Tanzania imesaini mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo inasimamia usafiri wa anga na hatua zinazopaswa kuchukuliwa baada ya ajali ya anga kutokea.

"Kwa hiyo ni mwendelezo wa kutekeleza makubaliano haya, pia Baraza la Mawaziri limeelekeza vitengo vyote vinavyohusika na kukabiliana na majanga viimarishwe kwa mambo mbalimbali ambayo yatatuwezesha sisi kama nchi kuongeza uwezo zaidi ya tulionao sasa katika kukabiliana na majanga pale yanapotokea."

"Ajali za ndege zinapotokea, zipo hatua tatu zinazofuatwa katika uchunguzi ikianza na timu ya uchunguzi ya ajali ya ndege ambayo inafanya uchunguzi wake na kutoa maelezo ya awali ndani ya siku 14, inafuatiwa na ripoti ya awali ambayo inatolewa ndani ya siku 30 na tutamaliza na ripoti kamili ambayo inatolewa ndani ya miezi 12 baada ya ajali kutokea, hatua hizi zote tayari zimeshaanza," alisema.

Msigwa aliomba wananchi wote kuendelea kuwa watulivu wakati uchunguzi huo unafanyika na baada ya kukamilika watajulishwa.

"Baraza la Mawaziri linawashukuru na kuwapongeza wananchi na wote waliohusika katika uokozi baada ya ajali hii kutokea," alisema.

Katika hatua nyingine, Msemaji huyo alipoulizwa kuhusu ajali za barabarani, alisema kuelekea mwisho wa mwaka kumekuwa na matukio ya ajali na kuwataka watumiaji wa vyombo vya moto kuzingatia sheria za usalama barabarani.

"Kuimarishwa kwa vitengo vya majanga ni pamoja na lililosemwa hivi karibuni ambapo serikali imeanza mchakato wa kutunga sheria ya kusimamia majanga na itafanya mambo mengi ikiwamo kuimarisha vyombo vya kukabiliana na majanga," alisema.

# Aua na kula nyama ya mtu

**Na Grace Mwakalinga,**
SONGWE

MKAZI wa Kitongoji cha Chang'ombe, Kijiji cha Kaloleni wilayani Songwe, Berta Shugha (69) ameuawa kikatili na mwili wake kukatwa vipande vipande huku baadhi ya viungo vikidaiwa kuliwa na muuaji.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Alex Mukama, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na tayari mtuhumiwa wa mauaji hayo amešhakamatwa.

Kamanda Mukama alimtaja mtu anayedaiwa kufanya mauaji hayo ni Lazaro Adamson (40), mkazi wa Kaloleni ambaye anadaiwa kufanya mauaji hayo juzi.

Wakizungumzia tukio hilo, baadhi ya wakazi wa Kitongoji cha Chang'ombe walisema walishtukia kuwapo mauaji hayo baada ya kuona damu kwenye maeneo mengi ya nyumba ya mtuhumiwa, jambo ambalo halikuwa la kawaida.

Jesca Abraham ambaye ni jirani wa mtuhumiwa, alisema baada ya kuona damu kwenye makazi ya Lazaro, walihoji na kujibiwa na mtuhumiwa kuwa alikuwa amechinja mbuzi kwa ajili ya kitoweo chake na alishachemsha kwa ajili ya supu.

Alisema majibu hayo yaliwashangaza kwa kuwa hawakuwahi kumwona mtuhumiwa akifuga mbuzi na zaidi walijua kuwa alikuwa na matatizo ya akili, hivyo waliamua kutoa taarifa polisi ili kujua mbuzi aliyechinjwa alikuwa wa nani.

Jesca alisema kuwa baada ya kutoa taarifa polisi, askari walifika kwenye nyumba hiyo mara moja na kukuta baadhi ya viungo vya binadamu kisha kumkamata Lazaro na kuondoka naye.

Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Simon Simalenga, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema: "Tangu niteuliwe kuwa Mkuu wa Wilaya, hili ndilo tukio baya zaidi kulishuhudia nikiwa kwenye wadhifa huu, ni la ajabu na linasikitisha."

Alisema kuwa baada ya kukamatwa kwa mtuhumiwa, alilazimika kufika kituo cha polisi kumwona aliyetenda ukatili huo na hata kufanya mahojiano naye.

Simalenga alisema kabla ya kufanya mahojiano na mtuhumwia huyo, alikwenda kuuona mwili wa marehemu, akiushuhudia ukiwa umekatwa vipande vipande na baadhi ya viungo havikuonekana eneo la tukio.

Simalenga alisema aliushuhudia mwili wa marehemu ukiwa umekatwa kichwa, kiwiliwili kikiwa kimetenganishwa na kuanzia kiunoni, mikono ikiwa kivyake na nyayo za miguu pia zikiwa kivyake.

Alisema mapaja ya marehemu pamoja na utumbo havikuwapo na mpaka sasa havijaonekana na haijulikani alikovipeleka.

Simalenga alisema kuwa pamoja na madai ya mtuhumiwa kuwa alikula nyama ya marehemu, bado haiwaingii akilini kuwa kwa muda mfupi alikuwa amemaliza kula mapaja yote ya marehemu pamoja na utumbo, hivyo Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo ikiwamo kubaini mahali vilipo baadhi ya viungo vya marehemu ambavyo havionekani.

Mkuu wa Wilaya huyo alisema viungo vya marehemu vilivyopatikana vimehifadhiwa katika Hospitali ya Mwambani.

# Wadau tabianchi wataja njia kukabili uhaba maji

**Na Jenifer Gilla,**
SHARM EL SHE

WADAU wa athari za mabadiliko ya tabianchi kutoka Tanzania, wametaja njia mbalimbali zinatakazosaidia kukabiliana na tatizo linalochangia kuwapo kwa uhaba wa maji nchini humo, ikiwamo kuchimba visima vya kisasa vya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua.

Waliyasema hayo katika Mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Athari za Mabadiliko ya Tabianchi unaoendelea mjini Sharm El She, nchini Misri, jana na ajenda kuu iliyoongelewa ni maji na wanawake.

Mkurugenzi wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Farhat Mbaruk, alisema kuwa kuna haja ya kuja na teknolojia ya kuchimba visima vya kuhifadhi maji ya mvua ambayo yatasaidia watu matumizi ya nyumbani, kilimo na mifugo kipindi cha ukame.

Alisema Zanzibar ni moja ya maeneo wanayotarajia kuanzisha teknolojia hiyo baada ya kina cha maji ya bahari kujaa na kuvamia vyanzo vya maji yaliyokuwa yanatumika kupikia na kunywa na sasa hayafai kwa matumizi hayo.

"Hii ni njia bora tunayoiona kwa sasa na tunataka kuitambulisha huku kwetu na inaratibiwa na Wizara ya Maji kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar, moja ya maeneo ambayo tunataka tuchimbe mabwawa ya kuhifadhi maji kwa ajili ya kilimo ni Bumwini," alisema.

Mtaalamu wa Mabadiliko ya Tabianchi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Pius Yanda, alisema moja ya mikakati mizuri ni kuchukua maji kutoka kwenye maziwa makubwa kama Victoria na kuyaboresha ili yatumike majumbani ingawa gharama zake ni kubwa.

Aliitaja njia nyingine yenye gharama nafuu kuwa ni kutengeneza miundombinu rafiki ya kuhifadhi maji ya mvua katika hali ya usafi ili yatumike kunapokuwa na uhaba.

"Mfano, kandokando ya barabara kunaweza kutengenezwa mitaro ya kuhifadhi majisafi, ambayo yangeweza kutumiwa na wanyama, lakini mfano huohuo tunaweza kuuchukua na kutengeneza mabwawa yatakayohifadhi maji ya kupikia," alisema.

Alisema upatikanaji wa maji umekuwa tatizo kwa sasa kutokana na miundombinu kutoendana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi na kwamba kuna kila haja ya kuliangalia hilo kwa upana.

Mratibu Sekta ya Maliasili na Mazingira, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Hawa Mwechaga, aliitaja njia nyingine kuwa ni serikali kushirikiana na wazawa kutunza vyanzo vya maji ikiwamo mito na maziwa.

Alitoa mfano wa eneo la Mto Malagarasi na TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau wa mazingira wazawa wanaoitwa Tuungane kwa Afya na Mazingira kupanda miti 4,000,000 pembezoni mwa mto huo.

**HALI ILIVYO NCHINI**

Mkurugenzi wa Shirika la Utu na Mazingira, Sara Pima, alisema hali ya upatikanaji wa maji nchini inazidi kuwa mbaya na kuathiri shughuli za kuchumi na kijamii za wanawake na mabinti na kuitaka serikali kuingilia kati.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE**

THE MWALIMU NYERERE MEMORIAL ACADEMY

## MAHAFALI YA KUMI NA SABA (17) KAMPASI YA KIVUKONI NA MAHAFALI YA SABA (7) KAMPASI YA KARUME ZANZIBAR - 2022

Mkuu wa Chuo anawatangazia wanafunzi waliohitimu masomo yao katika mwaka wa masomo 2021/2022 kwamba **Mahafali ya Kumi na Saba** yatafanyika kwenye Kampasi ya Kivukoni, siku ya **Ijumaa tarehe 25 Novemba, 2022 kuanzia saa TATU ASUBUHI (03:00)** na Mahafali ya Saba katika Kampasi ya karume Zanzibar yatafanyika **Jumatatu tarehe 28 Novemba, 2022** kuanzia saa **TATU ASUBUHI.**

**Wahitimu wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:**

1 Kuchukua Majoho kwenye ofisi namba 115 – Jengo la Uhuru **Kampasi ya Kivukoni kuanzia Jumatatu, tarehe 21 hadi Alhamisi, tarehe 24 Novemba, 2022 wakati wa saa za kazi na kwa Kampasi ya Karume-Zanzibar** wafike Ofisi ya PMU kuanzia **Ijumaa tarehe 25 hadi Jumapili tarehe 27 Novemba, 2022 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri. Majoho hayatatolewa siku ya mahafali.**

2. **MALIPO YA MAJOHO NI SHILINGI AROBAINI ELFU NA MALIPO YOTE YAFANYIKE KWA KUTUMIA CONTROL NAMBA.**

3. Majoho sharti yarejeshwe Chuoni kabla ya **tarehe 3 Desemba, 2022 kwa Kampasi ya Kivukoni na Kampasi ya Karume - Zanzibar. Vinginevyo faini ya shilingi 10,000/=** itatozwa kwa siku kwa yeyote atakayechelewa kurudisha joho hilo.

4. Zoezi la namna ya kupokea vyeti **(rehearsal)** litafanyika **Alhamisi, tarehe 24 Novemba, 2022 kuanzia saa 6.00 mchana** katika uwanja wa Mahafali **Kampasi ya Kivukoni na kwa Kampasi ya Karume-Zanzibar** zoezi hilo litafanyika **Jumapili tarehe 27 Novemba, 2022 kuanzia saa 4:00 asubuhi** katika uwanja wa mahafali. **Mhitimu atakayeshindwa kuhudhuria zoezi hilo, hataruhusiwa kushiriki katika Mahafali hayo.**

5. Kila Mhitimu atapaswa kujigharamia usafiri, malazi na chakula.

6. Kusanyiko la wahitimu wote **(CONVOCATION)** waliosoma katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere litafanyika **Alhamisi, tarehe 24 Novemba 2022** katika Ukumbi mpya wa Mihadhara **(NEW LT)** chuoni hapo kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa sita mchana.

7. Washiriki wote wa Mahafali wanatakiwa kuthibitisha ushiriki wao katika Ofisi ya Mitihani kabla ya **tarehe 25 Novemba, kwa kupiga simu namba 0782405552 AU 0767245451**

**Nyote Mnakaribishwa.**

**Mkuu wa Chuo,**
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere,**
**S.L.P. 9193,**
**DAR ES SALAAM.**
**Simu: +255 22 2820041/ 2820045/ 2820047**
**Faksi: +255 22 2820816**
**Barua pepe: rector@mnma.ac.tz**

217145201

RIPOTI MAALUM

# Uhaba wa maji; kitendawili kinachosubiri kuteguliwa

- Wanafunzi wakatisha masomo kutafuta maji
- Mabinti wana kilio chao cha madhila shuleni

**Na Mary Mosha,** aliyekuwa ROMBO

KILIO cha mabadiliko ya tabianchi kinasikika karibu kila kona ya nchi, madhara makubwa yakitajwa kuwa ukame uliosababisha uhaba wa chakula na shida katika upatikanaji wa huduma ya maji.

Kwa wakazi wa Rombo, kilio chao kinaelekezwa katika kile wanachokiita kitendawili cha muda mrefu cha uhaba wa maji, sasa wanalazimika kununua ndoo ya maji yenye ujazo wa lita 20 kati ya Sh. 100 na 500 huku kutokuwa na uhakika wa huduma ya umeme nako kukitajwa kuwa ni sehemu ya kuongeza tatizo.

Miongoni mwa waathirika wa uhaba wa maji ni wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ambao wanalazimika kukatisha vipindi vya masomo na kuutumia muda wa mapunziko kutafuta maji kwa ajili ya shughuli za shule zikiwamo za jikoni.

Katika kufuatilia undani wa madhila hayo, Nipashe inagonga hodi katika Shule ya Sekondari Kirachi na kukutana na mwanafunzi Frank Joseph anayekiri baadhi yao hulazimika kukatiza masomo kwenda kutafuta maji zaidi ya kilomita tatu kutoka shuleni.

"Kuna maji ya kisima cha mtu binafsi, anatuuzia wanafunzi Sh. 100 kwa ndoo, wanakijiji wanauziwa hadi Sh. 500 kwa ndoo. Na hii ni kwa siku ambazo kunakuwa na umeme tu kwa kuwa maji hayo hutumia umeme kuvutwa chini.

"Kutokana na mgawo wa umeme unaoendelea, mara nyingi tunakosa maji ya kupikia na hivyo kushinda njaa. Unakuta nyumbani umelala bila kula maana huku kwetu kwa sasa kuna shida kupata mlo, unapokuja shuleni unategemea upate angalau uji maisha yaende, napo hakuna maji ya kupikia.

"Kwa hiyo, hata kama kuna chakula kipo hapa shuleni, maji yanakwamisha. Upatikanaji wa chakula kwa sasa huko nyumbani ni tatizo kutokana na wazazi kutopata mavuno ya kutosha kwa misimu mitatu sasa," Joseph anafafanua.

### KILIO CHA MABINTI

Happiness Tarimo, mwanafunzi wa shule hiyo, anasema kutokana na kukosekana kwa maji, mabinti hupata matatizo makubwa hasa wanapokuwa wakati wa hedhi.

"Mara nyingi tunajiona wanyonge na kujitenga kutokana na hali ilivyo, hivyo tunaiomba serikali itusaidie tupate umeme wa uhakika utakaotusaidia katika kupata maji hasa nyakati hizi ambazo hatujapata maji ya uhakika," Happiness anawasilisha hoja yao.

Falisiana Tarimo, mkazi wa Rombo, anasema wanatambua kuwapo ukame kumesababishwa na na mabadiliko ya tabianchi, lakini wanaiomba serikali kuwekeza katika uchimbaji wa visima vya maji vitakavyosaidia kupunguza tatizo hilo kwa wanafunzi.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kirachi wakichota maji kwenye kisima kilicho nje ya eneo la shule yao muda ambao walipaswa kuwa darasani wiki iliyopita. **PICHA: MARY MOSHA**

"Hali yetu ni mbaya sana, tunauziwa maji hadi Sh. 500 kwa ndoo, hili ni tatizo kwetu maana kwa sasa hakuna hata vibarua vya kufanya kutokana na hali ya ukame. Bado maji tunauziwa, serikali inataka tufe?

"Tunaomba serikali iache siasa na kutuhudumia, watu binafsi wamepewa vibali wamechimba visima. Kwanini serikali haiwezi? Inatumiza sasa," Falisiana analalamika.

Anna Massawe, Mwalimu wa Shule ya Msingi Kirachi, anawasilisha vikwazo vinavyowakabili ni pamoja na tatizo la ukame uliosababisha ugumu katika kupata huduma ya maji.

"Tatizo la maji si kwa shule tu, bali pia linawaumiza hata walioko nje ya shule. Jamii inategemea maji ya kuchimba, hivyo kila siku inabidi wanafunzi waje na maji kutoka

nyumbani ambako wazazi wao wameshanunua.

"Hii ni kutokana na shule yetu kwa sasa haina maji, zamani bomba lilitosha kutoa huduma ya maji shuleni lakini kutokana na ukame, maji sasa hayatoki.

"Ni maombi yetu kwa Mungu mvua inyeshe ili tupate maji na kuachana na adha hii, wanafunzi wanalazimika kuleta maji kutoka nyumbani ili tuyatumie kwa ajili ya usafi kwenye madarasa na vyoo.

"Tuna tangi la maji ingawa lipo kwenye hali mbaya, tukipata msaada wa ukarabati, litatusaidia kuvuna maji nyakati za mvua" Mwalimu Anna anawasilisha kero zao.

### HATUA ZA UTATUZI

Nipashe pia inatua mezani kwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Msaranga, Fratern Arser anayekiri kijiji chao kukabiliwa na uhaba wa maji.

"Wananchi wanahangaika huku na kule kutafuta maji ambayo huchimbwa ardhini, hatujui hali yake ya usalama, ila tunatumia tukiendelea kumwomba Mungu atuepushe na magonjwa.

"Vyanzo vingi vya maji kwa sasa vimekauka kutokana na ukame, hali inayopelekea maji kupungua na watu kukosa maji. Hata mimi mwenyewe nyumbani kwangu ninanunua maji.

"Nilishawasilisha suala hili kwa ngazi za juu na wataalamu walifika na kufanya tathmini, wakabaini katika Kijiji cha Msaranga na Mahorosha hali ni mbaya zaidi, hivyo walituahidi kuchimbiwa kisima," Arser anasema.

Jukumu la msingi la diwani ni kutetea maslahi ya wananchi anaowawakilisha katika kata husika. Je, madiwani wa wilayani Rombo wanalitekeleza? Diwani wa Kisale

Msaranga, Matius Assenga ana ufafanuzi wa hatua wanazochukua, akitamka:

"Katika kata yangu, kuna shule za msingi sita na za sekondari mbili ambazo zote zinakabiliwa na tatizo hili la uhaba wa maji. Nimeshaiwasilisha kero hii kwenye halmashauri."

Ni uamuzi unaoungwa mkono na kupatiwa ushuhuda zaidi na Msarie Lyimo, Diwani wa Ngoyoni, anayesema tatizo la uhaba wa maji ni kubwa kutokana na ukame, akiitolea mfano kata yake kuwa vyanzo viwili vya maji vya Mhaheni na Ndimira vimekauka na kusababisha wananchi kupata shida kubwa, hasa wanafunzi.

"Kutokana na vyanzo hivyo kukauka, kilio cha shida ya maji kimeongezeka hasa kwa wanawake. Kwa sasa wanatumia maji kutoka bomba kubwa la Marangu, ndilo linalotumika katika tarafa nzima ya Mengwe ingawa haifikishi maji katika maeneo ya ukanda wa chini," Lyimo anafafanua.

Paul Tairo, mfanyabiashara wa maji ukanda wa chini, anasema kwa sasa ananunua maji lita 20 kwa Sh. 200 na kuyauza kwa Sh. 500 huku akilalamikia wateja wengi kukopa na baadhi yao kushindwa kumlipa.

"Tunanunua maji kwa Sh. 200 kwa lita 20, tunatembeza kwa watu binafsi na shule tukiwauzia kwa Sh. 500 kwa dumu la lita 20. Tunakumbana na vikwazo vingi, hasa watu kushindwa kulipa kwa wakati kutokana na ugumu wa maisha,

"Panapotokea msiba au sherehe ndipo tunanufaika kwa kuwa tunaweza kupeleka maji ya Sh. 25,000 hadi 50,000 kwa siku. Tatizo kubwa ni pale umeme unapokatwa.

"Tunachukua maji kwa watu binafsi ambao wamechimba maji yao chini na huvuta kwa kutumia umeme, hivyo kukatika kwa umeme kunasababisha biashara kuwa mbaya na wananchi kuendelea kuteseka zaidi," anasema.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira wilayani Rombo, Martin Kinabo, anataja hatua za kukabiliana na tatizo hilo kuwa ni pamoja na kutekeleza miradi minne itakayosaidia upatikanaji wa maji katika wilaya hiyo.

Anasema kukamilika kwa miradi hiyo kutasaidia vijiji 41 kuwa na uhakika wa kupata huduma ya maji kila siku. Anabainisha kuwa vijiji 18 kwa sasa vina hali mbaya zaidi kutokana na ukame ulioikumba wilaya hiyo na maeneo mengine nchini.

Anasema ujenzi wa mradi wa Wona Marangu hadi tangi la Amboni na mradi wa Njoro II kutoka Rongai hadi Mashati umetengewa zaidi ya Sh. bilioni 6.4 na mkandarasi anaendelea na kazi.

"Pia tumetenga Sh. milioni 30 kwa ajili ya uchimbaji wa kisima kirefu kitakachosaidia vijiji vya Msaranga na Mahorosha ambapo hatua za utangazaji wa zabuni zinaendelea.

"Vilevile, tumetenga Sh. bilioni 1.4 kwa ajili ya uboreshaji wa huduma ya maji katika vijiji vya Holili mjini, Holili vijijini, Mengwe Juu, Ngoyoni, Kelamfua, Ibukoni, Ikuini, Mahorosha na Msaranga," anabainisha mikakati yao.

Mwezi Agosti mwaka huu, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Clement Kivegalo, alitembelea miradi ya maji wilayani Rombo na kuagiza mkandarasi (kampuni ya Best One) anayetekeleza miradi miwili kwa jumla ya Sh. bilioni 5.3 kuikamilisha kwa wakati ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa maji katika wilaya hiyo lililogeuka kuwa kitendawili cha kihistoria.

Weransari Munis, Meneja wa RUWASA Mkoa wa Kilimanjaro, anapotafutwa na Nipashe kuzungumzia utekelezaji wa agizo hilo, anasema tayari mabomba yametandazwa na mradi huo unatarajiwa kukamilika Aprili mwakani.

Mbunge wa Rombo, Prof. Adolf Mkenda akiwa katika ziarani jimboni mwezi uliopita, alilalamika kuchelewa kukamilika kwa mradi mmoja na kuitaka RUWASA makao makuu kuingilia kati ili wananchi wa Rombo wapate huduma ya maji.

# Makalla ataka watupa taka ovyo wazomewe

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amesema licha ya sheria na kanuni kuwadhibiti wachafuzi wa mazingira hususani wanaotupa taka ovyo ni vyema sasa wakazomewa ili waone aibu kwa kosa wanalofanya.

Makalla alitoa kauli hiyo jana wakati wa kikao kazi na viongozi wa wilaya wakiwamo wakuu wa wilaya, wakurugenzi, meya na maofisa mazingira, kilichoketi kuweka mipango bora ya matumizi ya ardhi kulingana mipango miji ya mkoa na mikakati endelevu ya kuimarisha usafi na utunzaji wa mazingira.

Katika kikao kazi hicho kwa pamoja wamekubaliana kuweka nguvu kusimamia mipango miji ya mwaka 2020-2030 kwa kuhimiza utoaji wa vibali vya ujenzi kwa wakati na utekelezaji wa agizo la Wizara ya Ardhi kuhusu usitishaji vibali vya ujenzi wa vituo vya mafuta.

Pia Makalla ameelekeza watendaji kuanzia ngazi ya mtaa kubeba jukumu la usafi kwa kuweka mkazo kwenye kampeni ya usafi kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi na kudhibiti machinga kufanya biashara kwenye maeneo yaliyokatazwa.

Makalla aliwataka makandarasi wa utoaji taka kuhakikisha zinaondolewa kwa wakati na wananchi walipe ada.

Hata hivyo, RC Makalla ameelekeza halmashauri za mkoa huo kuangalia upya utoaji wa mikataba ya muda mrefu kwa makandarasi wa usafi ili waweze kukopesheka na kununua vifaa vya kisasa tofauti na sasa wanapopatiwa mikataba ya muda mfupi.

Makalla alisema amefanikiwa kupata vyombo vya kutupa taka ambavyo amepanga kuvigawa kwenye daladala na vituo vya basi kuanzia jana.

# Kampuni yajitosa uhaba wa maji Dar

**Na Halfan Chusi**

WAKATI uhaba wa maji ukiendelea kutikisa Dar es Salaam na maeneo mengine nchini, Kampuni ya Tamgo Tanzania Limited imeinunua kampuni ya MerryWater ikipanga kuongeza nguvu katika utatuzi wa kero ya maji.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Meneja wa kampuni hiyo, Tarek Mostafa alisema kuwa katika kutatua kero hiyo, moja ya mikakati yao ni kuongeza nguvu ikiwamo kuinunua kampuni hiyo.

"Tunajivunia sio tu kuendelea bali tumedhamiria kuiboresha huduma bora ya maji kwa wateja," alisema na kubainisha kuwa wana vifaa vya kutosha kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa maji, zikiwamo mashine za uchimbaji visima.

Alibainisha kuwa kampuni yao ilikamilisha mkataba wa kumiliki kampuni ya MerryWater tangu Mei Mosi mwaka huu kwa mujibu wa taratibu za kiserikali, inatarajia kuzindua rasmi shughuli zake Alhamisi jijini Dar es Salaam.

Kampuni ya Merrywater ilianzishwa Tanzania mwaka 1987 na kujijengea sifa bora ndani ya sekta ya huduma nchini kwa kipindi cha miaka 35.

Sifa hizo za kutoa huduma bora kwa wateja ndizo zilizoifanya kampuni ya Tamgo Tanzania kuanza mchakato wa kuinunua.

Tamgo Tanzania Limited ni sehemu ya kampuni za Zahid Group iliyoanzishwa mwaka 2020 kama sehemu ya upanuzi wa shughuli zake katika Bara la Afrika.

# TCRA yawezesha vijana wabunifu

**Na Halfan Chusi**

MAMLAKA ya Mawasiliano (TCRA) imewafungulia milango vijana wabunifu katika Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa kuwapa uwezeshaji uliokuwa unakwamisha ubunifu miaka yote nchini.

Uongozi wa mamlaka hiyo umesema unashirikiana na taasisi zingine kuweka mazingira rafiki kwa vijana wabunifu wa TEHAMA kutengeneza fursa za kukuza ubunifu na kuzalisha ajira kwa vijana kwa kuwawezesha vifaa muhimu kama vile kompyuta mpakato na simu ya kiganjani au vifaa.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabir Bakari, alisema jana kuwa serikali imeamua kutoa rasilimali kwa vijana wabunifu katika sekta ya TEHAMA.

Alisema rasilimali za mawasiliano zinazotolewa na TCRA kwa ajili ya vijana wabunifu kufanya majaribio ni pamoja na misimbo ya USSD, yaani rasilimali-namba (namba maalum zinazotumika kumpa mbunifu fursa ya kusambaza teknolojia aliyoibuni ndani na nje ya nchi).

Pia wanatoa kikoa (domain) cha dot tz (.tz) na masafa ya mawasiliano.

Dk. Jabir alisisitiza kuwa vijana wabunifu na wavumbuzi wa programu mbalimbali za kidijitali sasa wanaweza kujitokeza kupata rasilimali hizo zitakazowawezesha kupata fursa ya kutengeneza ajira, kujiletea kipato na kutatua kero mtambuka za jamii.

"Tumejipanga kuhakikisha wabunifu wapya hasa wa sekta ya TEHAMA wanaoweza kutatua kero za jamii yetu wanapata rasilimali hizi za mawasiliano, ili washiriki katika uchumi wa kidijiti," alisema.

Mkurugenzi huyo aliongeza: "Tumeweka utaratibu jinsi ya kusaidia vijana hawa kwa kutoa rasilimali hizi kwa muda wa miezi mitatu baada ya kuidhinishwa na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ambayo hujiridhisha kubaini kama wazo la kibunifu linakidhi kufanyiwa majaribio na hapo ndipo tunatoa rasilimali za masafa au misimbo ya namba fupi kwa muda wa majaribio wa miezi mitatu."


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONYESHA NIA: KUBUNI NA KUTEKELEZA PROGRAMU YA KUREJESHA MBINU ZA KUPATA MAHITAJI YA MAISHA KUPITIA UVUVI NA BAHARI KWA AJILI YA JAMII ZA WAVUVI ZA MKOA WA TANGA.**
**REJEA: 00000027**

EACOP Ltd (Kampuni) Tanzania, kampuni ya mafuta na Gesi, inaalika taasisi zenye uzoefu na sifa kuonyesha nia ya kutoa huduma ya kuandaa, kusimamia na kutekeleza ''Programu ya Kurejesha Mbinu za Kupata Mahitaji ya Maisha Kupitia Kuvua na Uvuvi wa Baharini'' ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na kusafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**
Kituo cha baharini cha Mradi wa EACOP kilichopo katika Rasi ya Chongoleani, kinajumuisha hifadhi ya baharini ya kituo cha mwisho (Marine Storage Facility), gati yenye kilomita 2 na kituo cha kushushia mizigo. Shughuli za uvuvi za jamii za eneo hilo zitaathiriwa na ujenzi na uendeshaji wa gati ambayo inawezekana ikajumuisha eneo hilo kufanywa kuwa ukanda uliotengwa, ambao vyombo vya uvuvi havipaswi kuwepo

Mpango Kazi wa Uhamishaji watu na Makazi (Resettlement Action Plans) wa nyongeza na Programu ya Kurejesha Mbinu za Kupata Mahitaji ya Maisha vimebuniwa na ukusanyaji wa taarifa za ziada unaendelea ili kuifafanua programu zaidi. Mtaa mmoja utaathiriwa zaidi, mtaa wa pili utaathiriwa kiasi na mitaa mingine miwili itaathiriwa.

Kampuni/watoa huduma ya ushauri/taasisi ya wataalamu, inahitajika kufanya ubunifu wa kina na kutekeleza programu ya uvuvi/Programu ya Kurejesha Mbinu za Kupata Mahitaji ya Maisha Kupitia bahari ikijumuisha ketengo kinacholenga kaya zilizoguswa na mradi na kitengo kinacholenga jamii nzima

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**
Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

1. Uthibitisho wa usajili kama shirika/taasisi ambayo shughuli zake zinahusiana na utekelezaji wa programu za uendelezaji uvuvi, programu za uvuvi za kijamii na mbinu za kupata mahitaji ya maisha kupitia baharí (mfano kukusanya mazao ya baharí, kuvua, nakadhalika) ndani ya Tanzania
2. Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
3. Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa kutekeleza programu za uendelezaji uvuvi, programu za uvuvi za kijamii na mbinu za kupata mahitaji ya maisha kupitia baharí (mfano kukusanya mazao ya baharí, kuvua, nakadhalika) na uzoefu wa kufanya kazi na jamii zinazotegemea mbinu za kupata mahitaji ya maisha kupitia baharí.
4. Mifano ya kazi zinazoonyesha uzoefu wa kufanya kazi zinazofanania na hizo zilizofanywa kipindi cha karibuni, ndani miaka mitano iliyopita toka siku ya tangazo hili
5. Wafanyakazi wataopendekezwa kufanya kazi kwenye mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
6. Uthibitisho wa kusajiliwa ndani ya kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi au udhibitisho kuwa wa maombi ya kusajiliwa katika kanzi data yameidhinishwa wakati wa kuwasilisha ombi la kuonyesha nia.
7. Mwombaji azingatie Kanuni ya Sekta ya Petroli ya Ushirikishwaji wa Wazawa/Ufafanuzi wa Kampuni ya Ndani

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe **20 Mb**) saa au kabla ya **saa tisa mchana saa za Afrika Mashariki** (EAT) tarehe **23 Nov. 2022.** Kichwa cha barua pepe kiwe ni **00000027.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

217142402

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mkidanganya mitihani mnaiangamiza Tanzania

**OKTOBA** ulikuwa mwanzo wa kipindi cha miezi miwili cha mitihani ya darasa la nne, la saba, kidato cha pili na sasa kidato cha nne.

Jukumu hilo linazihusu shule za msingi na sekondari na sasa mtihani ni ya kumaliza elimu ya sekondari.

Hata hivyo, moja ya tatizo kubwa sekta ya elimu ni udanganyifu wa mitihani. Ni kawaida kusikia Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) likitangaza kuwatuhumu walimu, wakuu wa shule, wanafunzi na wasimamizi pamoja na kufuta matokeo ya shule au vituo kadhaa kwa sababu za udanganyifu na utovu wa nidhamu katika mitihani ya sekondari na msingi.

Tunaona kuwa shinikizo la kutaka watoto wafanye vizuri hata kama hawana uwezo linawaweka walimu, wazazi, walezi na wasimamizi wa shule mara kadhaa kwenye kuhusishwa na udanganyifu wa mitihani kwa wanafunzi wao.

Hitaji hilo au shinikizo kutoka kwa wazazi, walimu kwa watoto kupata alama bora za juu na kuleta sifa kwa shule limekuwa jambo muhimu katika kuchochea tabia mbaya za wizi na udanganyifu wa mitihani.

Aidha, hatukosoi lakini tunazifahamu na kuzifuatilia juhudi za kurekebisha mitaala ndipo tunapopata uthubutu wa kusema kuwa mfumo wa sasa wa elimu unaonekana kusisitiza madaraja kwa kutizama (kufaulu kwa mitihani) ukichukuliwa kama jambo la sifa badala ya kutoa maarifa.

Tunajua kuwa zipo shule zinazolenga kupata alama nzuri za juu tena kuwa bora ili kuvutia wanafunzi zaidi na kujipatia fedha kutokana na utitiri wa watakaojiunga nazo na hivyo kupata mapato ya ziada.

Lakini, tunazidi kusisitiza kuwa mitihani ya udanganyifu inabakia kuwa tabia mbaya yenye madhara ya muda mrefu kwa watu binafsi na nchi, ni kuzalisha mbumbumbu na kujidanganya kuwa wewe ni bora wakati ukweli ni huna uwezo.

Tanzania inakabiliwa na changamoto za watumishi wa umma na wafanyakazi wanaotokana na maadili mabovu, wasio na uadilifu na pia mafisadi yote hayo ni matokeo ya kuwa na mienendo ya kukosa uaminifu kuanzia kwenye mitihani na uongo kwenye mitindo ya maisha.

Ukweli ni kwamba huwezi kuwa raia mwadilifu kama unatokana na kuanza kudanganya mitihani ukiwa mwanafunzi wa shule ya msingi, ukazidi kuharibu ukiwa kidato cha nne, sita na hata vyuo vikuu. Wewe si raia mwema wala mwadilifu.

Tunawakumbusha wazazi, walezi, walimu, wamiliki wa shule na wasimamizi kuwa ufike kipindi waache tabia mbaya ya wizi kwa vile mwizi au mharibifu, hatarajiwi baadaye maishani abadilike na kuachana na mienendo hiyo mibovu ambayo ndiyo msingi wa maisha yake.


Tunaona kuwa kuanza kudanganya mitihani ili upate fedha kwa wazazi na walezi na shule yako ionekane kidedea ni kupanda mbegu mbaya kwa Watanzania, ambayo inaharibu ustawi wa taifa kwa miongo mingi.

Tunaikumbusha NECTA, serikali, shule binafsi na za umma, walimu, wasimamizi, watahiniwa, walezi, wazazi, walimu na wasimamizi kuwa njia mbaya siku zote huishia katika matokeo mabaya.

Kama tunaandaa wasomi ili wawe rasilimali watu kwa njia mbaya za wizi, hawatakuwa waaminifu wala watiifu na nchi haiwezi kuendelea kwa sababu masuala ya kutokuwa na taaluma bora zilizotokana na rushwa yataangusha juhudi zote chanya ambazo taifa linawekeza ili kufikia maendeleo endelevu.

Ni wakati wa kuwa na taasisi ya kupambana, kuchunguza, kukomesha rushwa kwenye mitihani ili Tanzania iondoke kwenye shimo la maangamizo linalotokana na kuwa na wasomi, viongozi na nguvukazi iliyozalishwa kwa njia ya wizi na udanganyifu wa mitihani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongereni fomu 4, msiibe mitihani

**WATAHINIWA** 566,840 nchi nzima, walianza mtihani kidato cha nne jana, huku Baraza la Mitihani la Tanzania -NECTA likitoa onyo kwa wanafunzi watakaojihusisha na udanganyifu katika mitihani hiyo.

Baraza linatoa onyo hilo kutokana na ukweli kwamba, kumekuwapo na tuhuma za wizi wa mitihani ambao imekuwa ikijitokeza kila mwaka kwenye baadhi ya shule za msingi sekondari zikihusisha wanafunzi na walimu.

Ninadhani wanaojihusisha na wizi huo, wangeachana nao, kwani mtihani huo ni muhimu kwa wanafunzi na jamii, unapima umahiri wa wanafunzi katika masomo yote waliyojifunza kwa miaka minne.

Baada ya mtihani, matokeo yake yanatumika katika uchaguzi wa wanafunzi wanaojiunga na elimu ya juu na fani mbalimbali, hivyo ni muhimu ufaulu wao ulingane na uwezo wao wa darasani.

Ikumbukwe, wizi wa mitihani umekuwapo muda mrefu na unagharimu mustakabali wa maisha ya wanafunzi kutokana na adhabu zinazotolewa na NECTA kila mara yanapotangazwa matokeo.

Adhabu yenyewe ni kufutwa kwa matokeo ya mtihani kwa shule nzima, badala ya kutoa adhabu aidha kwa wanafunzi waliothibitika kufanya udanganyifu huo kwa lengo la kufaulu.

Hivyo, wale waliojiandaa kwa wizi au udanganyifu katika mtihani huo, ni vyema wasiwaponze wenzao, badala yake kila mwanafunzi atumie maarifa aliopewa na walimu kwa miaka minne aliokuwa shuleni.

Udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani kwa ngazi zote haukubaliki, ni vyema hatua zichukuliwe kwa wahusika, ingawa bahati mbaya wakati mwingine hata wasiohusika hujikuta wakihukumiwa.

Niwakumbushe tu wale wenye nia ya kuiba mitihani kwamba, wanawaponza wenzao hasa pale baraza linapoamua kufutia shule matokeo na kumbe walioshiriki katika wizi na udanganyifu ni wachache.

Ninadhani umefika wakati sasa mtindo wa kufutia matokeo shule nzima kama adhabu kwa wizi wa mitihani, iwe ni kwa wahusika tu, kwani sidhani kama inawezekana wanafunzi wote wakafanya udanganyifu.

Kwa ujumla linapozungumzia suala la udanganyifu, wizi au kuvuja kwa mitihani, huo ni mnyororo mzima wa udanganyifu unaohusisha hata baadhi ya wasimamizi wasio waaminifu na wenye tamaa ya fedha.

Wakati mwingine hata wamiliki wa shule au yeyote anayetengeneza mazingira ya wanafunzi kufanya udanganyifu ndani ya chumba cha mtihani. Hiyo ni kwa kuonyeshana majibu au maswali kufanyika nje ya chumba cha mtihani.

Lakini baadhi ya wamiliki au viongozi wa shule huwa wanatuhumiwa kushawishi wasimamizi kuhusika kufanya udanganyifu, ambapo ukiangalia utabaini kuwa sababu zote hizo haziwahusishi wanafunzi moja kwa moja.

Jambo la kusikitisha ni kwamba, athari za uamuzi wa kuwafutia zinawakumba wanafunzi moja kwa moja, hatua ambayo kwa namna moja au nyingine inaweza kuharibu malengo yao ya baadaye.

Pamoja na yote hayo, jambo la muhimu kutambua ni kwamba wizi haufai katika mitihani, badala yake mwanafunzi anatakiwa kutumia akili yake itakayomwezesha kusonga mbele kielimu.

Siyo siri kwamba, mwanafunzi anaweza kukwepa katika masomo iwapo atakuwa amefaulu kwa udanganyifu kwani sidhani kwamba huko anakoelekea ataendelea kuwa na watu wa kumbeba kwenye mitihani.

Mtindo huo wa wizi wa mitihani unaweza kulifanya taifa likawa na wasomi wasio na manufaa katika jamii au kwa nchi yao, kwa kutokuwa na weledi wa kutosha kuhusu fani na ujuzi wa aina mbalimbali.

Hivyo ni vyema wanafunzi wakaachwa wafanye mitihani, wafaulu kulingana na uwezo wao wa darasani, si kwa njia hizo ambazo zinaweza kuwaingiza kwenye matatizo na kusababisha kufutiwa matokeo.

Niwatakie kila la heri wanafunzi mnaofanya mtihani wa kidato cha nne, lakini mjaribu kuepuka njia zozote za udanganyifu na wizi wa mitihani, kwani ni sawa na kujiharibia.

HABARI KITAIFA

## Askofu ataja kiini matukio ya ukatili

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

ASKOFU wa KKKT Dayosisi ya Kusini Mashariki-Mtwara, Lucas Mbedule, amekemea migogoro ya ndoa, akiitaja ni chanzo cha kushamiri vitendo vya ubakaji, ulawiti na unyanyasaji wa kijinsia.

Amesema ili kudhibiti matukio hayo yanayoripotiwa kwa wingi kwa sasa, kuna haja wazazi kujikita zaidi katika kusoma neno la Mungu.

Aliyasema hayo mjini Masasi juzi wakati wa ibada ya Jumapili iliyoambatana na ubatizo na uzinduzi wa kanisa jipya la KKKT Masasi.

Alisema jamii ya sasa imekuwa na vitendo vibaya ambavyo havimpendezi Mungu, akiwa na ufafanuzi kwamba vinajitokeza kutokana na baadhi ya watu kutolijua neno la Mungu.

Alisema uovu ambao umekuwa ukitokea duniani kwa kiasi kikubwa unachagizwa na migogoro kati ya wazazi, yaani ndani ya ndoa ambapo baadaye hutengeneza kizazi kilichokosa maadili.

Askofu huyo alisema jamii yenye maadili inatokana na malezi ya wazazi pamoja na uadilifu, hivyo wazazi wakikosea katika kumlea mtoto, basi mtoto huyo inakuwa vigumu kuja kuwa mtu mwadilifu katika jamii.

Askofu Mbedule alisema kama jamii ingekuwa na utamaduni wa kusoma neno la Mungu na kulielewa vizuri, vitendo vyote vya kumkosea Mungu ambavyo vimeshamiri ndani ya jamii kama vile ubakaji, ulawiti na unyanyasaji vinavyotea hivi sasa, visingetokea.

Alisema kwa sasa jamii inashuhudia vitendo hivyo kwa sababu ya baadhi ya watu hawana hofu ya Mungu, hivyo kuamua kufanya vitendo kama hivyo kwa kuangalia maslahi yao ya kibinadamu.

Askofu Mbedule alisema viongozi wa dini wanakasirishwa na vitendo vyote ambavyo vinaendelea kutokea nchini vya kumkosea Mungu na watasimama kuhubiri neno la Mungu ili kila mmoja katika jamii aone vitendo hivyo havipaswi kufanywa.

"Kuwapo vitendo visivyompendeza Mungu ni wazi kabisa vinatokana na baadhi ya jamii kutomrudia Mungu. Tuache hivi vitendo havimpendezi Mungu, hebu tusome neno la Mungu na kulielewa ili tuwe na hofu na Mungu," alisisitiza.

Askofu Mbedule alisema baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa sehemu ya jamii inayofanya maovu na kuchangia kuwapo watoto kushiriki katika vitendo hivyo, akiwataka kufanya ibada na kutubu dhambi zao.

Isabela Mwakaluka, mmoja wa waumini wa kanisa hilo, alisema wazazi na walezi wanapaswa kuwa mfano bora kwa watoto kwa kumcha Mungu na kukemea matendo maovu.




Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omary Mgumba akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kulia), baada ya ufunguzi rasmi wa semina kwa wateja wa benki hiyo Mkoa wa Tanga iliyofanyika hoteli ya Regal Naivera jijini humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Baba na mwanawe jela kwa uongo nyaraka kesi ya ndoa

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imemhukumu Samson Muze na mtoto wake, Tuwaha Muze (44) kifungo cha miaka minne na nusu jela baada ya kupatikana na hatia ya kughushi makubaliano na kuwasilisha nyaraka za uongo za mwenendo wa kesi ya ndoa.

Hata hivyo, mahakama hiyo pia imemhukumu Samson kifungo cha nje cha mwaka mmoja baada ya kuzingatia maombi yake ya ugonjwa na umri mkubwa.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Romuli Mbuya baada ya mahakama kuridhika na ushahidi wa mashahidi wanne wa upande wa mashtaka ambao ulithibitisha mashtaka dhidi ya washtakiwa bila kuacha shaka.

Hakimu Mbuya alisema Muze atatumikia kifungo cha jumla ya miaka saba jela, ambapo kila kosa atatumikia miaka mitatu na nusu na hivyo adhabu yake itakwenda sambamba. Kwa mantiki hiyo, mshtakiwa huyo atatumikia kifungo cha miaka mitatu na nusu gerezani.

Mbuya alisema kwa upande wa mshtakiwa wa pili (Samson), amepatikana na hatia ya kughushi makubaliano ya uongo, lakini kutokana na maombi yake ya ugonjwa na umri mkubwa, mahakama imemhukumu kifungo cha nje cha mwaka mmoja.

Hata hivyo, kwa kipindi hicho mahakama imemtaka kutokutenda kosa lolote la jinai ndani ya muda huo, akitiwa hatiani kwa kutaka kumdhulumu nyumba ya ghorofa moja mkwe wake, Maimuna Soka kwa kushirikiana na mtoto wake, Tuwaha.

Kabla ya kutolewa hukumu hiyo, Wakili wa Serikali Tumaini Mafuru aliomba mahakama itoe adhabu kali dhidi ya washtakiwa hao ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia hiyo.

Baada ya Mafuru kudai hayo, Tuwaha kupitia wakili wao, Alexander Mzikila aliomba wapunguziwe adhabu kwa kuwa ana mke na watoto wanne wanaomtegemea, huku Samson akiiomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa ni mgonjwa.

Maimuna alidai kuwa Julai 2017, alisafiri kikazi kwenda mikoa ya Lindi, Mtwara na Songea na aliporejea Dar es Salaam, alifika majira ya saa tisa na kuelekea nyumbani kwake Mbezi Luis.

Alidai alipofika nyumbani kwake, alikuta nyumba yake imebadilishwa vitasa na watoto wake wawili nao walihamishwa kutoka katika nyumba hiyo kwenda kwa wazazi wa mume wake huku mlinzi aliyekuwa analinda nyumba yao, akimkatalia kuingia ndani ya nyumba yake.

Washtakiwa hao wanadaiwa kughushi makubaliano ya uongo ya upangaji wa nyumba ya ghorofa moja iliyoko Mbezi Luis, wakionyesha kuwa nyumba hiyo ni mali ya Samson wakati wakijua kuwa ni uongo na nyumba hiyo ni mali ya Maimuna Soka na aliyekuwa mume wake, Tuwaha Muze.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Auawa kwa kuchomwa kisu

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MKAZI wa Azimio, Kata ya Kihonda, Manispaa ya Morogoro, Henry Charles (45), ameuawa kwa kuchomwa kisu na watu wasiojulikana waliovamia nyumbani kwake kwa lengo la kuiba.

Kamanda wa Polisi Mkoa Morogoro, Fortunatus Muslimu, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo majira ya saa nane usiku, akieleza kuwa watu hao wasiofahamika, walivamia nyumbani kwa Charles na kwenda moja kwa moja chumbani kwake.

"Walifikia moja kwa moja chumbani kwake na kumtoa kisha kumpeleka sebuleni na mmoja kubaki chumbani ambapo mtu huyo alimlazimisha mke wa Henry kukabidhi suruali aliyokuwa amevaa mumewe siku hiyo," alisema Musilimu katika mazungumzo na Nipashe jana.

Alifafanua: "Baada ya kubaini katika suruali hiyo hakukuwa na fedha, mtu huyo alikwenda chumba cha binti wa mkazi huyo na kumwamuru ampe simu yake na baada ya kuchukua walimchoma kisu shingoni Charles na kutoweka na simu walizochukua katika nyumba hiyo bila kuiba kitu kingine."

Kamanda Musilmu alisema kuwa mke wa Charles alipiga kelele za kuomba msaada baada ya watu hao kuondoka na kwamba licha ya kumfikisha mumewe hospitalini, alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro.

Alisema wanaendelea na uchunguzi zaidi wa tukio hilo japo uchunguzi wao wa awali unaonyesha watu hao walikuwa wakifahamiana na marehemu enzi za uhai wake kutokana na mwenendo mzima wa uingizaji ndani ya nyumba hiyo na moja kwa moja kufikia chumbani kwa mmiliki.

Kamanda huyo alisema uchunguzi wa awali umebaini siku ya tukio, Charles alisikika akiongea kwa simu ya mkononi na kuagiza fedha zake ziwekwe sheli kwa kuwa tayari alishafika nyumbani.

Alisema polisi wanaendelea na msako kuwabaini watu hao ili hatua zaidi za kisheria zichukuliwe dhidi yao.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi ya Uongozi, Balozi Dk. Ombeni Sefue (kushoto), akimsikiliza Kaimu Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Dickson Richard, wakati wa uzinduzi wa Kigoda cha Utafiti cha Mkapa uliofanyika jijini Mwanza na kudhaminiwa na NMB. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yadhamini kongamano Kigoda cha Utafiti cha Mkapa

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

BENKI ya NMB imepongeza uanzishwaji wa kongamano la Kigoda cha Utafiti cha Mkapa liliofanywa na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino (SAUT), ili kuenzi uzalendo na utumishi mwema wa Rais wa awamu ya tatu, Hayati Benjamin Mkapa.

Kaimu Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Dickson Richard, alitoa pongezi hizo wakati wa uzinduzi wa kigoda hicho katika Kampasi ya Mwanza ya SAUT.

Richard alisema kuwa katika uzinduzi wa Kigoda cha Mkapa benki yao imeshiriki katika kuenzi kumbukumbu za kuzaliwa kwake. Alisema wako katika kuwekeza na kufanya ushirikiano na jumuiya kama SAUT katika kuboresha yaliyofanywa na waasisi wa nchi.

"Benki ya NMB ni zao la sera ya ubinafsishwaji ya Hayati Rais Benjamin Mkapa. Hivyo, Rais Mkapa ni chachu ya hatua zote kubwa ambazo NMB imekuwa ikizipiga na hata kukua na kuwa benki kubwa kama ilivyo sasa," alisema Richard.

"Hayati Mkapa alikuwa kiongozi aliyekuwa anasaidia watu wa kipato cha chini, na sisi kama benki tunathamini jamii zilizotuzunguka na kutatua kero zinazowakabili hususani katika sekta za elimu na afya.

"Na kwa mwaka huu wanafunzi 100 watapatiwa ufadhili wa masomo ya chuo kikuu kupitia programu yetu ya NMB Nuru Yangu Scholarship," alisema Richard.

Makamu Mkuu wa SAUT Kampasi ya Mwanza, Prof. Costa Mahalu, aliishukuru NMB kwa kudhamini kongamano hilo.

Prof. Mahalu alisema Hayati Mkapa alichangia kwa asilimia kubwa upatikanaji wa mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi wa vyuo binafsi. Alisema Hayati Mkapa pia aliisaidia SAUT kupatiwa eneo la kujenga chuo kikuu hicho mkoani Mwanza.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi ya Uongozi, Balozi Dk. Ombeni Sefue, aliwataka Watanzania kujenga utaratibu wa kujisomea vitabu ikiwa kama sehemu ya kumuenzi Hayati Mkapa.

"Watanzania inatakiwa tusome vitabu katika kumuenzi Hayati Benjamin Mkapa na ukiwa kiongozi, usomaji wa vitabu unaweza kukusaidia na kuwa mshauri wako mkubwa," alisema.

Aliwataka Watanzania kusoma vitabu na wasisome tu kwa kuwa wanataka kuwa viongozi. Alisema marais wastaafu Ali Hassan Mwinyi, Hayati Benjamin Mkapa na Hayati Julius Nyerere walikuwa waumini wakubwa wa kusoma vitabu.

Balozi Dk. Sefue aliwataka wanafunzi wa SAUT wasisome kufaulu mitihani tu, bali wasome kupanua upeo wa kujua mambo mengi zaidi.

Mke wa Hayati Mkapa, Anna Mkapa alisema Hayati Mkapa alitumia vitabu katika kuongoza taifa letu na alipenda kujifunza kupitia vitabu na kuandika hotuba kwa kutumia vitabu.

Aliwataka Watanzania wote waendelee kumwombea Rais Samia Suluhu Hassan katika kuijenga Tanzania mpya.

# Wawasilisha ombi serikalini kujengewa shule ya sekondari

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

KATA ya Mkange katika Halmashauri ya Chalinze wilayani Bagamoyo inahitaji shule ya sekondari ili kuwaondolea kikwazo wanafunzi kukatisha masomo kutokana na kutembea umbali mrefu kuifikia shule ilipo.

Imeelezwa kuwa kwa sasa kata hiyo ina shule moja iliyoko Matipwili ambako wanafunzi wanaotoka maeneo ya Mandamazingara wanalazimika kutembea umbali mrefu kuifikia shule hiyo na hakuna usafiri wa uhakika.

Diwani wa Mkange, Mohamed Gelegeza, katika mazungumzo na Nipashe jana, alisema kutokana na hali hiyo wazazi wanalazimika kutoa fedha kwa ajili ya bodaboda.

Gelegeza alisema hali hiyo imesababisha baadhi ya wanafunzi kukatisha masomo kutokana na kushindwa kutembea umbali mrefu kila siku na wazazi kutomudu gharama hizo za usafiri.

Diwani huyo alibainisha kuwa kwa mwaka 2019, wanafunzi 72 kati ya 129 walihitimu masomo huku 57 wakiacha shule kutokana na shida hiyo.

Alisema kwa sasa wamepata eneo kwa ajili ya ujenzi wa shule na maandalizi ya awali yanaendelea, akiwaomba wadau wa elimu kujitokeza kusaidia ujenzi huo utakaowawezesha watoto wengi kusoma.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chalinze, Hassan Mwinyikondo, alisema vikwazo katika sekta ya elimu vinaendelea kutatuliwa kwa kila kata kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi kupata elimu karibu na maeneo wanayoishi.

Mwinyikondo alibainisha halmashauri hiyo imepokea Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 60 vya madarasa ambavyo vitawezesha wanafunzi watakaochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwakani kupata nafasi ya kudahiliwa.

# HABARI KITAIFA

## RAS aagiza kupima ubora wa chumvi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IRAMBA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Singida, Dorothy Mwaluko, amewaagiza maofisa afya na lishe mkoani hapo kutembelea mashamba yote ya chumvi yaliyoko Singida na kupima chumvi inayovunwa ili kuona kiwango cha madini joto yaliyomo.

Alitoa agizo hilo juzi alipotembelea mashamba ya chumvi yaliyoko Sekenke, Kijiji cha Nkonkirangi wilayani Iramba ili kuona kiwango cha madini joto yanayopatikana katika bidhaa hiyo.

Katika ziara hiyo, wataalamu wa afya na lishe walipima chumvi na kubaini ina kiwango kidogo cha madini joto ndipo katibu tawala huyo alipotoa maelekezo kwa wataalamu hao kuyafikia mashamba yote ya chumvi na kupima viwango vya madini joto na kuwataka kuweka mpango wa kuongeza madini hayo kabla ya kumfikia mlaji.

Mwaluko aliwataka wataalamu hao kuanza kutoa elimu kwa wanunuzi wa chumvi hiyo kuhusu umuhimu wa madini joto katika mwili wa mwanadamu.

Alisema wanunuzi ndiyo watakaosaidia kuwaelimisha wateja wao kulingana na bidhaa watakayoihitaji.

Kaimu Ofisa Lishe wa Mkoa Singida, Christowela Barnaba, alisema bidhaa hiyo ni muhimu kuongezwa madini joto ili kuepuka kupata ugonjwa wa goita, jambo ambalo linaweza kugharimu maisha ya mlaji.

Alisema pamoja na kukutana na wanunuzi wao, wataendelea kutoa elimu kwa wavunaji na wachuuzi pamoja na viwanda kuhakikisha wanauza chumvi ambayo ina kiwango cha kutosha cha madini joto.

Ofisa Afya wa Mkoa wa Singida, Mgeta Sebastian, alisema mwananchi anahitaji kuwa na afya bora itakayomsaidia kuzalisha mali na kuongeza kipato, akionya kuwa ukosefu wa madini joto unaweza kusababisha kipato kinachopatikana kutumika kutibu maradhi.

Mgeta aliwashauri wavunaji chumvi hao kutazama afya zao kabla ya biashara na kuondoa imani potofu kwamba chumvi ikiongezwa madini joto, inabadilika rangi na wateja watakataa.

# 31,905 wajitokeza kuchanja kujikinga dhidi ya UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

WATU 31,905 wamejitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19 kisiwani Pemba, baada ya kuhamasishwa na kupewa elimu ya kujikinga na ugonjwa huo unaoendelea kuitesa dunia.

Kampeni ya chanjo hiyo inaendeshwa na Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, Amref, Akros, Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Watoto na Watoto (UNICEF) na Shirika la Chakula Duniani (WFP).

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa chama hicho, Seku Kasuga, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam juzi alipokuwa akizungumza na gazeti hili kuhusu maendeleo ya kampeni hiyo.

"Hadi sasa tangu kampeni ilipoanza mwezi uliopita, tayari watu 31,905 kutoka maeneo mbalimbali ya kisiwa cha Pemba wameshachanjwa. Tunaendesha kampeni kwa ufadhili wa Taasisi ya Mastercard Foundation kupitia CDC Africa," alisema Seku.

Alifafanua kuwa kampeni hiyo inayohusisha elimu na uhamasishaji wa chanjo ni ya mwaka mmoja na itaendelea hadi Septemba mwaka ujao, kwenye kanda ya Zanzibar na baadhi ya mikoa ya bara.

"Lengo ni kufikia hitaji la nchi la asilimia 70 la waliochanjwa katika mkakati wa kutokomeza Covid-19. Hivyo mradi huu utakaodumu hadi Septemba 2023, unaendelea kutekelezeka katika mikoa ya Iringa, Songwe, Simiyu, Rukwa, Mwanza, Katavi, Kagera na Tabora," alisema.

Seku alisema kwa kipindi kifupi, Chama cha Msalaba Mwekundu, kimefanya kampeni kubwa kwa kushirikiana na wadau wake na ana uhakika watu wengi zaidi watajitokeza kupata chanjo.

"Wito wetu kwa Watanzania kwa ujumla ni kwamba, kila mmoja achukue hatua ya kupata chanjo ya corona, Rais wetu Samia alionyesha njia, nasi tufuate nyuma ili kutumiza lengo la serikali la kutaka wetu wapate huduma hiyo kwa ajili ya usalama wa afya zao," alisema.

Alisema serikali inaendelea kuhimiza watu kujitokeza kupata chanjo hasa wale walio katika hatari zaidi ya kupata ugonjwa huo kama magonjwa sugu, shinikizo la damu, kisukari, saratani, UKIMWI na mengine wakiwamo pia wazee.

Kampeni ya chanjo ya UVIKO-19, ilizinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Julai mwaka jana na serikali imelenga kufikia asilimia 70 ya watu waliochanja ifikapo Desemba, mwaka huu, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa dunia wa kupambana na ugonjwa huo.



Meneja Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Absa Tanzania, Beda Biswalo (katikati), akipokea tuzo ya Benki Bora Kimataifa kwa kutoa Huduma Bora kwa Wateja kwa kundi la benki kubwa kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kilombero Sugar, Guy Williams, jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Ofisa Mkuu wa TEHAMA Absa, Emmanuel Mwinuka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wauza korosho kwa 1,875/-

**Na Stevie Chindiye,**
TUNDURU

WAKULIMA wa korosho wilayani Tunduru mkoani Ruvuma wameuza korosho zao kwa bei ya Sh. 1,875 katika mnada wa kwanza wa zao hilo msimu huu wa 2022/23.

Wakulima hao waliridhia kuuza korosho hizo katika mnada ambao ulifanyika katika Chama cha Msingi Namitili Amos, Tarafa ya Nakapanya wilayani hapo.

Katika mnada huo, jumla ya wanunuzi 18 walijitokeza kuomba kununua korosho hizo, bei ya juu ikiwa ni Sh. 1,905 na bei ya chini Sh. 1,862.

Awali, Meneja Shughuli wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Wilaya ya Tunduru (TAMCU), Marselino Mrope, alisema kuwa katika mnada huo kulikuwa na kilo 2,150,997 zilizowekwa mtandaoni kwa ajili ya kuuzwa. Meneja wa Bodi ya Korosho Tawi la Tunduru, Mokiwa Shauri Ally, aliwaambia wakulima hao kuwa katika msimu huu serikali imetoa maelekezo ya kutumia mfumo wa kutumia sanduku na kutoa nafasi kwa wanunuzi walioko nje ya nchi kushiriki.

Mokiwa pia alitumia nafasi hiyo kuwataka wanunuzi wa korosho kuzingatia maelekezo yanayotolewa na viongozi wanaosimamia shughuli hizo yakiwamo yanayowataka kuandika barua moja.

Awali Ofisa Ushirika Wilaya ya Tunduru, George Bisani, aliwataka viongozi wa vyama vya msingi na chama kikuu kufanya kazi zao kwa uaminifu na kutochelewesha malipo ya wakulima baada ya fedha kutoka kwa wanunuzi kuingia kwenye akaunti za vyama.

Akifunga mnada huo, Makamu Mwenyekti wa TAMCU, Mussa Manjaule, aliwataka wakulima kukumbuka kulipa madeni ya pembejeo walizokopa katika taasisi za kifedha ili kulinda uaminifu wao kwenye taasisi hizo ikizingatiwa msimu huu korosho 'zimewapiga chenga' wakulima wengi.

# Walia kunyimwa ajira za SGR

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

BAADHI ya wakazi wa Halmashauri ya Itigi wilayani Manyoni mkoani Singida wamelalamika kutopewa ajira katika mradi wa ujenzi reli ya kisasa (SGR), wakidai kipaumbele kimetolewa kwa watu kutoka nje ya halmashauri hiyo.

Waliwasilisha malalamiko hayo kwa Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Rahabu Mwagisa, juzi wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Songambele, Kata ya Tambukareli, Halmashauri ya Itigi.

Wananchi hao wakiwamo, Mayoi Elieza, Hamisi Samade na Yussuf Muhuta, walimweleza mkuu wa wilaya kuwa kumekuwa na shida katika upatikanaji wa ajira za mradi wa SGR, akitolea mfano kituo cha usaili kimewekwa mkoani Tabora na kuwapo viashiria vya rushwa.

Kufuatia malalamiko hayo, Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Mwagisa, aliwaahidi wananchi hao kulifuatilia suala hilo kwa kuumulika utaratibu uliotumika kutoa ajira katika mradi wa ujenzi wa reli hiyo.

Alisema mradi wa SGR unatarajia kutoa nafasi za ajira takriban 500 kwa wananchi wa Wilaya ya Manyoni na kwamba ajira hizo zitatolewa kwa awamu.

Mwagisa alisema amekuwa akipokea ujumbe mwingi wenye malalamiko kutoka kwa wananchi juu ya namna ajira hizo zinavyotolewa na kusababisha wengi wao kukosa imani na mchakato mzima wa utolewaji wa ajira za mradi huo.

Alibainisha kuwa utaratibu wa ajira katika mradi huo unaelekeza wananchi katika maeneo yanayopitiwa na mradi kupewa kipaumbele lakini amekuwa akipokea malalamiko kuwa wanaoajiriwa ni wageni kutoka nje ya maeneo mradi ukakopita.

Mkuu wa Wilaya alisema kutokana na hali hiyo, atakutana na uongozi wa Kampuni ya Yapi Markez inayotekeleza mradi wa SGR ili kuzungumzia suala hilo.

"Nitakutana na Waturuki, nifanye nao mkutano, ninadhani kuanzia wiki ijayo ili tubaini tatizo lilipo, kama ni wao au kuna watu wanatumika tutashughilika nao," aliahidi.

Katika hatua nyingine, kiongozi huyo wa wilaya alipiga marufuku kuuzwa maeneo malisho ya mifugo yaliyotengwa kwa ajili ya wafugaji.

Mwagisa alisema kumekuwa na utaratibu wa watu kuuza maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho ya mifugo katika maeneo mbalimbali wilayani hapa, jambo ambalo ni kosa kisheria na kwamba ofisi yake ilishakemea na kulitolea mwongozo.

Aliongeza kuwa suala hilo likifumbiwa macho, litasababisha mgogoro mkubwa wa ardhi miongoni mwa jamii kama ilivyo katika maeneo mengine nchini.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas (kulia), akimkabidhi rasmi Kamishna Mwandamizi wa TAWA Kanda ya Kusini Mashariki, Abrah Juuru, hati ya umiliki wa hifadhi ya Mbambabay yenye ukubwa wa hekari 597 ikijumuisha visiwa viwili, milima na sehemu ya maji ya Ziwa Nyasa katika hafla iliyofanyika Mbambabay wilayani Nyasa. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

# NICOL yapata faida bil. 3.8/-

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya Uwekezaji ya NICOL imepata faida ya Sh. bilioni 3.8 baada ya kodi na kutangaza gawio la Sh. 20 kwa kila hisa litakalotolewa mwezi ujao.

Gawio hilo lilipitishwa mwishoni mwa wiki na mkutano mkuu wa nane wa mwaka wa wanahisa uliofanyika kwa njia ya video kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Arusha.

Akizungumza baada ya mkutano huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NICOL, Erasto Ngamilaga, alisema mkutano mkuu ambao umefanyika ni takwa la kisheria kwa kampuni kama hizo kufanya na wanahisa wake wote.

Alisema kwenye mkutano huo walihudhuria wanahisa wa mikoa ya Mwanza, Mbeya, Arusha na Dar es Salaam ambapo wale wa mikoani walifuatilia mkutano huo kupitia mtandao.

Alisema kwenye mkutano huo wamepata fursa ya kuwaeleza wanahisa namna kampuni ilivyowekeza kwenye miradi mbalimbali na ilivyopata faida ya Sh. bilioni 3.8 baada ya kodi.

Alisema wanahisa wamepitisha gawio la Sh. 20 kwa kila hisa ambayo itaanza kulipwa Desemba 15 mwaka huu.

"Wanahisa wamefurahi sana kuona kampuni inafanya vizuri na sisi viongozi tumewaahidi kuweka mikakati mizuri zaidi kuhakikisha kampuni inazidi kusonga mbele na kupata faida kubwa zaidi siku za usoni," alisema Ngamilaga.

Mwenyekiti wa Bodi ya NICOL, Dk. Gideon Kaunda alisema kampuni hiyo imekuwa ikitoa gawio kila mwaka na aliipongeza bodi mpya kwa kuwekeza sehemu mbalimbali hasa kwenye hati fungani za serikali.

Alisema kampuni hiyo imewekeza asilimia 30 ya uwekezaji wake kwenye hati fungani na ndiyo sababu kampuni hiyo imeendelea kupata faida mwaka hadi mwaka na kuwapa gawio zuri wanahisa wake.

Alisema wanahisa wa NICOL nchi nzima wanafikia 30,000 na wamekuwa wakiandaa mbinu za kuwafikia kushiriki mikutano wakiwa kwenye maeneo wanakoishi badala ya kulazimika kwenda Dar es Salaam kwenye mkutano mkuu wa mwaka.

"NICOL inapenda kuona wanahisa wake wanapata gawio kila mwaka na kweli kampuni imefanya vizuri na gawio limeongezeka kwa kiwango ambacho kampuni zingine zimeshindwa kufikia na tunadhani mwakani tutazidi kuongeza gawio kubwa zaidi kwa wanahisa wetu," alisema.

Mwanahisa Muttamwega Mugaywa alipongeza kampuni ya NICOL kwa utendaji mzuri na kuonyesha matumaini makubwa kwa wanahisa wake.

"Ni furaha kubwa kuona NICOL inabeba uchumi na ninawashauri watu wengine waje wanunue hisa zao mapema NICOL kwa sababu kuna faida nyingi kuwa mwanahisa wa kampuni ya wazalendo.

"Ninawapongeza viongozi kwa kusimamia vizuri kampuni na sasa tunapata gawio zuri, ninawashauri wengine nao wachangamkie hisa za kampuni yetu," alisema Muttamwega.

Mwanahisa mwingine, Suzana Masele alimpongeza Mwenyekiti wa Bodi ya kampuni hiyo, Dk. Gieon Kaunda kwa namna anavyoisimamia kampuni hiyo na menejimenti nzima.

# Ruvuma kuzalisha tani 37,500 za parachichi

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKOA wa Ruvuma unatarajia kuzalisha tani 37,500 za parachichi ifikapo mwaka 2025 kutokana na mikakati madhubuti iliyowekwa.

Mkuu wa Mkoa huo, Kanali Laban Thomas, akizungumza na waandishi wa habari juzi, alisema lengo ni kuongeza uzalishaji wa zao hilo kama yalivyo mazao mengine ya biashara na kuwawezesha wananchi kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla.

Alisema kwa sasa uzalishaji ni hekta 2,446 zinazozalisha tani 1,769 na kwamba lengo kufikia zaidi tani 37,500 ifikapo 2025, mwaka ambao ni ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999-2025.

"Tija ya uzalishaji kwa eneo kwa sasa ipo chini ambapo uzalishaji kwa eneo la hekta moja ni tani 0.7228, miongoni mwa mikakati inayotekelezwa ili kuongeza uzalishaji wa zao la parachichi ni kuwezesha kuwaunganisha wakulima kupitia vikundi vya wakulima," alisema.

Mikakati mingine ni kuwapatia wakulima mbegu za parachichi, kuwafundisha namna ya kuanzisha kitalu cha miche ya parachichi, kuwafundisha namna ya kubadi (grafting), kuandaa shamba, kupanda na kuhudumia miche ya parachichi.

Ofisa Kilimo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Onesmo Ngao, alisema msimu wa mwaka 2021/22 wakulima walihamasishwa kulima zao la parachichi ambalo sasa lina soko kubwa ndani ya nje ya nchi hasa katika nchi ya China ambayo ina mahitaji makubwa ya zao hilo.

Akizungumza mjini Songea hivi karibuni, Balozi wa China nchini, Chen Mingjian alitoa rai kwa wakulima mkoani hapo kuongeza uzalishaji wa soya na parachichi kwa kuwa yana soko kubwa China.

Uzalishaji wa parachichi mkoani Ruvuma unafanyika katika wilaya za Songea, Mbinga na Nyasa.



# TAKUKURU yahoji watumishi H'shauri Handeni tuhuma kuuza ardhi ya serikali

**Na Hamida Kamchalla,**
HANDENI

WATU wanne wakiwamo watumishi watatu wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, wanahojiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kutokana na tuhuma za kuuza ekari 500 za ardhi ya serikali na kuruhusu uvunaji wa mbao 1,000 katika eneo hilo.

Amri ya kukamatwa na kuanza kuhojiwa, ilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa huo, Omari Mgumba, alipokuwa akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Kwamsisi, Wilaya ya Handeni.

"Kwa kukaa kwangu hapa muda mfupi tu, nimebaini kwamba viongozi wenu wametumia vibaya madaraka yao na kuuza ardhi ya serikali.

Kwa nyakati tofauti wameuza maeneo ya umma. Hili halikubaliki na nitaanza kushughulika nao leo (jana).

"Sasa TAKUKURU, kamata hawa viongozi wa vijiji na watendaji na hao wananchi 27 waliotajwa hapa, wakidai ardhi hiyo ni yao. Watafuteni wote peleka ndani, kama kuna serikali mlikuwa mnaijaribu kuitania sio hii ya sasa chini ya Rais Samia Suluhu Hassan."

Waliokamatwa ni Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kwamsisi (VEO), Erick Chipindula, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kwedikabu, Rajabu Makamba, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kwedikabu (VEO), Zahara Sempule na Ofisa Misitu wa Wilaya ya Handeni, Elinihaki Mdee.

Baada ya kuwaweka chini ya ulinzi watendaji hao na Mwenyekiti wa Kijiji cha Kwedikabu, Mkuu huyo wa mkoa, alihoji kwa nini watu hao wasiwajibike kisheria, kwa kuwa walikuwa na nia ovu ya kujipatia fedha za umma isivyo halali.

"Kuna rushwa hapa inaonekana inaendelea, haiwezekani kukawa kuna watu wanachukua mali za umma kwa maslahi yao binafsi, halafu tunakaa tunabembelezana. Tunataka mkajieleze ili tuone hatua za kuchukua zaidi ya hii ya kuwakamata."

Kutokana na tuhuma hizo za uuzaji wa ardhi ya umma, Mgumba alisisitiza kuwa kama kuna ardhi yoyote imeporwa kwa njia haramu ya kutengeneza, itarudi kwenye kijiji husika.



Mmoja wa wanahisa wa Kampuni ya Uwekezaji (NICOL), akizungumza wakati wa mkutano wa mwaka wa kampuni hiyo uliofanyika kwenye ukumbi wa Julius Nyerere mwishoni mwa wiki **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Kesi kupewa ujauzito mwanafunzi kidato cha 4 uchunguzi haujakamilika

**Na Jaliwason Jasson,**
SIMANJIRO

MAHAKAMA ya Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, imeelezwa kuwa uchunguzi wa tuhuma za kumpa ujauzito mwanafunzi wa kidato cha nne, zinazomkabili mchimbaji mdogo wa madini ya tanzanite, Erick Peter (39), bado haujakamilika.

Akizungumza jana mahakamani humo, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Mosses Hamilton, alidai kuwa kutokana na kesi hiyo kuwa na maslahi ya umma, uchunguzi wake bado unaendelea na hivyo, wanaomba tarehe nyingine ya kutajwa shauri hilo.

Kesi hiyo namba 102 ya mwaka 2022, inasikilizwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Charles Uisso.

"Mheshimiwa Hakimu, uchunguzi wa shauri hili lililoko mbele yako bado haujakamilika. Tunaomba mahakama yako tukufu, ipange tarehe nyingine ya kutajwa kwa shauri hili," alidai Hamilton.

Katika hati ya mashtaka, inadaiwa kuwa katika tarehe isiyotajwa mwezi Mei mwaka huu, mshtakiwa alitenda kosa la kumpa mimba mwanafunzi wa sekondari.

Kosa la kumpa ujauzito mwanafunzi ni kinyume na kifungu cha 130 (1) na (2), na kifungu 131 cha Kanuni ya Adhabu, Sura 16 cha Sheria Mwenendo wa Makosa ya Jinai ilivyofanyiwa Marejeo Mwaka 2002; ikisomwa pamoja na Sheria ya Elimu, kifungu 60 (A) (2) na (3) iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Baada ya upande wa mashtaka kuwasilisha ombi hilo, Hakimu Uisso, aliahirisha shauri hilo hadi Novemba 22, mwaka huu, itakapotajwa tena mahakamani.

# Walimu wanaojigeuza wanaharakati kuchukuliwa hatua

**Na Cynthia Mwilolezi,**
SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera, amesema serikali haitasita kuchukua hatua dhidi ya walimu watoro na wanaoshindwa kuwajibika katika taaluma yao kutokana na kujigeuza wanaharakati, wakati tayari serikali imeshalipa madai yao mbalimbali, ikiwamo fedha za kujikimu, likizo, matibabu na posho nyinginezo.

Dk. Serera alitangaza vita hiyo jana, dhidi ya walimu wa aina hiyo, alipokwenda kuongoza harambee ya uchangiaji wa mradi wa ujenzi wa ofisi za utawala za Chama cha Walimu Tanzania (CWT), zinazojengwa katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani humo.

"Walimu wameshalipwa madai yao mengi, kwa hiyo serikali imetimiza wajibu wake ipasavyo. Basi na ninyi timizeni wajibu wenu ili kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika wilaya yetu ya Simanjiro," alisema.

Katika harambee hiyo, Mkuu huyo wa wilaya, alifanikisha kupatikana kwa zaidi ya Sh. milioni 26, ambazo zilichangwa na wafanyabiashara mbalimbali, wakiwamo wa madini, wachimbaji wadogo, wananchi wa kawaida na walimu.


Kabla ya hafla hiyo, Katibu wa CWT wa Wilaya ya Simanjiro, Nazama Tarimo, alimshukuru Dk. Serera, kwa kukubali kuongoza harambee hiyo, akisema ushiriki wake unaashiria mwamko mzuri wa viongozi wa umma, kuunga mkono shughuli zinazofanywa na watumishi wake.

"Tunajenga ofisi za chama, kwa ajili ya kutetea na kuboresha maslahi ya walimu. Kwa tafsiri halisi ni kwamba hii ofisi itawasaidia walimu kufanya kazi kwenye mazingira bora zaidi. Katika Wilaya ya Simanjiro, kuna walimu 929 wakiwamo Maofisa Elimu Kata 18, Maofisa elimu ya msingi na sekondari 10, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wawili, Wadhibiti Ubora wa shule watatu, walimu wa sekondari 277 na walimu wa msingi 617.

Katika harambee hiyo, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Simanjiro, Kiria Laizer, alisema walimu ni kada muhimu katika jamii kwa kuwa ndio wanatengeneza wataalamu, na ni vyema wakaungwa mkono.

"Kutokana na hali hiyo, mimi binafsi nawachangia shilingi milioni moja ili mjenge ofisi yenu. Mnasaidia sana kuwapa elimu wananchi, hasa jamii yetu ya kifugaji ya Kimasai, ambayo inaishi hapa kwa asilimia 90," alisema Laizer.

Naye Diwani wa Mirerani, Salome Mnyawi, alisema wataendelea kumuunga mkono Mkuu huyo wa wilaya na yeye binafsi anachangia Sh. 400,000.





# Polisi yahadharisha viashiria kundi ‘watoto wa ibilisi’

**Na Hamida Kamchalla,**
TANGA

JESHI la Polisi limesema kuwa kundi la kihalifu lililokuwa likitikisa katika viunga mbalimbali vya Halmashauri ya Jiji la Tanga, maarufu kama ‘watoto wa ibilisi’ bado linaviashiria vya kuwapo licha ya kudhibitiwa.

Kundi hilo la vijana wadogo wanaotembea wakiwa zaidi ya 10, hupita kwenye mitaa mbalimbali kuanzia saa 12 jioni na kuzusha hofu huku likitishia usalama wa wananchi na mali zao katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi, Henry Mwaibambe, licha ya jitihada kubwa zinazofanyika hivi sasa kuhakikisha kundi hilo halifanyi uhalifu, bado watoto hao wa ibilisi wako mafichoni na hawajaisha mitaani, hivyo ni wajibu wa wakazi wa Jiji hilo kulisaidia jeshi hilo kuwafichua.

“Tupeni ushirikiano ili tuendelee kutokomeza uhalifu katika mji huu. Mkoa umefanya kazi nzuri ya kuwadhibiti hawa watoto wa ibilisi, lakini hawajakwisha wote, wengine wapo na baadhi yao wanatumia usafiri wa pikipiki, yaani hizi bodaboda kufanya uhalifu na wanapora watu wakiwa kwenye usafiri huo.

“Mtoto amekamatwa kwa uhalifu, ana bodaboda haina hata namba ya usajili, halafu anakuja mzazi wake ofisini analalamika akitaka mwanawe aachiwe kwamba hana makosa, anaonewa. Hapo hapo, anakwambia uchungu wa mwana anajua mzazi.”

Inaelezwa kuwa, kundi hilo la watoto wa ibilisi, huvamia makazi ya watu na kupora mali, huku wakiwa na silaha za jadi ikiwamo panga, shoka, bisibisi, nyundo na visu.

Kutokana na mkakati huo inaokuja nao wa kulifuta mitaani kundi hilo, Kamanda Mwaibambe, alisema bila kuweka mikakati na kuachana na roho ya huruma, itakuwa vigumu kuwadhibiti watoto hao kutokana na baadhi ya wazazi kuwakingia kifua.

Mpaka sasa Jeshi la Polisi, mkoani Tanga, limenasa pikipiki 20 ambazo nyingine hazina namba za usajili na magari mawili yaliyotumika kwenye matukio ya kihalifu. Pia limekamata simu, camera za video, bangi na pombe haramu ya gongo katika kipindi cha wiki tatu.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Henry Mwaibambe, akionesha bunduki feki iliyokamatwa na jeshi hilo juzi katika msako maalumu wa wiki tatu mkoani humo, pia vitu mbalimbali vilikamatwa ikiwamo silaha, simu za mkononi, televisheni, magari mawili, dawa za kulevya aina ya bangi pamoja na pombe haramu aina ya gongo. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA.**

## Wanaoharibu vyanzo vya maji kuondolewa kwa nguvu

**Na Oscar Assenga,** MUHEZA

SERIKALI imesema itawaondoa kwa nguvu wananchi wanaoendelea kuvamia na kuharibu vyanzo vya maji kwa kuanzisha machimbo ya madini katika Tarafa ya Amani, Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga.

Mkuu wa wilaya hiyo, Halima Bulembo, aliyasema hayo jana alipotembelea chanzo cha maji cha Mto Zigi, wilayani humo pamoja na kuzindua mradi wa majaribio wa utunzaji wa vyanzo vya maji katika Kijiji cha Kwemwewe, Kata ya Mbomole.

“Hatutawavumilia kwa hilo na ninawaonya wanaovamia vyanzo vya maji ili kutafuta madini, muache mara moja na muondoke bila kusubiri kuondolewa kwa nguvu.

“Kumekuwa na tabia ya wananchi kuvamia maeneo ya vyanzo vya maji na kufanya shughuli za kiuchumi ikiwamo uchimbaji wa madini, jambo ambalo linasababisha uharibifu kwenye vyanzo hivyo ikiwamo uchafuzi.”

Alisema kutokana na uwepo wa athari hizo kubwa kwa jamii watahakikisha wanakula sahani moja na wahusika ili iweze kuwa fundisho kwa wengine ambao wamekuwa na tabia kama hizo.

Awali, akitoa taarifa kuhusu eneo hilo, Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Mazingira ya Asili ya Amani, Fikiri Maiba, alisema katika eneo hilo kuna chanzo cha maji cha Mto Zigi, ambacho kinalisha Wilaya za Tanga, Muheza na Mkinga.

Alisema katika vyanzo hivyo, kuna uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji kutokana na uchimbaji na utafutaji wa dhahabu, hivyo jamii inapofuata madini na kujitokeza uharibifu huo wanasababisha janga kwa taifa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Tanga-UWASA, Dk. Ally Fungo, alisema kutokana na uharibifu wa vyanzo vya maji, wamekuwa wakitumia zaidi ya Shilingi bilioni moja kutibu maji kutokana na uchafuzi unaofanyika.

# H’shauri yaanza mpango kudhibiti magonjwa yasiyopewa kipaumbele

**Na Allan Isack,** ARUMERU

HALMASHAURI ya Arusha, imeanza kutekeleza mpango mkakati jumuishi wa taifa wa kupambana na kudhibiti magonjwa yasiyopewa kipaumbele, kwa watoto wenye umri wa miaka mitano hadi 14, ambao wameandikishwa shuleni na wasio kwenye mfumo rasmi wa elimu.

Jana Katibu Tawala wa Wilaya ya Arumeru, James Mchembe, alisema serikali itahakikisha mpango huo wa kitaifa, unatekeleza shughuli hiyo kwa ufasaha ili kufikia malengo ya kuwakinga watoto, ambao wako kwenye hatari ya kuambukizwa magonjwa ya minyoo tumbo.

Kutokana na mkakati huo, Mchembe, aliagiza timu ya wataalamu iliyochaguliwa kutekeleza mpango huo kuhakikisha inafanya kazi kwa bidii na kwa kushirikiana ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na serikali.

“Wataalamu wa dawa kinga, ni vyema mkajikita kutoa elimu ya usafi kwa wananchi, kwa ajili ya kujikinga na minyoo kwa kuwa na vyoo bora. Lakini nawasihi wananchi muwe na tabia za kupima afya na kunawa mikono kwa majisafi na sabuni kabla ya kula, kabla ya kunyonyesha mtoto, wakati wa kumtawaza baada ya kutoka chooni na kuvaa viatu.”

Aidha, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha, Ojung’u Salekwa, akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa mpango huo, aliishukuru serikali kutokana manufaa kwa watoto, wananchi na jamii kwa ujumla.

“Naipongeza serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuleta mpango huu wa kuandaa watoto wenye afya bora, ambao ndio wajenzi wa taifa la kesho na asiyeshambuliwa na magonjwa afya ya akili kwa kuwa itamwezesha kuitumikia nchi yake,” alisema Mwenyekiti Ojung’u.

Kwa upande wake, Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya na Ustawi wa Halmashauri ya Arusha, Dk. Peter Mboya, alisema halmashauri hiyo, inatarajia kutoa kinga tiba ya minyoo tumbo kwa watoto 80,000 wenye umri kuanzia miaka mitano mpaka 14.

Alisema mpango huo, umekusudia kuendeleza mpango jumuishi wa taifa wa kudhibiti magonjwa yasiyopewa kipaumbele ukiwa na dira ya kuwa na wananchi wenye afya bora na ustawi usiodhoofisha.

Naye Mratibu wa Magonjwa Yasiyoambukiza wa Halmashauri ya Arusha, Ramadhani Kulewa, alisema halmashauri hiyo inategemea kutoa kinga tiba ya ugonjwa wa minyoo tumbo kupitia vituo 211, vituo vya afya 56 na kwenye shule za msingi 155, huku wahudumu 433 wakiwamo walimu 310 na wahudumu wa afya 112.

Nipashe
TESA
Jumanne Novemba 15, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 19

## COP 27 kufanyika Misri hakuna tija kama waharibifu hawatatoa fedha kuinusuru Afrika



Ukurasa 17

## Msisimko wasichana mashujaa wafugaji walipovunja mwiko



Ukurasa 16

Utajiri uliojificha ndani ya haki miliki: Huanzia kuzisajili, zitambulike, zilindwe

SAYANSI

**NA SABATO KASIKA**

AJALI YA NDEGE BUKOBA

# Fahamu asili, kazi kisanduku cheusi kumbe si cheusi, tena hakiungui

MARA ndege inapopata ajali kama ilivyotokea Bukoba hivi karibuni, kimbilio ni kisanduku cheusi ambacho kina taarifa za mwenendo wa safari zote za ndege hadi siku ilipoanguka.

Kisanduku cheusi au black box watu wengi hawakifahamu ni kama siri ya wahandisi wabunifu wa ndege waliyoiweka ili kupata taarifa iwapo itapata matatizo.

Ajali iliyotokea mkoani Kagera, ndege ya Precision Air, alianguka ndani ya Ziwa Victoria na kuua watu 19, uchanguzi wake umeanza na kisanduku cheusi kikitarajiwa kujibu maswali ya chanzo.

Mhandisi wa ndege mstaafu, Gideon Mgusi, anazungumza na Nipashe kuelezea maana ya black box na jinsi inavyofanya kazi ya kubainisha chanzo cha misukosuko inayoiangusha ndege.

Anasema ni kifaa ndani ya ndege kinachonasa na kutunza taarifa mbalimbali za mwenendo wa ndege wakati wote inapokuwa angani na kwamba kina kitu au 'memory card au hard disc' ya kompyuta inayorekodi kila kitu, kuanzia siku ilipoanza kupaa.



Gedeon Mgusi (kulia) akitengeneza ndege. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

"Kwa kawaida katika ndege kubwa kama Airbus na Boeing kuna vifaa viwili vya kunasa taarifa. Hivi ndivyo kwa ujumla wake huitwa black box. Cha kwanza kinanasa sauti na kelele zote ndani ya chumba cha marubani," anasema Mhandishi Mgusi.

Kina uwezo wa kutunza sauti miaka yote hata saa mbili baada ya ajali na kwamba mazungumzo yote kati ya marubani wenyewe, na minara ya kuongozea ndege (control towers) au rubani na abiria wake anasema.

"Kifupi, sauti au kelele zozote ndani ya chumba cha marubani hunaswa na kutunzwa. Hata ukivuta nyuma kiti mikwaruzo hunaswa. Kuna kinasa sauti ndani ya chumba hicho kikiitwa Cockpit Voice Recorder (CVR) japo kisanduku hicho hakiko ndani ya chumba hicho," anasema.

Kifaa kingine huitwa Flight Data Recorder (FDR) ambacho hunasa na kutunza taarifa za aina nyingi na mbalimbali na kwamba ndicho chenye 'memory card au hard disc' zinazorekodi mambo mengine mengi mno.

Mfano, kasi ya ndege angani, kulinganisha na hewa ilipo ndege, mwendokasi, muda unaotumika, uwezo wa injini inapofanya kazi, kiasi cha joto, mwelekeo wa inapokwenda.

Anaongeza kuwa: "Kwa kifupi, FDR ni kama mpelelezi wa kila kinachofanyika ndani ya ndege. Kulingana na aina zake, ina uwezo wa kuhifadhi data kulingana na muda kuanzia saa tano, 10 hadi 25 tangu ilipozimwa na kurudi nyuma."

**HISTORIA BLACK BOX**

Mugusi anasema kifaa hicho kilianzishwa miaka 69 iliyopita nchini Australia na kwamba kwa kipindi cha miaka miwili kati ya 1952 na 1954, ndege ya kwanza aina ya Jet ikiitwa Comet ilipata ajali na kuua takriban abiria 110.

"Idara ya Usafiri wa Anga ya Australia ilikutana na ndipo mtaalamu Dk. David Warren, akapendekeza kuwekwa chombo cha kurekodi sauti. Hiki kilikuwa kama kinasa sauti 'tape recorder' iliyowekwa ndani ya chumba cha rubani," anasema.

Anaongeza kuwa tangu wakati huo, kifaa hicho kimefanyiwa marekebisho na maboresho mengi hadi kuwa na uwezo mkubwa na weledi katika zama hizi.

"Tunaposema kifaa hiki au black box tunaaminisha vyote viwili, yaani CVR na FDR. Wakati mwingine vinakuwa ndani ya mkusanyiko mmoja ingawa vinafanya kazi tofauti na vinawekwa maeneo tofauti pia," anasema.

INAENDELEA UK.18

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI

### TISHIO JIPYA VVU WASICHANA

# UN -WOMEN, AIDS waja na majukwaa kupaza sauti, kuwaelimisha, kuwakinga




Viongozi wa kimataifa na kitaifa pamoja vijana wakishiriki mkutano wa kujadili namna ya kumkomboa msichana na VVU na UKIMWI. **PICHA: JULETE MKIRERI**

ZIPO jamii zinazoendekea kusimamia na kutetea mila na desturi zinazomkwamisha binti au mtoto wa kike katika maeneo mbalimbali, kuanzia kupata elimu, kufanyakazi hata kufikia umri wa kuolewa na kuchagua mwenza anayempenda.

Moja ya haki ambazo ananyimwa ni ya kusoma ambayo ni iko kikatiba, lakini kipaumbele zaidi kinatolewa kwa mtoto wa kiume huku kauli mbiu ya mila za baadhi ya makabila ikieleza kwamba mtoto wa kike majukumu yake ni ya nyumbani na akikua ni kuolewa na kuzaa watoto.

Hata kwenye kujifungua kinamama wanashangilia zaidi ujio wa mwanaume wakipiga vigelegele mara nyingi zaidi kuliko akizaliwa msichana. Lakini familia zikichinja kondoo kusherehekea tofauti na akizaliwa binti wanachinja mtetea, unyanyasaji huanza kwenye uzazi.

Imani kuwa kazi yao ni kuzaa watoto husababisha baadhi kuozwa udogoni na hata wanapopata mimba hakuna anayeripoti polisi wala mahakamani kudai haki. Mazingira hayo yanasababisha msichana na wanawake kupata athari mbaya zikiwamo hata kuambukizwa maradhi mfano VVU na UKIMWI, kupoteza maisha kwenye uzazi, kuzidi kudidimia kwenye dimbwi la umaskini.

Oktoba 11 kila mwaka inafanyika siku ya mtoto wa kike, wasaa

> Tunahitaji kuwa na mijadala ya kitaifa ambayo tutahakikisha watoto wa kike wanashiriki kusikiliza na kupaza sauti zao kila mahali ili kuondokana na hatari za maambukizi ya VVU.

unatoa fursa kwa mashirika na taasisi zinazopingana na mila kandamizi kufanya makongamano na mikutano ya kujadili namna ya kumkomboa mtoto huyu.

Maadhimisho ya mwaka huu, yameshuhudia Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UN WOMEN) likifanya mkutano mkubwa jijini Dar es Salaam, uliozikutanisha nchi 14 kupigania vipaumbele vya msichana.

Nipashe inashiriki mkutano huo ambao mawaziri na viongozi vijana kutoka nchi hizo akiwamo mwenyeji Tanzania ni pamoja na Kenya, Zambia, Rwanda, Lesotho, Zimbabwe na Namibia wanajadili namna ya kumkomboa msichana na mwanamke kutoka hatari ya kupata VVU na UKIMWI.

Elimu inatajwa kuwa ni njia muhimu inayomkinga kwani endapo atakuwa amesoma atapata ujuzi utakaomweka salama kutumia maarifa, ujuzi na rasilimali kubuni miradi mbalimbali ya maendeleo ya kiuchumi.

Ili kufikia azma hiyo zinahitajika jitihada za kuielimisha jamii kuweka kipaumbele cha elimu kwenye familia lakini kumwezesha mwanamke kiuchumi ili kumwondoa katika hatari ya kupata maambikizo.

Mwanamke akipata maambukizo anakumbana na ubaguzi kutoka kwenye familia yake na jamii inayomzunguka hususani kwenye maeneo ya huduma.

Akizungumza katika mkutano huo Mkurugenzi wa UN Women, Sima Bahours, anaeleza kuwa inahitajika sauti zaidi ya kuwasemea watoto wa kike kuhusiana na vikwazo vinavyosababisha kuingia katika maambukizi ya magonjwa hayo.

Sima anakumbusha kuwa mabadiliko ya mitazamo pia yanahitajika katika kuibua sauti za wanawake na pia ili zipatikane hususani kupitia majukwaa mbalimbali kuanzia ya kijamii na hata kisiasa.

"Tunahitaji kuwa na mijadala ya kitaifa ambayo tutahakikisha watoto wa kike wanashiriki kusikiliza na kupaza sauti zao kila mahali ili kuondokana na hatari za maambukizi ya VVU," anasema Sima.

Aidha, jambo la kuwatetea watoto linapaswa kusaidia kupunguza vitendo vya kikatili kwa kundi hili pamoja na wanawake.

"Tunapaswa kukomesha masuala ya ukatili wa kingono tupaze sauti zetu kila mahali kwa kuwashirikisha pia vijana wa kiume, UN Women inaamini kila hatua ya maendelea ni pamoja na kutatua matatizo ya kijinsia," anasema.

#### YANAYOHITAJIKA

Sima anabainisha kuwa ili kufanikisha mpango mkakati wa mapambano hayo yanahitajika mambo manne ambayo ni pamoja na kufafanua mambo yanayowakabili wasichana vikwazo vinavyowakabili pamoja na kuwekeza kwenye taasisi za watoto wa kike pamoja na haki zao.

Mkurugenzi huyo anasema jambo jingine ni pamoja na kubadili mila na kuwezesha wanawake kuwa viongozi na kushiriki katika majukwaa mbalimbali yanayoandaliwa.

"Tunapaswa kuinua sauti zao na kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI kwa maisha ya sasa na ya baadaye," anasema Sima.

Ananukuu ripoti ya UN inayoeleza kuwa kila baada ya dakika mbili wasichana kadhaa wanaambukizwa VVU wakiwa katika harakati ya kupata mahitaji na haki zao.

Mkurugenzi wa UN-WOMEN, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoonyesha mapambano ya kuwainua wanawake.

Mkurugenzi Mtendaji wa UNAIDS, Winnie Byanyima, katika mkutano huo, anasema jamii inapaswa kukomesha ukatili wa kingono kwa kuwashirikisha vijana wa kiume kwenye mijadala ya kupambana na unyanyasaji.

Winnie pia anasema elimu ni moja ya njia ya kumkomboa mtoto wa kike kupata uambukizo wa VVU na UKIMWI akiwa na umri mdogo lakini hali duni za maisha inaelezwa kuwa chanzo cha wanawake na wasichana kuambukizwa.

Mmoja wa viongozi vijana wasichana Rahma Jumanne, anaeleza katika mkutano huo kuwa wasichana na wanawake wanapitia mateso na wako kwenye hatari ya kupata maambukizo na kila aina ya ubaguzi wa kijinsia kutoka kwenye jamii inayowazunguka.

Anasema huu ni wakati muafaka kwa mtoto wa kike kuwa mstari wa mbele kupigania haki zake na kuonyesha uwezo wao, karama na talanta walizojaliwa kwa umoja na nguvu moja.

"Kwa umoja wetu viongozi vijana tunatoa wito kwa wasichana na wanawake sehemu mbalimbali duniani kupaza sauti zetu kupambania haki zetu. Tunaishauri serikali, taasisi za kimataifa na mashirika ya watu binafsi kushirikiana nasi kama wabia na wadau katika kuondoa vikwazo na kutengeneza mipango endelevu na madhubuti katika kuwekeza kuwezesha wanawake kupata elimu bora na maarifa kwa vitendo," anasema.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, anasema Tanzania itaendelea kushirikiana na majukwaa ya Uganda na Malawi kupeana uzoefu, kufikia Ajenda ya Afrika ya kulinda watoto na kuwa na viwango sawa vya malezi na makuzi ya watoto wa kike barani hapa.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

KUOZA WALIOMALIZA LA 7

# Sungusungu na jukumu maalumu zisitokee ndoa ili waingie sekondari

TATIZO la ndoa za utotoni mkoani Shinyanga, limeendelea kupingwa na wadau mbalimbali na ili kuhakikisha linakwisha na wanafunzi wanaomaliza darasa la saba, hawaolewi ila wanasoma na kutimiza ndoto zao, Mkuu wa Wilaya Jasinta Mboneko amekuja na agizo jipya.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta, pamoja na kukemea vitendo hivyo vya ndoa ya utotoni analiagiza, jeshi la jadi 'Sungusungu', kufanyakazi kwa juhudi zote ili kutokomeza ndoa za utotoni na zile za mwanafunzi hasa wanaomaliza la saba.

Anaagiza kuwa kusiwe na ndoa ya mwanafunzi yeyote aliyehitimu darasa la saba mwaka huu itakayofungwa kwa kipindi hiki ambacho wengi wapo nyumbani wakisubiri matokeo ya mtihani wao uliomaliza mwezi uliopita.

Akizungumza na Nipashe, Mkuu wa Wilaya anasema wanafunzi wanapokuwa nyumbani kama wakati huu, baadhi ya walezi na wazazi hutumia nafasi hiyo kuwaozesha ndoa za utotoni na matokeo yakitoka ya kujiunga na kidato cha kwanza wanakutwa tayari baadhi yao wameshaolewa na kuhama vijiji.

Anaahidi: "Serikali tutaendelea kuwashughulikia wazazi na walezi ambao wanaendekeza mazoea ya kuozesha watoto wao wadogo, tunataka wasome na kutimiza ndoto zao ili taifa lipate wataalamu wakiwamo madaktari, wahandisi, wanasiasa na viongozi mbalimbali."

Katika kuunga mkono juhudi za kupambana na ndoa hizo, Shirika la WEADO linalotetea haki za wanawake, watoto na wazee la mkoani Shinyanga, limezindua mradi wa vunja ukimya zuia ndoa na mimba za utotoni, ambao utatekelezwa katika kata mbili za Masengwa na Tinde.

Wakishirikiana na Taasisi ya Foundation for Civil Society wanaoudhamini, WEADO inalenga kuhamasisha jamii kuachana na mazoea hayo yaliyopitwa na wakati na kuwaendeleza watoto, kimasomo ni kwa mujibu wa ofisa mradi wa shirika hilo Winnie Hinaya.

Akizungumza na gazeti hili anasema kata hizo mbili za Masengwa na Tinde zitakuwa za mfano wa namna ya kupambana na kutokomeza ndoa na mimba za utotoni mkoani Shinyanga na utadumu ndani ya miezi nane ambao kwa hutua za awali ulianza Septemba na utakwenda hadi Aprili mwaka 2023 kwa gharama ya Shilingi milioni 37.8.

Anasema lengo kuu la mradi huo ni kupunguza kiwango cha ndoa na mimba za utotoni mkoani Shinyanga, ambao unaongoza kitaifa kwa asilimia 59 kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto (UNICEF) mwaka 2012.



Ofisa Miradi wa WEADO, Winnie Hinaya, akizungumzia mradi wa vunja ukimya zuia ndoa na mimba za utotoni ambao watautekeleza Masengwa na Tinde. **PICHA: MARCO MADUHU**

> Matukio ya ukatili kwa watoto wadogo yapo mkoani Shinyanga licha ya kupungua, kwa takwimu za Aprili hadi Juni mwaka huu lakini jumla ya watoto 113 wamefanyiwa ukatili wa kingono.

"Kwenye mradi huu tutakuwa tukitoa elimu kwa wazazi juu ya madhara ya kuozesha watoto ndoa za utotoni, umuhimu wa kuunda mabaraza ya watoto, kutokomeza masuala ya mila na desturi kandamizi, pamoja na kuzingatia malezi bora na makuzi ya watoto," anasema Winnie.

Mkurugenzi wa Shirika la WEADO, Eliasenya Nnko, anasema katika mradi huo furaha yao ni kuona watoto wanakuwa salama na kuondokana na masuala ya ndoa za utotoni.

Anaongeza kuwa ndoa hizo zisipopigiwa kelele mara kwa mara, jamii inajisahau na kuziendeleza na kusababisha kukithiri kwa na hatimaye kuzima ndoto za watoto na wanawake kufanikiwa maishani lakini Tanzania ikiendelea kuwa na kinamama mbumbumbu na wajinga.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Nicodemas Simon, anasema wadau mbalimbali wamekuwa na mchango mkubwa katika mapambano ya kutokomeza ndoa na mimba za utotoni na kuisaidia serikali kukuza elimu hasa ya watoto wa kike.

Anasema serikali pekee haiwezi kupambana na suala hilo la kutokomeza ndoa za utotoni pasipo kushirikiana na wadau wa wengine wakiwamo wa utetezi wa haki za binadamu, maendeleo na usawa wa jinsia ambao wao huwafikia watu wengi zaidi pamoja na maeneo ambayo mkono wa serikali haiwezi kufika.

"Serikali tutaendelea kuwa unga mkono wadau na juhudi zao katika mapambano haya ya kutokomeza ndoa za utotoni ili wanafunzi na watoto wetu wasome na kutimiza ndoto zao," anasema Simon.

Ofisa Maendeleo wa Halmashauri ya Shinyanga, Aisha Omary, anasema serikali inahitaji pia kushikwa mkono na washirika wengine katika mapambano ya kupunguza ndoa za utotoni kwani peke yake isingeweza.

Anasema ndoa za utotoni katika halmashauri hiyo ya wilaya ya Shinyanga kwa sasa zimepungua tofauti na miaka ya nyuma wakati huo kukiwa na hali mbaya zaidi.

"Kwa takwimu za ndoa za utotoni mwaka huu, kuanzia Januari hadi Septemba ndoa zilizoandaliwa ni tatu lakini hazikufanikiwa. Tulizitibua na tukawaokoa wanafunzi kwa kushirikiana na wadau na sasa wanaendelea na masomo yao na hatua za kisheria dhidi ya watuhumiwa zikichukuliwa," anasema Aisha.

Akitoa maoni yake Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Shinyanga Lidya Kwesigabo, anaitaka jamii kuacha tabia ya kuendekeza masuala ya mila na desturi kandamizi na kuozesha watoto ndoa za utotoni mambo yanayowaharibi uelekeo wa maisha yao na kuongeza ujinga na umaskini kwenye maeneo mengi.

Anasema serikali pamoja na wadau wamekuwa wakipaza sauti kupinga ndoa hizo za watoto, lakini baadhi ya jamii bado wamekuwa wagumu kubadilika na kuendelea kuozesha wanafunzi na kukatisha masomo yao kwa tamaa za kupata mifugo, fedha na zawadi nyingine zinazowafikia kupitia mahari.

"Matukio ya ukatili kwa watoto wadogo yapo mkoani Shinyanga licha ya kupungua, kwa takwimu za Aprili hadi Juni mwaka huu lakini jumla ya watoto 113 wamefanyiwa ukatili wa kingono," anasema Lydia.

Nuru Jeremiah kiongozi wa kiroho kutoka Kanisa la AICT Masengwa, Wilaya ya Shinyanga, anaiomba jamii iwe na hofu ya Mungu na kuacha tabia ya kuwafanyia watoto ukatili wa kingono ikiwa ni pamoja na kuwaozesha ndoa za utotoni na kuwakatisha masomo.

Anasema jamii ikiwa na hofu ya Mungu ndoa za utotoni hazitaweza kuendelea kwa sababu ni kumnyima mtoto haki yake ya msingi ya kukua, kusoma na kusimamia maisha yake hapo baadaye kunakosababishwa na kumfanyia ukatili wa kijinsia.

"Sisi viongozi wa dini tunakemea ndoa za utotoni na tutaendelea kupiga kelele kupitia madhabahu zetu ili jamii iache kuozesha watoto wadogo bali waachwe wasome na kutimiza ndoto zao,"anasema.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Utajiri uliojificha ndani ya hakimiliki

- Huanzia kuzisajili, zitambulike, zilindwe
- Faida ukiwa hai, ukifa ulinzi hadi miaka 50



Zephania Lyamuya kutoka Ofisi ya Hakimiliki Taifa, (kushoto), akielimisha wanahabari wa IPP kuhusu sheria za ulinzi wa hakimiliki. **PICHA: THE GUARDIAN LIMITED**

MASUALA ya hakimiliki yanaweza kuwa mageni kwa wengi, lakini wasanii na wabunifu huenda wakawa na ufahamu kwani ndiyo wanaojitahidi kulinda kazi zao.

Waliobakia wanaweza kujiuliza hakimiliki ni nini hasa? Kwa mujibu wa Zephania Lyamuya, Kaimu Mkuu wa Idara ya Sheria Ofisi ya Haki Miliki, anaieleza kuwa ni haki ya kipekee anayokuwa nayo mtunzi wa kazi kuamua matumizi ya kazi yake.

Akielimisha wanahabari wa IPP, hivi karibuni, kuhusu sheria na ukiukwaji wa hakimiliki na athari zake, anasema hakimiliki ni haki pekee ya kisheria ya mtu anayehusika kuchapisha, kusambaza, kucheza au kurekodi kazi ya maandishi, kisanii au kazi za muziki, anayokuwa nayo mtunzi au mbunifu wa jambo hilo yeye peke yake na kuwakataza wengine wasitumie, bila kibali chake.

Anawaambia wanahabari kuwa sheria inalinda waliobuni kazi zao dhidi ya matumizi ya kazi zaona kujipatia faida bila kumzingatia au kumnufaisha mmiliki, akileza kuwa ulinzi wa kazi ni wa muda wote akiwa hai na hata akifa zinalindwa miaka 50 baada ya kifo.

Baadhi ya kazi hizo ni picha anazopiga au kuchora, kuchonga, muziki alioimba, nyimbo, filamu, mavazi, michoro, matangazo ya runinga na ala za muziki.

Anasema zinalindwa ili wapate haki ya kiuchumi au kuingizia kipato. Ni lazima mwenye kazi aruhusu izalishwe, itengenezwe tena iuzwe mfano picha, utafiti, habari, hadithi ichezwe filimu.

Anasema kazi hizo zinarithiwa na warithi wakaendelea kunufaika kimapato. Aidha, anasema sheria hiyo inataja haki za maadili ambazo kazi inapotumika mmiliki unatajwa na kupata heshima, kwa mfano wimbo, filimu, kitabu au picha.

> “Maliasilia zinaitwa ‘folk lore ni mali za jamii fulani, ni lazima kupata ruhusa yao mfano, vazi la Wamasai, sheria inasema mlinzi wa mali za jamii kama ngoma, mavazi na muziki ni Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA).

#### KAZI ZA JUMUIYA

Kwenye jamii kuna vitu kama nyimbo na ngoma asilia za kabila fulani mfano Wanyasa na ngoma ya Mganda, Lyamuya anasema kazi hizo hulindwa na serikali na kuwaonya watu wasijiaminishe kuwa ni mali ya kila mtu anayetaka anatumia afaidike kiuchumi.

“Maliasilia zinaitwa ‘folk lore ni mali za jamii fulani, ni lazima kupata ruhusa yao mfano, vazi la Wamasai, sheria inasema mlinzi wa mali za jamii kama ngoma, mavazi na muziki ni Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA).”

Ulinzi wa mali hizo unakwenda pamoja na kuruhusu matumizi ambayo yananufaisha jamii nzima, mfano Mganda wa Wanyasa ni kabila zima, hakuna anayeumiliki, hivyo, anayetaka kuitumia anaomba BASATA na ili wote wanufaike mtumiaji anatoa huduma kwa wananchi kama kisima cha maji yanayotumiwa na wote.

#### UHARAMIA/WIZI

Akizungumzia wizi wa kazi za kisanii anatoa mfano wa ‘Live band’ kwenye baa ni wizi wa muziki mingine kwa vile zinapigwa, wateja wanalipia, bendi haijasajiliwa inatoa burudani kwa kuimba nyimbo za wengine ambao hawajatoa kibali tena hawapati kitu.

Lyamuya anasema ni kinyume cha sheria na kuwataka watu kufuatilia na kujua sheria ya ulinzi wa hakimiliki.

Anakumbusha umuhimu wa wasanii leo kulinda mawazo yao dhidi ya uharamia kwa mfano, anahimiza kuandikishiana wazo la ubunifu na kukataza lisitumike popote, unapokutana na waendelezaji.

Anawashauri wasanii na wabunifu kutumia wanasheria wakiwa na mawazo yenye tija ili yalindwe kisheria kabla huwajalifikisha kwa watu mbalimbali.

Anasema baadhi ya wezi wa kazi za kisanii unafanywa kwa kujificha, kama kuchukua CD za muziki kuzifytua na kuzalisha nyingine ‘feki’ ambazo husambazwa mitaani kwa siri tena usiku wa manane.

Uharamia mwingine hufanywa hadharani watu wanatumia kompyuta kuchoma CD, kunakili miziki ndani ya flush na kuziuza.

Wapo wanaozinadi flush ina nyimbo 1,000, wamejaza nyimbo ambazo ni kazi za wengine na kuziuza kwa faida, Lyamuya anasema huo ni wizi.

#### SABABU ZA UHARAMIA

Anasema ziko nyingi lakini bei kubwa ya kazi halali za wasanii husababisha kukimbilia kuvunja sheria, lakini hazipatikani za kutosha, pia wamiliki wanakuwa wazito kutoa kazi zao wakiogopa kutapeliwa na wanawapa kusambaza au kuzizalisha tena.

Lyamuya anazungumzia athari za uharamia kuwa ni kusababisha wazalishaji wasipate faida kutokana na ubunifu na juhudi zao. Mfano aliyetunga muziki hapati kitu licha ya kwamba unanunuliwa na kusikika kila kona.

Teknolojia imewezesha kazi hizo pia kufanyiwa mambo ya ujanja na kuondoka kwenye mikono ya wasanii na kubakia maskini.

Athari nyingine ni kuwa na kazi za kisanii hasa muziki na filamu zisizo na viwango na kuchochea mporomoko wa maadili jamii inapozitumia.

#### HATUA KUDHIBITI

Anasema kwanza jamii kuelewa hakimiliki inalindwa kazi asilia ya mtu kama muziki, picha na filamu inatakiwa imnufaishe mzalishaji wa kwanza.

Lakini Lyamuya anawakumbusha watu wasidandie kazi za kisanii au kibunifu waombe kibali kwa mmiliki, wanunue siyo kuiba vitu vya wengine.

“Sheria ipo na inalinda. Watanzania, wasaniii na wanahabari someni ili mjue Sheria ya Hakimiliki ya mwaka 1999 ambayo imefanyiwa pia marekebisho 2022 na kuizingatia”.

“Kuna Mkataba wa Berne wa 1886, Tanzania imeuridhia wa kulinda kazi za watu wengine za nje ili wao nao walinde za Watanzania,” anasema.

Anaongeza kuwa kuna mazingira sheria inaruhusu matumizi ya kazi za watu wengine bila kibali cha mmiliki chini ya utaratibu wa matumizi huru. Katika eneo hilo mhusika anaweza kutumia kazi za wengine kama picha, video na taarifa kwenye vyombo vya habari kwa lengo la kuelimisha na kuhabarisha.

Aidha, anaweza kuzitumia kwenye mihadhara na kufundisha na cha muhimu kwenye mazingira yote ambayo hatumii kazi hizo kujipatia kipato au manufaa kiuchumi.

“Ukishazingatia masharti hayo cha msingi utaje chanzo cha kazi hiyo ni nani? Jarida utaje jina lake na kama ni televisheni, utafiti au kitabu. Utumie kwa kiasi kidogo siyo kunakili kila kitu.” Anasema Lyamuya.

#### ULINZI KISHERIA

Anawaambia wanahabari kuwa ulinzi wa kazi za Watanzania upo na unatajwa kikatiba kama haki ya kumiliki mali.

Aidha, anasema Kifungu cha 42 cha Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki kinapiga marufuku wizi wa kazi za hakimiliki na kinafafanua adhabu na faini zitakazohusika.

Anasema kuna kifungo na faini pia na wakati mwingine kugharamia gharama ya kuharibu kazi, tena sheria ya hakimiliki inataja kuwa kama wakati wa kesi kazi zinahifadhiwa mshtakiwa ataghar-amia, kulipia mzigo ukihifadhiwa au kutozwa faini ya asilimia 30 ya thamani ya mzigo lakini kufungwa hata miaka mitano jela.

Sheria nyingine inayohusika na ulinzi wa haki miliki ni za kuzuia uhalifu mitandao, kuna faini ya Shilingi milioni 20 iwapo mtu atatumia kitu chochote kinachotumia ‘network’ kama kompyuta au simu kuchukua kazi ya mtu mwingine mitandaoni ni kinyume cha sheria.

Anasisitiza kuwa sheria nyingine ni Mkataba wa Berne unaoagiza kulindwa kazi ndani kama nchi inavyolinda zile za nje.

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI

# Msisimko wasichana mashujaa wafugaji walipovunja mwiko

• Ni kutoroka nyumbani, kushtaki wazazi, kufuata masomo kijiji jirani, leo ni kidedea

“KATIKA familia yetu kipaumbele ni ndoa, elimu tumeipa kisogo hata ukifanya juhudi gani ili upelekwe shule hawakusikilizi. Watoto kwa wakubwa na jamii wanataka uchunge mifugo na baadaye wakuoze,” ni maneno ya binti wa miaka 15, Anna Charles.

Ana sio jina halisi, ni mtoto anayekumbusha kisa cha kusikitisha kuwa akiwa na miaka 11 alilazimika kutoroka nyumbani Kijiji cha Ngeta wilayani Kibaha mkoa wa Pwani, baada ya wazazi wake kugoma kumpeleka shule licha ya kuwaomba sana.

Wawili hao wanaosoma Mlandizi wanazungumza na Nipashe wakieleza hali inayowazunguka, wakisema familia tangu udogo wazazi walikataa kuwasomesha ili wachunge mifugo.

Anasema siku zilizidi kwenda na umri wake kuongezeka huku akiwa na hofu ya kuozeshwa kama ilivyozoeleka ndani ya wanakijiji cha Ngeta.

Anakumbusha kuwa jamaa zote waliomzunguka kuanzia wazazi, ndugu wa karibu na jamii ilimweleza kuwa kutokana na umri wake hawezi tena kusoma ila asikilize maamuzi na mipango ya wazazi.

“Sikuwa nakubaliana na namna ambavyo jamii yetu ya Wamang’ati ilivyokuwa inawaozesha katika umri mdogo, niliahidi kukipambania kile ninachokipenda,” anasema.

Anaongeza: “Siku moja nikiwa nachunga nilipoteza ng’ombe kaka yangu alinipiga sana. Nilitafakari nitaendelea kuchunga mifugo hadi lini na kupigwa tatizo linapotokea na umri wangu nilielewa wazi kinachofuata sasa ni ndoa jambo ambalo sikukubaliana nalo.”

#### WAUNGANA KUAMUA

Anna anaeleza kuwa wakati akiwa anatafakari hatua za kuchukua alipata wa kumuunga mkono ambaye ni mtoto wa kaka yake aliyekuwa na miaka 10 wote kwa pamoja walikuwa wakitamani kusoma ingawa familia yao hawakuona umuhimu wa kuwapeleka shule.

“Siku moja tuliamua kutoroka nyumbani kwenda kijiji cha jirani cha Kikongo kuomba msaada kwa viongozi wa serikali kupelekwa shule.”

Anaeleza kuwa waliamua kwenda kwa viongozi wa kijiji chao lakini wakakumbuka kuwa waliwahi kuombwa msaada na mtoto wa kaka yao, aliyetoroka mara mbili nyumbani kwao ili akapate elimu shule za jirani, lakini walichofanya ni kuongea na wazazi wake na kumrejesha kijijini jambo ambalo liliwapa hofu.

Anasema pamoja na mtoto wa kaka yake waliondoka nyumbani hadi Kikongo ambako walitaka kuonana na mtendaji ili awape msaada wa namna ya kuishi huku wakisoma.



Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Kibaha, Yahaya Mbogolume, akizungumza na wananchi (hawapo pichani) kuhusu mila kandamizi. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

> Tulisubiri familia yote wameshaondoka nyumbani saa 6:00 mchana tukaanza kutembea tulijipanga tukikutana na yeyote njiani tunamwambia tutarudi.

“Tulisubiri familia yote wameshaondoka nyumbani saa 6:00 mchana tukaanza kutembea tulijipanga tukikutana na yeyote njiani tunamwambia tutarudi,” anasema.

#### KUPOKELEWE KIJIJINI

Kwa mujibu wa binti huyo walipofika kwa mtendaji hawakumkuta na badala yake waliowakuta waliwaomba kuunganishwa na mtendaji, alipigiwa simu akasema yuko nje ya ofisi ila akaagiza bodaboda iwafikishe mahali alipokuwa.

Anaeleza kuwa walipofika kwa mtendaji aliwaunganisha na Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, ambaye aliwapeleka katika kituo cha kulea watoto wanaotoka mazingira hatarishi.

Anna anasema kwa msaada wa ofisa huyo walianza maisha mapya katika kituo hicho na kuandikishwa katika Shule ya Msingi Mlandizi kuanza masomo kwenye darasa la Mpango wa Elimu kwa Walioukosa (MEMKWA) mwaka 2018.

“Tukiwa shuleni mwanzo tulikumbana na vikwazo kutengwa huku wengine wakisema hawezi kukaa karibu na MEMKWA ilituumiza mwanzoni lakini baada ya kurejea kilichotupeleka shule tuliachana na maneno yao tukasimamia elimu yetu,” anaeleza Anna.

Anasema sasa wapo darasa moja na wanafunzi wengine na maendeleo yao kitaaluma yamemaliza maneno ya kejeli waliyokuwa wakiitwa awali.

#### MAWASILIANO NYUMBANI

Anna anasema wakati wa likizo wamekuwa wakienda kuwasalimia wazazi wao na kutokana na hatua waliyochofanya hawajakumbana na vitisho na hata kwa rafiki zao wamekuwa wakiwaona ni mashujaa na hawafanyiwi unyanyasaji, kwa vile wanahofia kushtakiwa.

#### WAFANYA MAAJABU

Akizungumzia maendeleo ya wanafunzi hao Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mlandizi Alfred Luoga, anasema aliwapokea 2018 mmoja akiwa na umri wa miaka 10 na mwingine 11.

Anasema licha ya kuanzia katika darasa la MEMKWA mmoja katika matokeo ya darasa la nne alipata wastani wa alama A na mwingine B na sasa wanasoma darasa la sita wakiwa na maendeleo mazuri na ya mfano.

Luoga anasema maendeleo yao yanazidi kubadilika kila mara ambapo katika muhula wa kwanza mwaka huu mmoja ameshika nafasi ya kwanza akiwa na wastani wa B na mwingine nafasi ya sita akiwa na wastani wa B kati ya wanafunzi 107.

“Mabinti hawa kwa sasa darasani wanaongoza kitaaluma, nidhamu wako vizuri, ni watiifu na wasikivu lakini kutokana na tabia zao sasa wote ni viranja(viongozi) na hii inaleta faraja kwetu,” anasema Luoga.

Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Yahaya Mbogolume, anasema anajivunia kuwasaidia wasichana hao kukimbia ndoa za utotoni na ataendelea kufuatilia maendeleo yao ili kuleta fundisho kwa wazazi ambao wanapenda kuwaozesha watoto wao na kuwakosesha haki ya elimu na kudumaza maendeleo na maisha yao.

Mbogolume anasema wilayani humo eneo la Magindu na Dutumi ndiko, zinakotokea ndoa nyingi za utotoni ambazo hufanyika kwa siri na anapata taarifa baadaye tena wasichana wakishaozwa na kutoroshwa mbali.

Anasema jamii za wafugaji zinahusika na kikubwa wanachotazamia ni kupata mifugo ambayo ni mahari na ndicho kinachowasukuma kuipa elimu mgongo.

“Mtoto wa kike kwao ni mali wanajua, anapokua anaozeshwa ili wapate ng’ombe hata kama umri wake bado na hili tumejaribu kulifuatilia sana lakini kama unavyojua ndoa zao zinafanyika kwa siri mno,” anaeleza Mbogolume.

Anasema ndoa za utotoni katika halmashauri hiyo zimekuwa zikikumbwa na migogoro mbalimbali ambayo inasababisha baadhi ya wanandoa kuomba kuachana.

Kutokana na hali hiyo anasema kitengo chake wanaendelea kutoa elimu kwa jamii mara kwa mara na kueleza madhara ya ndoa za utotoni.

Mbali ya elimu pia wanahusisha kamati za ulinzi na usalama huku wakisisitiza upande wa wananchi kujiunga na kamati hizi ili kutoa taarifa kwa haraka kudhibiti ndoa hizo kufungwa na kumnusuru mtoto wa kike kuolewa akiwa na umri mdogo.

Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 iliyopingwa mahakamani inaeleza kuwa ni wajibu wa baba kuwatunza kwa kuwapatia elimu matibabu, malazi na mavazi, sheria hiyo pia inatamka kuwa ni kosa la kisheria kumwozesha mtoto wa kike aliye chini ya umri wa miaka 16.

Katika sheria hiyo pia inaeleza kuwa iwapo mtoto wa chini ya miaka 14 ataozeshwa basi ni lazima kuwe na kibali cha mahakama na kwamba mtoto wa miaka 15 anaweza kuozeshwa pale ambapo kuna idhini ya wazazi au walezi.

# Fahamu asili, kazi kisanduku cheusi kumbe si cheusi, tena hakiungui




Ajali ya ndege iliyotokea hivi karibu Bukoba mkoani Kagera. **PICHA:MTANDAO**

**INATOKA UK.13**

### RANGI YA KISANDUKU

Akizungumzia rangi, Mugusi anasema ni ya mng'ao mkali au nyingine ni rangi ya chungwa na siyo nyeusi, na kufafanua kuwa kuna dhana kwamba jina 'black box' linatokana na kutunza taarifa ambazo hazijulikani hadi zipelekwe kusomwa katika maabara na wataalamu maalum.

"Hivyo ni nyeusi kwa vilivyomo ndani hatuvijui ni wachache wanaozitambua Kama vile Afrika liliitwa bara jeusi, siyo kwa sababu watu wake ni weusi, bali kwa kipindi hicho mambo yaliyokuwamo ndani ya Afrika yalikuwa hayajulikani," anasema.

Aidha, anasema mara kifaa hicho kinapopatikana, huwa kimezungukwa na majivu meusi na kwamba sababu za kuitwa black box hata leo ni mjadala.

Anaongeza kuwa tangu kilipotengenezwa kimekuwa na sura za aina nyingi, kuanzia miaka ya 60 hadi 80, FDR zilikuwa kama yai, rangi ya njano au nyekundu na kwamba 'black box' siyo boksi au kasha wala hakuna rangi nyeusi.

> "Cockpit Voice Recorder CVR na Flight Data Recorder FDR hupaswa kuwamo ndani ya ndege kubwa zenye injini za jet kwa ndege za biashara.

### INAPOFUNGWA

Mhandisi Mgusi anasema kifaa hicho hufungwa sehemu ya nyuma ya ndege sehemu ambayo mara nyingi haiguswi ajali inapotokea au kuharibika kirahisi.

"Kifaa hiki kimetengenezwa kwa madini ambayo hayaungui, kwani sifa zake hakitakiwi kuungua kiurahisi hata kama ajali imehusisha moto, ndio maana kinaweza kuhimili joto la nyuzi 2,000°F au sentigrade1,093.3 kwa saa," anasema.

Mtaalamu huyo anaongeza; "vifaa vya black box na vingine vingi vya kutunza taarifa vyote vimefunikwa na aluminum na madini ya silica na kwamba kifaa chote kinazungukwa na chuma cha pua ambacho kina uwezo mkubwa kuhimili joto kali la hadi nyuzito 2,000 F au Sentigredi 1,093. 3 kwa saa. Ni kama joto la tanuri la kuyeyusha chuma.

"Inapata umeme lakini kuna betri yenye uwezo wa kutunza chaji kwa mwezi mmoja na ikiwa majini kama ndege imeangukia ziwani kazi yake ni kutoa ishara ili wachunguzi wapate kujua mahali ilipo hasa ndani ya maji na betri hiyo ndiyo moyo wa black box."

Anabainisha kuwa baada ya kifaa hicho kupatikana, hupelekwa kwenye maabara maalum, ili kusomwa na kutafsiri data zilizomo na hayo hufanyika mbele kampuni iliyotengeneza ndege, wachunguzi wa ajali kutoka nchi ndege iliposajiliwa na wataalamu wengine wa usafiri wa anga duniani.

"Taarifa zitakazopatikana, lengo si kutoa lawama, bali kujifunza chanzo cha ajali husika na kutengeneza taratibu za kuzuia tukio la aina hiyo lisijitokeze tena," anasema Mugusi.

Hata inapolazimika kufungia aina fulani ya ndege, lengo ni kutaka watengenezaji wa ndege au injini wafanye marekebisho ndipo waruhusiwe kuendelea kutoa huduma za usafiri.

"Pamoja na hayo, usafiri wa ndege umeendelea kuwa salama kuliko aina nyingine ya usafiri kutokana na hatua mbalimbali za usalama ambazo huwa zinachukuliwa," anasema.

Anafafanua kuwa, kila tukio au ajali hasa ya ndege, ni fursa ya kuboresha aina hiyo ya usafiri, mifumo na black box ili kuwezesha kupata visababishi vya ajali, ili kuweka mifumo bora ya kuzuia nyingine.

### KUFUNGA BLACK BOX

Mugusi anasema kanuni na Sheria ya Usafiri wa Anga zinaeleza aina ya vifaa au vyombo vinavyopaswa kuwamo ndani ya ndege kulingana na ukubwa wake na matumizi yake.

"Cockpit Voice Recorder CVR na Flight Data Recorder FDR hupaswa kuwamo ndani ya ndege kubwa zenye injini za jet kwa ndege za biashara. Kwa ndege ndogo zenyewe hazihitajiki kuwa na black box," anasema.

Mgusi anasema ndege ndogo zina kifaa kingine kidogo cha kutoa taarifa iwapo imeanguka nchi kavu au majini na kwamba huitwa Emergency Locator Transmitter (ELT).

Anasema ELT ni kifaa cha mawasiliano ambacho ndege ikianguka kinatuma ishara kwenye masafa fulani yaliyopangwa kutumika na kifaa hicho tu na kinasaidia kupata mahali ndege ilipoangukia.

ELT hairekodi wala kutunza taarifa zozote bali huonyesha eneo au mahali kilipo tu, mtaalamu huyu ambaye kwa sasa ni Meneja wa Udhibiti Ubora wa Kampuni ya Ndege ya Sky Dive ya Zanzibar, anasema amefanya kazi maeneo mbalimbali ikiwamo Wizara ya Kilimo na kustaafu serikalini mwaka 2016.

"Mwaka 1981 niliajiriwa Wizara ya Kilimo Anga kama mhandisi wa ndege na nimepitia maeneo mbalimbali hadi nilipostaafu, hivyo nina uzoefu na masuala ya anga," anasema Mugusi.

## WANENAVYO MALENGA

### MEZA KITI VIWE BORA

Mwili wako binadamu, usikae palepale,
Lazima tujifahamu, twende hapa pia pale,
Vinginevyo twala sumu, magonjwa haya na yale,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Kazi zako wafahamu, za kukaa palepale,
Na wewe wajifahamu, maumivu hapa pale,
Ili uweze jikimu, usikae palepale,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Ufanye kazi kwa zamu, pale kwenye meza pale,
Kisha jipatie hamu, uinuke toka pale,
Hebu zunguka kwa zamu, uende hapa na pale,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Kiti chako wafahamu, unachokalia pale,
Ili afyayo idumu, kiwe bora kiti kile,
Kipande shuka kwa zamu, na mgongo uwe vile,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Kompyuta kwako muhimu, mejaa mezani pale,
Usawa wake muhimu, shingo ibakie dole,
Kuwa juu sana sumu, afya itakuwa lele,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Egonomia elimu, ndiyo wapatiwa tele,
Afya zetu ni muhimu, tusifikishane kule,
Miili iwe migumu, tuwe na nyingi kelele,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Kiti kukaa muhimu, kiwe kimeenda shule,
Miguu tunafahamu, kaa iwe chini pale,
Kuning'inia ni sumu, wala usibaki vile,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Vya kukanyagia muhimu, hasa kwa wafupi wale,
Kufika chini vigumu, kikalia viti vile,
Hicho ni kitu muhimu, tusipate shida zile,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Kuzingatia muhimu, egonomia ni shule,
Kudharau kwako sumu, hutakuwa vilevile,
Mwili takuwa mgumu, maumivu yaleyale,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Kulinda afya muhimu, maarifa haya tele,
Sote tuingie zamu, tuzipunguze kelele,
Migongo kuwa migumu, kunywa kunywa dawa zile,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**Simu: +255 767 22360**
**na barua pepe: lwagha@gmail.com**

ELIMU

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

MABADILIKO TABIANCHI

# COP 27 kufanyika Misri hakuna tija kama waharibifu hawatatoa fedha

MKUTANO wa Copenhagen au COP27 wa mazingira, ulipata jina la COP ikiwa ni kifupisho cha Copenhagen mji mkuu wa Denmark. Kwa mara ya kwanza vikao vya kujadili mabadiliko ya tabianchi vilianzia huko.

Kongamano hilo la kujadili changamoto za mabadiliko ya tabianchi linaendelea hata leo na safari hii linafanyika mjini Sharm el-Sheikh, Misri.

Kwa Afrika ni tukio linalofanywa 'nyumbani'. Lakini la kufikiria ni hivi, una mafanikio gani kwa Afrika, bara linaoumizwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi?

Vigogo na mabilionea wanaozalisha hewa chafu duniani, wanapokusanyika Sharm el-Sheikh Misiri, wanajua kwamba Waafrika wamechoka, ni kwa sababu wanateseka kwa kile ambacho hawakukisababisha.

Mataifa yaliyoendelea kama China, Marekani, India, Japan na matajiri wengine duniani wenye uchumi mkubwa, wanazalisha asilimia 97 ya hewa chafu wanaitesa Afrika Tanzania ikiwamo.

Muda mrefu umepita, bara hili liliahidiwa kupata dola bilioni 100 kwa mwaka ili kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa hasa mataifa ya Kusini ya Jangwa Sahara ilipo Tanzania.

Lakini kinachoshangaza ni 'longolongo' mazungumzo na maneno mengi hakuna fedha, viongozi wanaotoa ahadi tena wazalishaji wa hewa zenye athari wanataka kuona Waafrika wanaangamia?

Viongozi wa Afrika walio kwenye mkutano huko Misiri na dunia nzima ifahamu kuwa ni wakati wa kulipa fedha hizo na kutimiza wajibu wao kwa sababu Afrika inateseka sana kutokana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa yanayosababishwa na nchi zilizoendelea.

Ni COP ya Afrika, kwa hivyo suala la fedha lishughulikie shida za Afrika kwa kuweka pesa mezani na kuachana na longo longo wakati watu wanakufa.

### AHADI HEWA

Katika Mkutano wa 15 wa Nchi Wanachama (COP15) wa UNFCCC huko Copenhagen mwaka 2009, mataifa yaliyoendelea yalijitolea kufikia lengo la pamoja la kukusanya dola bilioni 100 kwa mwaka ifikapo 2020 kwa ajili ya nchi maskini kusaidiwa kupambana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa kwenye kupunguza uharibifu unaoletwa ongezeko la joto duniani.



Baadhi ya viongozi wa Afrika (mstari wa mbele kutoka kushoto) Rais wa Ghana, Nana Akufo-Addo, Rais wa Senegal na Mkuu wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Macky Sall, Waziri Mkuu wa Uholanzi, Mark Rutte na Rais wa Kongo, Felix Tshisekedi katika mkutano wa mabadiliko ya tabianchi Misri. **PICHA: AFP**

Huko Copenhagen, mataifa hayo yalikubaliana kujitolea kwa lengo la kuhamasisha dola bilioni 100 kwa mwaka ifikapo 2020 kushughulikia mahitaji ya nchi zinazoendelea lakini hadi leo ni ahadi hewa, hivyo COP inapokuja Afrika ni lazima viongozi waje na fedha siyo maneno matupu tena.

Ukweli ni kwamba, kwanza, Afrika inachangia asilimia tatu pekee ya uzalishaji wa gesi chafu duniani lakini inakabiliwa na athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi. Kwa mfano nchi kama Cabo Verde ni ndogo sana Afrika, katika miaka mitano iliyopita, mvua zimekuwa chache mno.

Mabadiliko ya hali ya hewa yanatishia maisha ya zaidi ya watu milioni 100 katika umaskini uliokithiri hasa kwa wakazi wa Kusini ya Jangwa Sahara ni taarifa za ripoti za COP.

Ongezeko la joto duniani linatarajiwa kuyeyusha barafu iliyosalia barani Afrika kwa mafano katika Mlima Kilimanjaro kwa miongo michache ijayo.

Yamesababisha kupungua kwa maji ambayo ni muhimu kwa binadamu, uzalishaji shambani na mifugo yote yameleta ukosefu wa usalama wa chakula, umaskini na watu kuhama kutafuta chakula na sehemu bora ya kuishi na si kukimbia vita tena.

Mauritania kwa mfano kuna maeneo mengi makubwa yameachwa au kukimbiwa kwa sababu yamekuwa jangwa.

Ukiangalia Pembe ya Afrika Ethiopia, Djibout na Somalia hakuna mvua na kila wakati ni ukame, njaa kwa binadamu na vifo vya mifugo. Hata Afrika Mashariki migogoro kati ya wakulima na wafugaji; kuanzia Kenya, Tanzania hadi Uganda ni mambo yasiyoacha kutokea hata raia kuuliwa na mifugo kuporwa. Mabonde kama la Ziwa Chad yamekauka na kote na sasa hakutakuwa na wakulima wala wafugaji .

Kwa mujibu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ripoti za 2022 , Afrika inapoteza kati ya dola bilioni 7 na bilioni 15 kwa mwaka kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Na kama mambo hayatabadilika, inaonya kuwa kutakuwa hitaji la dola bilioni 50 kwa mwaka ifikapo 2030. Ni wazi kuwa Afrika haina uwezo wa kupata fedha zinazohitaji kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Ifikapo mwaka 2030 Afrika itahitaji kati ya dola trilioni 1.3 hadi 1.6 hizo pesa zinatoka wapi?

### AFRIKA INAKOMESHWA

Afrika inakomeshwa kwa sababu inalazimishwa kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi ambayo haikuizalisha . Lakini je, inakabilianaje na kile ambacho haikukisababisha?

Inakomolewa kwani hakuna msaada unaonekana kuendesha miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa ambayo yamesababishwa na wengine.

Hewa ya carbon dioxide inasafirishwa na upepo inasambaa dunia nzima lakini inapanda angani na kujaza anga ikiharibu utanda wa ozone (ozone layer) ambayo sasa imetoboka na kuruhusu miale mikali ya juu kuichoma dunia na kubakia ardhini na kuendelea kuongeza joto angani, ardhini na baharini Afrika ikiteseka zaidi kwa sababu haina fedha wala teknoloji.

> Kwa mujibu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ripoti za 2022 , Afrika inapoteza kati ya dola bilioni 7 na bilioni 15 kwa mwaka kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

### COP IWE NA TIJA

Wakati Waafrika wanaposhiriki kwenye COP27 ndani ya bara lao lazima kuwe na kutoa fedha za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa kwa kiwango kikubwa. Kituo cha Kimataifa cha Afrika cha Kukabiliana na Mabadiliko hayo lazima kipate fedha na kiwekeze kupunguza matatizo ya hali ya hewa.

AfDB inasema zinahitajika dola bilioni 25 kwa Afrika ni lazima mkutano wa Sharm el-Sheikh, usiishie kwenye maneno ukusanyaji fedha uonekane na zitumike kukabiliana na hali hiyo mbaya barani Afrika na kazi ionekane ikifanyika ili kunusuru mamilioni ya Waafrika wasio na hatia.

Mathalani, AfDB ina mfuko unaoitwa Mfuko wa Maendeleo ya Afrika (ADF), ambao unasaidia nchi za kipato cha chini na zinazotumia mfuko ADF.

Nchi tisa kati ya 10 duniani zilizo katika hatari kubwa ya kukabiliwa na mabadiliko ya hali ya hewa ziko Kusini mwa Jangwa la Sahara, kwa asilimia 100 kati yao wanatoka nchi za ADF wanahitaji dola bilioni 60 kwa mwaka kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi lakini zinapatikana dola bilioni18 kwa mwaka bado 42.

### PESA ZINAHITAJIKA ILI

Pesa zinazohitajika ni kwa ajili ya kusaidia wakulima kupata teknolojia zinazostahimili hali mbaya ya hewa kwenye kilimo. Nyingine kwa ajili ya kuwapa bima kukabiliana na hasara ya kilimo inayoletwa na hali ya hewa kama vile ukame au mafuriko.

Nyingine zisaidie kujenga skimu za umwagiliaji kuchimba na kupata vyanzo vipya vya maji, pia kukarabati hekta mamilioni za ardhi iliyoharibiwa na mabadiliko ya tabianchi.

Inahitaji fedha kuwapa mamilioni ya Waafrika maji ya kunywa hasa wale wanaoishi kwenye maeneo makame ambayo milioni 18 hawana huduma hiyo.

Lakini mambo hayaishii hapo wanatakiwa pia serikali za Afrika kupata fedha za kujenga miundombinu ya kutunza mabilioni ya mita za ujazo za maji kuhifadhi maji na kuongeza uwezo wa kuwa na akiba kukabili ukame.

Mambo ni mengi lakini COP kuwa nyumbani hakutakuwa na maana kama hakuna fedha na Afrika ikiwamo Tanzania itaachwa kubaki kama ilivyo.

# HABARI PICHANI



Ofisa Tawala Wilaya ya Magu akiwa na washiriki wa semina ya uendeshaji nyumba za matumaini baada ya kuzindua nyumba ya Kitongo maalum kwa watoto wenye ulemavu wa kichwa kikubwa na mgongo wazi. Semina hiyo imeshirikisha wadau wa Child Help kutoka mataifa mbalimbali ikiwamo Uganda, Kenya, Zambia, Zimbabwe, Zanzibar na Ubelgiji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Ofisa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Magonjwa Yaliokuwa Hayapewi Kipaumbele (NTDPC) kutoka Wizara ya Afya, Clara Jones, akizungumza katika warsha ya waandishi wa habari Dar es Salaam jana, kuhusu ugawaji wa kinga tiba kudhibiti matende na mabusha katika wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akizungumza katika mkutano wa uzinduzi wa Chama cha Wajane Mkoa wa Dar es Salaam juzi na kuwahakikishia wajane kuwa serikali itashirikiana na chama hicho ili kulinda maslahi yao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## CHEMSHABONGO NA -00 21 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. papasa kidogo
5. chukuliwa mgongoni
8. hali ya kuwa sawasawa
10.kamilifu 11. Uo
12.hali ya kuongea kwa gadhabu
13.mtu anayebagua watu wasiofuata misingi yake ya dini
15.Kaka yake Mama
16.malizika kwa kitu 19.kielekezi
20.kiitikio cha shikamoo
23.hekima 24.karatasi ngumu
25.kilevi cha sukari na mchele


Chini:
1. kibubutu
2. kinyume cha mchana
3. mbolea 4. mwanzo
6. elimu ya uuzaji na ununuzi wa bidhaa 7. jambo la kushangaza lisilo la kawaida 9. sadikisha
14.dalili ya jambo fulani
17.taarifa 18.mzazi wa kiume
19.mji mkuu wa zamani Romania
21.rejea 22.msimu wa mavuno wakati wa kipupwe




## Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

KAMISHENI
BALAKI
KOMESHA
BAMAKO
AMALI
AMINA
LALAMISHA
MILANGO
ALASIRI
KINASA
BANDIA
NAAM
UTAMU
SHAIRI

ASI
IRA
KAA
SAA
AHA
UMA
URU
UANGA
ATIA
USO




Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| K | E | N | Y | A | | A | G | U | A |
| A | | A | | | | D | | | D |
| K | A | M | A | T | W | A | | | A |
| A | M | B | I | A | | B | | M | |
| | B | A | B | A | | U | M | B | A |
| H | A | R | I | R | I | | | A | |
| A | | I | K | A | M | A | | O | A |
| M | | | A | B | A | D | I | | S |
| A | D | A | | U | R | A | T | H | I |
| K | | G | | | A | M | A | A | |
| I | J | A | P | O | | U | | I | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| D | A | M | U | | | M | | L |
| H | | T | H | A | M | A | N | I |
| A | G | U | A | | | M | | B |
| N | | M | B | A | B | A | N | E |
| A | N | W | A | N | I | | | R |
| | | A | | G | A | I | D | I |
| M | | | | U | | D | U | A |
| K | U | J | I | K | W | A | A | |
| U | | U | | I | | D | | |
| U | T | A | K | A | T | I | F | U |





## Chuo chawapatia wanafunzi mbinu ya ujasiriamali

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

CHUO cha Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Tawi la Mbeya, kimewapatia wanafunzi wake mbinu mbalimbali za kukabiliana na tatizo la ajira nchini kwa kuwafundisha elimu ya ujasirimali.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Chuo cha TIA, Prof. William Amos, alipofungua mkutano uliohusisha wanafunzi, taasisi za kifedha na wajasiriamali waliofanikiwa.

Alisema mpango huo ni moja ya mikakati ya kukabiliana na tatizo la ajira nchini na TIA itaendelea kuwa wabunifu kuanzia programu zitakazowasaidia vijana na wajasiriamali kuanzisha shughuli za kuwasaidia kujikwamua kiuchumi.

"Wasomi ni wengi kwa sasa, lakini ajira ni chache, wanafunzi wanapoazna elimu ya vyuo vikuu matarajio yao makubwa ni kupata nafasi za ajira serikalini jambo ambalo halipaswi kukaa kwenye vichwa vyetu," alisema.

Prof. William alisema kutokana na hali hiyo, chuo kimeona ni vyema elimu ya ujasiriamali iwe ajenda ya chuo hicho ili kutoa fursa kwa vijana ya kujiajiri na kupunguza tatizo la ajira nchini.

Rais wa Serikali ya Wanafunzi TIA, Dauson Gervas, alisema elimu ya ujasiriamali waliyoipata itasaidia kukabiliana na tatizo la ajira nchini kwa kuwa tayari wamefundishwa mbinu za kuanzisha biashara.

"Elimu hii imekuja wakati muafaka kwa sababu baadhi yetu tunakaribia kuhitimu hivyo itakuwa chachu na mkombozi katika suala zima la kujiajiri tunaporejea mtaani," alisema.

Mkurugenzi wa Kampuni ya uchoraji na ubunifu ya Allyrich, Richard Mulungu, alisema katika ulimwengu wa ukuaji wa teknolojia vijana wanapaswa kujifunza ubunifu na kuanzisha vitu vitakavyowavutia wateja.

**"Wasomi ni wengi kwa sasa, lakini ajira ni chache, wanafunzi wanapoazna elimu ya vyuo vikuu matarajio yao makubwa ni kupata nafasi za ajira serikalini jambo ambalo halipaswi kukaa kwenye vichwa vyetu," alisema.**

# Bomoa bomoa yadaiwa kuathiri nyumba za wajane

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

BOMOA bomoa, inayoendelea jijini hapo imedaiwa kuathiri idadi kubwa ya nyumba za familia za wajane na kusababisha kukosa hifadhi baada ya serikali kutoa siku tatu kuondoka.

Novemba 7, mwaka huu, bomoa bomoa hiyo ilianza katika mitaa ya Iganzo, Kata ya Isanga na kusababisha taharuki kwa wananchi wanaodaiwa kuvamia hifadhi ya mita 22.5 ya barabara kutoka Mbeya kwenda Wilaya ya Chunya na kujenga makazi.

Wakati serikali ikieleza miundombinu ya hifadhi ya barabara kuvamiwa na baadhi ya wananchi wanaosema walianza kuishi tangu mwaka 1981 na ujenzi wa barabara uliwakuta, Tulimbumi Kajange ambaye ni mjane alisema kuwa alifika Mtaa wa Iganzo mwaka 1981 alijenga makazi na kupata familia ya watoto saba kukiwa hakuna miundombinu ya barabara.


"Watu wamekuja nyumbani kwangu kubomoa nyumba sababu wanadai niko kwenye hifadhi ya barabara, yaani kwa miaka yote niliyoishi hapa tangu nikiwa binti hadi sasa nimezeeka ndio niondolewe wakati hapa hakukuwa na barabara yoyote ya lami kwa kweli nimeumizwa sana maana sina pa kwenda nina kundi kubwa la watoto wanaonitegemea," alisema Kajange.

Diana Samson alisema, bomoa bomoa imewaingiza katika umaskini kwa kuwa mwaka jana walitakiwa kubomoa mita 15 na walitii, lakini sasa wameambiwa wabomoe tena mita 7.2 maeneo ambayo wamewekeza miradi ya vibanda vya biashara na makazi.

Mjumbe wa nyumba kumi mtaa wa Iganzo, Agen Mwakigonde, aliiomba serikali kulinusuru kundi kubwa la wazee ambao wengi wao ni wajane kwa kuwa wao ndio waathirika kutokana na kumiliki maeneo mengi. Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD), Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Masige Matari, alisema bomoa bomoa imewagusa wananchi waliojenga makazi ndani ya mita 22.5 katika hifadhi ya barabara ambayo iko kisheria.

"Ikumbukwe kuwa mwaka 2014 maeneo yote ya barabara yalipimwa na kuwekwa gharama za kuwataka kubomoa na kabla ya kuanza tuliwatangazia lakini walikaidi hadi tulipoanza zoezi la kubomoa," alisema Mhandisi Matari.

Alisema, kutokana na kilio cha wananchi aliongeza muda wa wiki mbili kwa walio ndani ya mita 22.5 ya hifadhi ya barabara kubomoa nyumba zao kwa hiari kabla ya kazi hiyo kuendelea.



Meneja Ufundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (MBEYA UWSSA), Mhandisi Benard Konga, akitoa maelezo kwa madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya namna mtambo wa uzalishaji mali unavyofanya kazi kwenye chanzo cha Nzovwe juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mahakama yaanza kusikiliza kesi ya kunajisiwa mtoto

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MAHAKAMA ya Hakimu Wilaya ya Mbeya, imeanza kusikiliza kesi ya jinai inayomkabili mchimbaji wa madini, Boaz Mwambepo (32), mkazi wa Soweto anayetuhumiwa kumnajisi mtoto wa kike mwenye umri wa miaka mitano.

Ilianza ushahidi wa Jamhuri kwa kumsikiliza mwathirika wa shauri hilo ambalo linaendeshwa na Wakili wa Serikali, Davice Msanga.

Mbele ya mahakama hiyo, mtoto huyo (jina limehifadhiwa) alidai mahakamani kuwa Oktoba 13, 2022, majira ya saa 10 usiku, mshtakiwa ambaye ni jirani aliyekuwa akimwita mjomba kwa muda mrefu, aliingia ndani ya chumba anacholala kisha kuzima taa na kuwasha taa ya simu na kumwingilia kimaumbile.

Akisimulia zaidi mtoto huyo alidai mtuhumiwa alimwambia asipige kelele akimtishia kumuua ndipo alipoanza kumbaka hali iliyomsababishia maumivu na michubuko sehemu zake za siri kisha kuondoka kupitia dirishani.

Baba mzazi wa mtoto huyo alidai muda mfupi baadaye walisikia mtoto wao akilia ndipo walipoenda kufungua mlango wa chumba chake na kukuta akilalamika akisema anajisikia maumivu ndipo walipomchunguza na kubaini ameingiliwa.

Baba huyo alidai bila kujua alimpigia simu jirani yake ambaye ndiye mshtakiwa ili amsaidie gari kumpeleka hospitali mwanawe.

Alidai kuwa mshtakiwa aliampa ufunguo wa gari lake ili ampeleke mtoto hospitali na kurudi nyumbani kwake, lakini mbele ya mahakama na kwenye gwaride la utambulisho mtoto alimtambua kuwa ndiye aliyemfanyia kitendo hicho.

Alidai kuwa kwa mujibu wa uchunguzi wa hospitali mtoto wao aliingiliwa na kusababishiwa maumivu makali na michubuko sehemu zake za siri.

Baada ya ushahidi huo Mwendesha Mashtaka wa Serikali wakili Davice Msanga, aliiomba mahakama kuahirisha kesi hiyo hadi tarehe nyingine.

Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Mbeya anayesikiliza shauri hilo, Paul Rupia, aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 15, mwaka huu na shauri litakuja kwa ajili ya Jamhuri kuendelea kutoa ushahidi wake huku mshtakiwa akiwa nje kwa dhamana.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, mshtakiwa anadaiwa kutenda tukio hilo Oktoba 13, 2022 kwa kuvunja dirisha katika chumba anacholala mtoto wa rafiki yake ambako analaza gari lake na kumtendea jinai hiyo kisha kuondoka na nguo ya ndani na suruali ambazo mtoto huyo alivaa.





# Matokeo utafiti zaidi 100 kujadiliwa na wataalamu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MATOKEO ya utafiti zaidi ya 100 uliofanywa kwenye nyanja mbalimbali za kibiashara yatawasilishwa na kujadiliwa na wataalamu wabobezi kwenye kongamano la tatu la maendeleo ya biashara na uchumi.

Kongamano hilo limeandaliwa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), litafanyika kwa siku mbili jijini hapo na kufunguliwa leo na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Emanuel Mjema, aliyasema hayo jana jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kongamano hilo na mahafali ya 57 ya kampasi za CBE.

Alisema kongamano hilo litahudhuriwa na viongozi mbalimbali wa bara na visiwani na mada ndogo zitakazowasilishwa ni biashara ya ndani na kimataifa, uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni.

Pia alisema mada zingine ubunifu na ujasiriamali, uwezeshaji wa biashara na ushirikiano wa kiuchumi, uwekezaji wa teknolojia, uchumi wa buluu na zuio mnyororo na fedha za kidigitali.

"Lengo la mdahalo huu wa kitaaluma ni kujenga uwezo na mitandao miongoni mwa watafiti na wadau wengine barani Afrika na kutoa fursa ya kuleta maendeleo ya kiuchumi kupitia biashara, pia zipo faida binafsi nyingi," alisema.

Kuhusu mahafali, alisema takribani wahitimu 2,000 watatunukiwa vyeti vyao kwa ngazi mbalimbali.

"Kabla ya mahafali kutakuwa na wiki ya makongamano ya kitaaluma, maonesho ya idara za kitaaluma ambayo yatahusisha wahitimu wa zamani wa CBE, pia kutakuwa na semina mbalimbali," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Kampasi ya CBE Dodoma, Dk. Kembo Bwandi, alisema chimbuko la utafiti uliofanywa ni kuunga mkono jitahada za serikali kuhamia Dodoma ili kuibua fursa zilizoko na matokeo yake yalionesha fursa za ardhi, elimu na afya.



Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, akiangalia maendeleo ya masomo kwenye daftari la mmoja wa wanafunzi anayesoma Shule ya Sekondari ya Miyuji Dodoma alipotembelea shuleni hapo juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**



## Wamtafuta binti mwenye tatizo la akili aliyetoweka

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

FAMILIA ya Shaban Cheni ya Chinangali West jijini hapo inamtafuta binti yao Mariam Cheni (29) pichani juu mwenye tatizo la akili baada ya kutoweka nyumbani kwao Jumamosi iliyopita katika mazingira ya kutatanisha.

Baba wa binti huyo, Shaban Cheni, akizungumza na Nipashe jana, alisema licha ya mtoto wao kuwa na tatizo la akili hana tabia ya kutoka nyumbani na kutafutwa kama ilivyo sasa.

"Hana tabia ya kuondoka ondoka na kisha kutafutwa, tumejitahidi kumtafuta maeneo mbalimbali vikiwamo vituo vya polisi vya jirani, hospitalini na kwa ndugu, lakini hakuna taarifa zozote za kuonekana kwake," alisema Cheni.

Cheni alisema ametoa taarifa kituo cha polisi na kuandikiwa namba DOM/CH/1024/2022 huku akiwaomba watu wenye taarifa zozote za kumuona binti huyo wawasiliane kwa simu namba 0652 002430 (Cheni) au 0657 858287 (Mwajuma Hellen) ama kituo chochote cha polisi.

# Sababu kushamiri ukatili kwa watoto yatajwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Ustawi wa Jamii Mkoa wa Dodoma, Josephine Mwaipopo, amesema moja ya sababu iliyochangia vitendo vya ukatili kwa watoto kushamiri ni wazazi na walezi kutotimiza wajibu wao wa kutoa malezi bora.

Pia utafutaji wa maisha kwa wazazi na walezi hao imetajwa kuwa ni sehemu kubwa ambayo inachangia watoto kukosa uangalizi wa karibu na kujikuta wakifanyiwa ukatili.

Mwaipopo, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na walimu, walezi na wamiliki wa shule binafsi za awali kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, katika tamasha lililoandaliwa na walimu wa shule binafsi jijini hapo.

Ofisa huyo alisema kuwa hizo ni sababu chache zinazosababisha watoto nchini kufanyiwa ukatili wa hali ya juu.

Alisema, wazazi na walezi wengi wamekuwa sababu kuu ya watoto kufanyiwa ukatili huo kutokana na ubize wa kutafuta maisha na wengine kutokuwa na ukaribu na watoto wao ili kuwapatia elimu ya malezi na makuzi.

Pia alitaja sababu nyingine ya ukatili huo kwa watoto ni mitandao ya simu ambazo wanaachiwa na wazazi kuangalia picha mbalimbali zikiwamo za ngono.

"Watoto wa siku hizi wanaachiwa simu za mikononi na wazazi na walezi humo kwenye simu hizo wanakutana na picha chafu zikiwamo za ngono suala ambalo ni hatari kwa kizazi cha sasa," alisema.

Alizipongeza shule za awali na binafsi kwa kuisaidia serikali kuwalea watoto na kuwafanya kuwa na maadili ya kiroho na kimwili.

"Serikali lazima ziwapongeze shule hizi za awali za binafsi kutokana na mchango mkubwa wa malezi ya watoto na tumeshuhudia sisi wenyewe shule hizi zikishika nafasi hata kwenye matokeo ya mitihani kwa kufanya vizuri," alisema.

Kwa upande wake, Katibu wa shule za awali za binafsi Mkoa wa Dodoma, Rehema Andrew, alisema tamasha lililoandaliwa na walimu hao limelenga kuwapa fursa ya kujifunza malezi na makuzi ya watoto.

Alisema hiyo ni pamoja kuwalea na kuwafundisha vyema na kuwalinda watoto dhidi ya maadui na vitendo viovu hatarishi kwa maendeleo ya watoto.

"Sisi kama walimu wa shule binafsi tutaendelea kutoa mchango madhubuti katika kuhamasisha jamii kuelimisha watoto wetu katika mazingira yasiyokinzana na utamaduni, mila na desturi za Kitanzania," alisema.



# HABARI ZANZIBAR

## Serikali yaagiza shehia kupatiwa huduma ya maji haraka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Shabaani Ali Othman, ameuagiza uongozi wa wizara hiyo kufikisha huduma ya majisafi na salama haraka katika Shehia ya Kizimbani Jimbo la Bububu, Wilaya Maghari 'B' Unguja ili kuwaondolea tatizo la ukosefu wa maji wananchi wa eneo hilo.

Akizungumza juzi na wakazi wa eneo hilo, alisema haiwezekani wananchi wakose maji kwa muda wa miezi minne na kuutaka uongozi wa wizara yake shehia hiyo inafungiwa mashine ya kusukumia maji katika kisima cha rasilihema ili wapate huduma hiyo.

Alisema ikiwa changamoto kubwa ya maji katika eneo hilo inatokana na mashine ya kusukumia maji kuungua hivyo wizara yake inajukumu la kufunga mashine nyingine ili wananchi wapate huduma hiyo muhimu.

Alisema Serikali ya Zanzibar kupitia wizara hiyo inatekeleza miradi mikubwa ya maji ili kuwandolea wananchi tatizo la majisafi na salama ikiwa ni ahadi ya Rais Dk. Mwinyi na muda mfupi miradi hiyo itakamilika.

"Haiwezikani miundombinu ya maji ipite eneo hili wananchi wa Kizimbani wasipate maji, nimekuja na Katibu Mkuu na watendaji wa mamlaka ya maji (ZAWA) ili wasikie malalamiko yenu na kuyafanyia kazi, hivyo mashine za maji zikifika tu Katibu Mkuu nakuagiza kisima cha rasilihema kifungwe mashine ya maji," alisema Othman.

Aidha, alisema ZAWA inajukumu la kurudisha miundombinu ya maji kwa wananchi ambayo imekatwa wakati wa ulazaji wa mabomba ya maji ikiwa ni utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji Zanzibar.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Joseph Kilangi, alisema wizara inategemea kupokea mashine za kusukumia maji mwishoni mwa Desemba, mwaka huu na kuwahakikishia wakazi wa eneo hilo kufungiwa mashine katika kisima chao ili wapate huduma hiyo.

Hatua hiyo ya uongozi wa wizara hiyo kufika eneo hilo inatokana na malalamiko ya wakazi wa Shehia ya Kizimbani kwa kukosa majisafi na salama katika eneo hilo kwa kipindi cha muda mrefu.

# Mkutano mabalozi 49 wanaowakilisha nchi waanza

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUTANO wa kwanza wa mabalozi wa nchi 49 wanaoiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali, umefunguliwa jana visiwani hapa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mkutano huo ambao pia umewashirikisha wakuu wa idara na vitendo vya Wizara ya Mambo ya Nje ukiwa na kaulimbiu 'Mwelekeo mpya katika kuimarisha diplomasia ya uchumi' ambayo inaakisi na kuchagiza mwamko mpya katika utekelezaji wa sera ya mambo ya nje inayolenga kuinufaisha Tanzania kiuchumi na kijamii katika mazingira ya kiushindani kimataifa.

Akizungumza kwa niaba yake wakati akifungua mkutano huo, Naibu Waziri, Balozi Mbarouk Nassor, alisema jumuiya ya kimataifa imegubikwa na ushindani katika matumizi ya rasilimali na maliasili chache zilizopo duniani katika harakati za kujileta maendeleo na ustawi.

Alisema ni vyema kujipanga na kufanya tathmini ya mara kwa mara ya mwelekeo wa sera kuhusu uhusiano wa kimataifa kwa lengo la kuendelea kulinda na kutetea maslahi mapana ya taifa.

"Wizara hii imepewa dhamana ya kusimamia uhusiano na ushirikiano baina ya Tanzania na nchi zingine, jumuiya za kikanda na kimataifa hivyo tunao wajibu wa kutoa ushauri kwa waliotupa dhamana hii kuhusu yale yote tunayoyaona nje ya mipaka yetu, yawe ni mabaya au mazuri," alisema.

"Katika hili nipende kusisitiza kuwa kila wakati tujenge utamaduni wa kutathmini kwa kina mwenendo wa kidunia tukibainisha fursa na changamoto zilizoko ili ushauri tunaoutoa uwawezeshe wadau wetu kufanya maamuzi sahihi".

Naibu waziri huyo, alisema endapo watabaini soko ambalo linaweza kupokea bidhaa ambazo Tanzania inazalisha kwa wingi na kwa ushindani ni vyema kuorodhesha vigezo vya soko hilo kwa ufasaha na kufikisha taarifa kwa wafanyabiashara au wazalishaji wa bidhaa hizo kwa wakati.

Aliwataka kutoishia kutoa taarifa bali wafuatilie katika hatua zote mnyororo wa manunuzi hadi kufanikisha bidhaa husika katika soko hilo na kuhakikisha uendelevu katika soko hilo.

Aidha, aliwataka mabalozi hao kuondokana na dhana ya kuwa wao ni wabeba taarifa na badala yake kuwa wasimamizi wa masuala yote ambayo yapo ndani ya dhamana zao na kufanya kazi kwa pamoja na ushirikiano.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Balozi Josepho Sokoine, alisema matarajio ya mkutano huo mabalozi hao wataibua hoja na mapendekezo yenye maslahi mapana ya nchi.

Alisema kupitia mkutano huo watabadilishana mawazo ambayo yatasaidia kuboresha mchango wa wizara katika kufanikisha azma ya Rais Samia kukuza uchumi na maendeleo ya nchi.

Pia alisema watabadili mtazamo wa baadhi ya mambo huku wakipata hamasa ya kuongeza bidii na juhudi kwa lengo la kulinufaisha zaidi taifa na kuwa na mwelekeo mpya.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Fatma Rajab, alisema mkutano huo ni nyenzo muhimu katika kuimarisha diplomasia ya uchumi na sera ya mambo ya nje na utatoa funzo kwa mabalozi kujadiliana na kubadilishana uzoefu na kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zilizoko.

"Kaulimbiu ya mkutano huo ni mwelekeo mpya katika kuimarisha diplomasia ya uchumi ambapo inalenga kuwezesha kupitia mapitio ya tulipotoka, tulipo sasa na tunapoelekea kwa msingi huo mkutano huu utaibua masuala mbalimbali yatakayojadiliwa ili kuchangia utekelezaji wa diplomasia ya uchumi kwa maslahi ya taifa," alisema.

Katika mkutano huo mada mbalimbali zitajadiliwa ikiwamo utendaji wa kazi za mabalozi hao katika balozi zao, mwenendo wa dunia na taathira yake katika diplomasia ya uchumi, nafasi ya itelijensia katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi, fursa na mikakati ya kuiwezesha Tanzania kunufaika na eneo huru la biashara, utaratibu wa mikopo ya faragha kwa ajili ya uendeshaji wa vitega uchumi na ununuzi wa majengo na vitendea kazi ubalozini, fursa za kiuchumi Zanzibar katika maeneo ya uchumi wa buluu na nafasi ya chuo cha diplomasia katika kuendeleza diplomasia ya Tanzania.



Mabalozi wa Tanzania wanaowakilishi nje ya nchi wakiwa katika mkutano wa mabalozi wa kujadili masuala ya diplomasia na uchumi uliofanyika Hoteli Verde Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Chuo cha Utalii mkombozi wa ajira Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANAFUNZI wa Chuo cha Utalii (Zenj Centre of Excellence for Tourism) Michamvi, Mkoa wa Kusini Unguja, wamesema kuwa kuanzishwa kwa chuo hicho ni mkombozi wa kupata ajira katika sekta ya utalii na ajira nyingi katika hoteli za kitalii visiwani humo zinashikiliwa na wageni.

Wakizungumza na waandishi wa habari kwenye chuo hicho, wanafunzi hao walisema ajira nyingi katika hoteli za kitalii zimechukuliwa na wageni kwa sababu wazawa hawana taaluma ya kutoa huduma mbalimbali katika hoteli hizo.

Iddi Haji Duni, miongoni mwa mwanfunzi wa chuo hicho, mkaazi wa Bwejuu Mkoani humo, alisema matarajio yake baada ya kumaliza masomo kuwa mpishi mkubwa duniani ambaye atatoa huduma za chakula katika hoteli kubwa za kitalii.

Alisema amevutiwa na uwapo wa chuo hicho ambacho kabla ya kujiunga alikuwa akifanya kazi za kutengeneza pikipiki (gereji) na ujuzi alioupata chuoni hapo utamsaidia katika kuongeza kipato.

Mwanafunzi mwingine, Asma Rashid, alisema muda mrefu ndoto yake ni kupika vyakula bora vyenye virutubisho kwa sasa amejifunza namna ya upishi bora ambao ni tofauti na alio uzoea kupika nyumbani kwao.

"Nimejifunza jinsi ya kupika chakula bora ambacho ni tofauti na upishi wa nyumbani nilio uzoea vyakula vya hotelini havitakiwi kuiva sana," alisema.

Kadhalika alisema, baada ya kumaliza mafunzo hayo ndoto yake ni kukidhi vigezo vya kupata ajira katika hoteli za kitalii.

Aliishauri jamii ya kizanzibari kuachana na zana potofu ya kuwa mtoto wa kike akifanya kazi katika hoteli atakiuka mila na silka ya Mzanzibari au kufanya vitendo kinyume na maadili.

Naye mwalimu wa chuo hicho, Robert Mkulu, alisema wanafunzi wanapata mafunzo kwa muda wa mwaka mmoja kwa nadharia na vitendo na kufanya kazi katika hoteli mbalimbali za kitalii.

Alisema wanafunzi wana uhakika wa kupata ajira kutokana na chuo hicho kuwa na mtandao mkubwa wa kuwaunganisha na hoteli mbalimbali za kitalii.

Alisema wanapokea wanafunzi mbalimbali wakiwamo wa vijijini na huwajenga kinadharia katika masuala ya nidhamu kuwahudumia wageni.


Mkuu wa chuo hicho, Talal Aturkhan alisema wamejipanga kutoa wanafunzi wenye uwezo na utaalamu wa kuendesha mambo ya utawala katika hoteli. Alisema mpaka 2023 chuo hicho kinatarajia kutoa wanafunzi 135 ambao watakua na uwezo wa kuendesha shughuli za hoteli.

"Nafasi nyingi za masuala ya uendeshaji wa hoteli zinashikiliwa na wageni kwa sababu wenyeji hawana uwezo na utaalamu hasa katika masuala ya uongozi," alisema.

Alisema moja ya changamoto kubwa ni masuala ya lugha kwa wanafunzi na anakusudia kuanzisha mafunzo ya lugha za kigeni ili kuendana na kasi ya soko la utalii.

Mkuu huyo aliahidi chuo hicho kitakuwa na uwezo wa kutoa wahitimu wenye uwezo na sifa na kuingia katika ushindani wa soko la ajira.

Mafunzo yanayotolewa chuoni hapo ni mapishi, uhudumu, usafi wa vyumba, upokeaji wa wageni na hudumu wa vinywaji.



HABARI KANDA YA ZIWA

# Madiwani wafurahishwa ongezeko watalii hifadhini

**Na Marco Maduhu,**
SERENGETI

MADIWANI wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, wameshangaa na kufurahishwa na uwapo wa watalii wengi katika Hifadhi ya Serengeti na Ngorongoro.

Wakiwa katika shughuli za utalii wa ndani juzi, madiwani hao walisema, tangu Rais Samia Suluhu Hassan atangaze vivutio vya utalii hapo nchini kupitia filamu ya The Royal Tour, mwitikio umekuwa mkubwa wa watu kufanya utalii wakiwamo Watanzania na wageni nje ya nchi.

Hassan Mwendapole, Diwani kutoka Kata ya Kambarage, alisema hajawahi kuona watalii wengi katika Hifadhi ya Serengeti, pamoja na uwanja wake wa ndege kutumika na watalii kwa muda mrefu huku wakiingia na kuondoka tofauti na miaka ya nyuma.

"Filamu ya Rais Samia ya The Royal Tour kutangaza vivutio vya utalii hapa nchini imezaa matunda, kumekuwa na ongezeko la watalii wengi sana kwenye hifadhi zetu," alisema Mwendapole.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alimpongeza Rais Samia kwa kutangaza vivutio vya utalii nchini, huku akitoa wito kwa Watanzania kumuunga mkono kwa kutembelea hifadhi hizo.

Alisema watalii wa ndani na nje ya nchi wanapokuwa wengi wakifanya utalii kwenye hifadhi, pato la taifa linaongezeka na fedha hizo zinarudi kwa wananchi wenyewe kutekelezwa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Aidha, Diwani wa Ndala, Zamda Shabani, alisema filamu ya The Royal Tour ndiyo imewahamasisha kwenda kufanya utalii kwa kutembelea hifadhi, na hiyo ni yake ya kwanza na kufikiria kitu kama hicho, lakini kwa sasa amejifunza mambo mengi pamoja na kuona wanyama mubashara.

Kwa upande wake Si Ging Cong mtalii wa kigeni kutoka nchini China, alisema anafarijika kutembelea hifadhi za taifa za Tanzania, kwa kuwa zina wanyama wengi wa kila aina hasa katika mbuga ya Serengeti.

## Serikali yatoa tani 200 mahindi ya ruzuku

**Na Mathias Marwa,** MUSOMA

SERIKALI imetoa msaada wa tani 200 za mahindi katika Manispaa ya Mji wa Musoma na Halmashauri ya Musoma Vijijini ili kusaidia wananchi kutokana na kupanda kwa bei ya chakula.

Akitoa mgawanyo wa mahindi hayo juzi, Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Khalfan Haule, alisema tayari tani 30 zimepokewa kwa ajili ya Manispaa ya Musoma na zingine 30 kwa ajili ya Musoma Vijijini.

Alisema tani 60 za mahindi ugawaji wake ulianza Jumamosi katika maeneo yaliyobainishwa kuwa ni Baruti kwa wananchi wa Manispaa Musoma, wananchi wa Musoma Vijijini ni Mugango na Bukima.

Pia tani nyingine 140 zitawasili wakati wowote na kwamba wananchi watauziwa mahindi hayo kwa bei nafuu ya Sh. 920 kwa kilo moja.

Alisema mahindi hayo yametolewa kutoka Ghala Kuu la Taifa la Serikali mkoani Shinyanga kutokana na malalamiko yaliyotolewa na wananchi wa Musoma kwa kuongezeka kwa bei ya chakula.

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, aliwataka watendaji, madiwani na wenyeviti wa vijiji na mitaa ugawaji kwa kuwaandaa wananchi na kuwapa mwongozo ili wapate huduma hiyo bila usumbufu.

Msaada huo umewafikia wananchi baada ya juhudi za Mkuu wa Wilaya kwa kushirikiana na Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini. Hivi karibuni, Muhongo aliongoza ugawaji miche 100,000 ya miti mbalimbali kwa wananchi wa jimbo lake kukabiliana na hali ya ukame inayotishia dunia.

Baadhi ya wananchi wameonesha wasiwasi wao kuwa huenda wasipate chakula hicho kwa uwiano wakihofia kuchukuliwa na matajiri na baadaye kuuzwa tena kwa bei ya juu.




Mkazi wa Magulu wilayani Kilosa, mkoani Morogoro (katikati), akionyesha shauku yake baada ya kupokea Sh. milioni 8 alizoshinda kwenye mchezo wa kubashiri matokeo wa Bikosports katika kilele cha Bonge Bonasi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaoendesha gari wakiongea na simu watakiwa kudhibitiwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JESHI la Polisi kitengo cha Usalama Barabarani, limetakiwa kuwabana madereva wanaoendesha vyombo vya moto wakiwa wanaongea na simu ili kupunguza matukio ya ajali nchini kunakosababisha ongezeko la watu wenye ulemavu.

Vitendo hivyo ambavyo vinafanywa mara nyingi na madereva wa mabasi yaendayo mikoani, husababisha kushindwa kuendesha kwa weledi na kuongeza wimbi la ajali nchini.

Hayo yalibainishwa jana na majeruhi wa ajali za magari waliokuwa wamelazwa Hospitali ya Manispaa ya Kahama, wakati walipotembelewa na viongozi wa Timu ya Mbasi FC na kutoa misaada yenye thamani ya Sh. 450,000.

Mmoja wa majeruhi hao, Boniphace Makoye alisema, ajali nyingi zinazotokea mara kwa mara hususani mabasi yaendayo mikoani inasababishwa na madereva wanaoendesha huku wakizungumza na simu za mkononi huku akiliomba Jeshi la Polisi Usalama Barabarani kudhibiti vitendo hivyo.

Naye Daudi Maziku alisema, kuna baadhi ya madereva wanadiriki kuachia usukani na kujibu jumbe za simu wanazotumiwa hasa za kifamilia na kuwachanganya hatimaye kushindwa kuendesha vyema na kusababisha ajali zinazopoteza maisha ya abiria wasiokuwa na hatia.

"Tumekuwa tukitoa taarifa juu ya mwenendo wa madereva wakati wa safari, lakini askari wetu wa usalama barabarani wanatusikia hawachukui hatua yoyote na pale inapotokea ajali ndiyo wanakumbuka kuchukua hatua huku walikuwa na uwezo wa kuzia kabla," alisema Maziku.

Muuguzi kutoka wodi ya kinamama waliojifungua kwa njia ya upasuaji na kawaida, Eveline Sakala, alisema wengi wao wanaojifungua hawana uwezo wa kukidhi mahitaji yao kama sabuni, taulo, soksi na kofia na msaada huo umefika kwa muda mwafaka.

Awali, mlezi wa timu hiyo, Anna Petro, alisema wameamua kuwatembelea wagonjwa wote katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama kwa niaba ya mawakala wa vituo vya mabasi vidogo vya majengo na CDT na kutoa misaada mbalimbali kwa kile wanachokipata katika kazi zao.

Alisema, vitu walivyotoa ni pamoja na sabuni katoni tano, dawa ya meno boksi mbili, miswaki 200, pamoja na juisi katoni saba vyote vikiwa na jumla ya Sh. 450,000 na kuwataka wengine kujitokeza na kusaidia wagonjwa.

## HABARI KIMATAIFA

# Viongozi G20 wawasili Indonesia

**BALI,** Indonesia

VIONGOZI kutoka mataifa yenye uchumi mkubwa zaidi duniani G20 wanaendelea kuwasili katika kisiwa cha Bali nchini Indonesia kwa ajili ya mkutano baada ya mlipuko wa janga la UVIKO-19 uliotawaliwa na msuguano kati ya Marekani na China.

Mkutano huo wa G20 unatokea katikawakati ambapo watu kutoka kila pembe ya dunia wanakabiliwa na gharama kubwa ya maisha ikiwamo kupanda kwa bei za vyakula na mafuta, mzozo wa vita nchini Ukraine na tishio la matumizi ya silaha za nyuklia.

Mkutano huo unachukuliwa na wengi kama fursa adimu kwa viongozi wa G20 kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazoikabili dunia. Pia inaelezwa kuwa ni mkutano mkubwa zaidi wa viongozi wa nchi zilizoendelea kiviwanda tangu kuanza kwa janga la ugonjwa wa UVIKO-19.

**Mshauri wa usalama wa kitaifa wa Marekani Jake Sullivan, alisema kuwa Biden atakuwa muwazi kwa Xi na anatarajia hilo pia kutoka kwa Rais huyo wa China.**

Waziri Mkuu wa Uingereza, Rishi Sunak, ambaye anahudhuria mkutano huo kwa mara ya kwanza tangu aingie madarakani, alitoa wito kwa mataifa yenye nguvu duniani kuungana dhidi ya unyonyaji wa uchumi wa dunia unaofanywa na wale aliowaita watendaji wabaya.

Baada ya kuwa Waziri Mkuu wa tatu wa Uingereza ndani ya mwaka mmoja, Sunak anatarajiwa kuwa na mkutano wake wa kwanza na Rais wa Marekani, Joe Biden pamoja na viongozi wengine wa dunia katika mkutano wa kilele kisiwani hapo.

Inatajwa kuwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, ushindani kati ya China na Marekani umeongezeka kwa kasi. Beijing inaonekana kuwa na nguvu na yenye ushawishi na inapambana kuwa taifa lenye nguvu kubwa duniani na kuchukua nafasi ya Marekani.

Mazungumzo ya jana ya ana kwa ana kati ya Biden na Xi pembezoni mwa mkutano huo, yana kumbukumbu kwa mbali kama mazungumzo ya vita baridi kati ya viongozi wa Marekani na muungano wa Sovieti huko Potsdam, Vienna ama Yalta ambayo yaliamua hatima ya mamilioni ya watu.

Biden aligusia kuhusu mkutano huo na Xi, na kutahadharisha juu ya kuvuka mstari mwekundu wa kila nchi kwa matumaini kwamba, ushindani kati yao hautakuwa chanzo cha nchi hizo mbili kuingia kwenye makabiliano na migogoro.

Mshauri wa usalama wa kitaifa wa Marekani Jake Sullivan, alisema kuwa Biden atakuwa muwazi kwa Xi na anatarajia hilo pia kutoka kwa Rais huyo wa China.

Maofisa walisema, Biden ataisukuma China kuionya Korea Kaskazini ambaye ni mshirika wake, baada ya nchi hiyo kufanya majaribio kadhaa ya silaha zake za nyuklia.

Aidha, Xi anatajwa kuwa huenda asiwe msaada mkubwa kwa Marekani na kwamba anaingia kwenye mkutano huo na Biden baada ya kuchaguliwa kwa muhula wa tatu wa kihistoria hivi karibuni na kumfanya kuwa kiongozi mwenye nguvu zaidi wa China.

Vile vile Biden, alitiwa nguvu na habari kwamba chama chake cha Democrats kimeendelea kudhibiti baraza la Seneti baada ya kupata matokeo mazuri kuliko ilivyotarajiwa katika uchaguzi wa katikati ya muhula.

Pia ilielezwa kuwa safari ya Rais wa Urusi Vladimir Putin, kushiriki katika mkutano huo umeingia doa kutokana na uvamizi wake wa kijeshi nchini Ukraine, huku ikielezwa kuwa amemtuma waziri wake wa mambo ya nje Sergei Lavrov kumwakilisha. **DW**

## Mahitaji muhimu yaanza kusambazwa Ukraine

**KYIV,** Ukraine

MAOFISA wa Ukraine wameanza kusambaza chakula, maji na dawa katika mji wa kusini wa Kherson, Ukraine baada ya vikosi vya nchi hiyo kuingia katika eneo hilo la kimkakati ambalo Urusi ilishikilia tangu kuanza kwa vita ambapo kwa sasa wamekimbia.

Hatua hiyo ilianza kutekelezwa mwishoni mwa wiki iliyopita, huku ikielezwa kuwa zaidi ya theluthi tatu ya wakazi 300,000 walikimbia mji na kubaki watu 75,000 kuwa chini ya uvamizi wa Urusi kabla ya kuondoka vikosi vya Moscow wiki iliyopita na vikosi vya Ukraine kuanza kusonga mbele.

Mshauri wa meya wa Kherson, Roman Golovnya, alisema vikosi vya Urusi wakati vipo katika eneo hilo vilifanya kila hila kuhakikisha watu waliosalia katika mji wanakabiliwa na hali ngumu.

Vikosi vya Ukraine vina hofu kwamba majengo mengi ya Kherson yanaweza kuwa yameharibiwa sana kama ilivyo katika miji mingine kama vile Mariupol na kwamba wameukuta uko madhubuti licha ya kuwa na kiwango kidogo cha usambazwaji wa maji.**VOA**





Waokoaji wakiwahi kwenye eneo lililotokea mlipuko Mtaa wa Istiklal mjini Istanbul, Uturuki juzi. **PICHA: RFI**

# Sita wauawa kwa bomu Uturuki

**INSTANBUL,** Uturuki

TAKRIBANI watu sita wameuawa na wengine 81 kujeruhiwa katika mlipuko uliotokea kwenye eneo lenye shughuli nyingi katikati mwa mji wa Istanbul, nchini Uturuki.

Gavana wa Jiji la Uturuki, Ali Yerlikaya, alisema mlipuko huo ulitokea juzi kwenye barabara ya maduka katika ya eneo la Taksim Square, na kuharibu miundombinu na maadhi ya vyombo vya usafiri.

Waziri wa Mambo ya Ndani, alibainisha kwamba mshukiwa wa tukio hilo ameshakamatwa.

Makamu wa Rais, Fuat Oktay, awali alisema mlipuko huo ulidhaniwa kuwa ni shambulio la kigaidi lililotekelezwa na mwanamke.

Rais Recep Tayyip Erdogan, wakati akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari mjini Istanbul, alilaani kile alichokiita shambulio baya, akisisitiza kuwa waliohusika wataadhibiwa na kwamba kulikuwa na harufu ya ugaidi.

Waziri wa Sheria, Bekir Bozdag, aliviambia vyombo vya habari vya Uturuki kuwa mwanamke mmoja alikuwa amekaa kwenye benchi katika eneo hilo kwa zaidi ya dakika 40, na kuondoka dakika chache kabla ya mlipuko huo kutokea.

Jana asubuhi Waziri wa Mambo ya Ndani Suleyman Soylu alisema mtu anayeshukiwa kuacha bomu amekamatwa na polisi na kukishutumu Chama cha Wafanyakazi wa Kurdistan (PKK) kwa kuhusika.

Kundi la PKK ni kundi la wanamgambo linalotaka kuwapo kwa taifa huru la Wakurdi ndani ya Uturuki. Na kwamba Umoja wa Ulaya na Marekani wanalichukulia kama shirika la kigaidi, huku ikielezwa kuwa hadi sasa hakuna aliyedai kuhusika na mlipuko huo.

Waziri wa serikali Derya Yanik, aliandika kwenye mtandao wake wa kijamii wa twetter kwamba mfanyakazi wa wizara ya serikali na binti yake mdogo walikuwa miongoni mwa waathiriwa. **BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**ALICE MUGISHA MAKAKA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0248-0004** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Marian Girls' Secondary mwaka 2014. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0264-0521** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Barbro Johanson Model Girls' Secondary mwaka 2017. Cheti cha Chuo chenye Registration namba **2017-04-0755**3 cha University of Dar es Salaam mwaka 2020. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/418719/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BENNO W SONGAMBELE**

Anatangaza kupotelewa kwa Kadi ya gari yenye usajili wa namba **T 875 DZW** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi kilicho karibu au piga simu namba **0784723401.**

**MOR/RUH/RB/441668/2022**

---

FORM 58

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 1015 OF 2022**
**In the matter of the Estate of the late IRENE CHRISTOPHER LUPEMBE**

**and**

**In the Matter of Application for Letters of Administration by ALEX JAMES NDYAMKAMA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 8 day of DECEMBER 2022
DATED AT DAR ES SALAAM this 04 day of NOVEMBER 2022.

Registrar/Senior Resident Magistrate

---

FORM 58

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 950 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late DANIEL MAKALA SHANGO**

**and**

**In the Matter of Application for Letters of Administration by MAGDALENA DANIEL SHANGO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 29 day of November, 2022.
Dated at DAR ES SALAAM this 18 day of October, 2022.

Senior Resident Magistrate

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 120 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late: EZEKIEL (MATATIZO) DICKSON NSEBELE**

**BY 1. EDINA GODFREY MGWABI**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 17day of NOVEMBER.........2022
Dated at MOROGO this 09 day of NOVEMBER.........2022

RESIDENT MAGISTRATE

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE DISTRICT COURT P.O. Box 660, Morogoro

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**ATHUMANI SULEMANI AHMED** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 389509** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 18/02/2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu naye. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/443186/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HAMIS RASHID ISSA**

Anatangaza kupotelewa kwa Kadi ya gari (**mitsubishi cattle**) yenye usajili wa namba **T 862EAP** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi kilicho karibu au piga simu no: **0755271985.**

**MOR/MOR/RB/442071/2022**

## KUPOTEA KWA KITAMBULISHO CHA URAIA NIDA

**DIANA MALAGI KAPELA**

Anatangaza kupotelewa kwa Kitambulisho cha uraia (NIDA), kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi kilicho karibu au piga simu no:**0742890905.**

**MOR/MOR/RB/432940/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa D,SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na 2184/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ALLY CHANZI WA KIUMBO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HASSANI ALLY CHANZI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 13 Mwezi 12 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 9 Mwezi 11 Mwaka 2022**

HAKIMU

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Elkana David Kaseko** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **Suzuki Swift T.604BTX** yenye jina la David Anderson Ruteri. Kwa yeyote atakaiona atoe taarifa kwenye kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Elkana David Kaseko kwa simu namna **0755-991574** ambaye ndiye mmliki wa gari hilo kwa sasa.

Taarifa ya Polisi
**SHI/SHI/RB/438882/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**BAHATI .M. MKENGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S1450/0519** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **EFATHA SEMINARY SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/435704/2022**

---

**BILO STAR DEBT COLLECTOR CO. LTD**
**WE ARE DEALING GENERAL AUCTIONING, DEBT COLLECTION, EVICTION, INVESTIGATION AND REPOSSESSION, STORAGE, COMMISSION AGENCY AND GENERAL BUSINESS.**

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **BILO STAR DEBT COLLECTOR COMPANY LIMITED** kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu tutauza kwa mnada wa hadhara magari ambayo ni kama yafuatayo:-

| MAELEZO YA MAGARI | ENEO LA MNADA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|
| Magari aina ya mabasi YUOTONG, DRAGON na ZHONGTONG | Ghala ya BILO STAR lililopo Mbezi Beach Dar es Salaam | Mnada utafanyika tarehe 26/11/2022 kuanzia saa tano asubuhi na kuendelea |

117147602

**MASHARTI YA MNADA**
Mnunuzi atakayefanikiwa kununua magari husika atalazimika kulipa 25% papohapo na kiasi kilichobaki 75% atatakiwa kulipa ndani ya siku 14 kuanzia tarehe yam nada. Akishindwa kulipa 25% aliyolipa haitarudishwa na mnada utarudiwa.

**KWA MAELEZO ZAIDI**
**Fika ofisi zetu zilizopo Mbezi Beach au wasiliana nasi kwa simu namba 0719206984, 0716943424 email: bilostarcompany@gmail.com , S.L.P 16095 DAR ES SALAAM.**


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail:**
**advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Inspeka, Nature sasa wajipanga kurudi upya

**Na Mwandishi Wetu**

WAKONGWE wa Bongo Fleva kutoka Temeke, Inspekta Haroun na Juma Nature, wamerudi kivingine baada ya kuandaa kazi yao mpya yenye nyimbo takribani sita.

Akizungumza na wanahabari, Inspekta alisema, kilichowapoteza kwenye gemu ilikuwa ni majukumu ya kimaisha, lakini kushindwa kuwekeza mzigo wa maana kwenye muziki kutokana na majukumu hayo.

"Tunamshukuru Mungu kwa sasa amejitokeza bwana Gaza ambaye amejitolea kuweka mzigo ili tuweze kurudi mjini.

"Tumeshafanya 'Mzee wa Busara' na kuna nyimbo nyingine kama sita hivi zitafuata.

"Tunaanza na hii ya Mzee wa Busara kwa sababu tunaona hili tatizo bado lipo mtaani, audio kafanya Mr T Touch na video kafanya Hanscana.

"Tunaachia audio na halafu video kisha mambo mengine yataendelea," alisema Inspekta.





# JANJARO: ASLAY HEBU TOA NGOMA MPYA

**Na Mwandishi Wetu**

MKALI wa Bongo Fleva, Janjaro, ameonyesha kukerwa na ukimya wa msanii mwenzake, Aslay Isihaka.

Janjaro amesema kuwa hapendezwi kabisa na ukimya wa mkali huyo pasipo kuachia kazi yoyote, tofauti na ilivyozoeleka wakati akiondoka katika bendi ya Yamoto.

"Tunataka muziki! Aslay mwaka ukiisha haujaachia muziki, tusizoeeeeane," aliandika Janjaro kupitia Instagram yake kwa msisitizo.

Itakumbukwa, Aslay kwa sasa yupo chini ya usimamizi wa Rockstar Africa ambapo Agosti mwaka huu alitangaza rasmi kusainishwa nao.

Mara yake ya mwisho kuachia wimbo ilikuwa ni Januari 21, mwaka 2021, ambapo aliachia video ya wimbo wake uitwao "Nashangaa".

# *Rayvanny adai sasa anasaka mchumba*

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva, Rayvanny, amefichua kwamba yuko singo na tayari kusaka mchumba.

Kupitia ukurasa wake rasmi wa Instagram, Rayvanny amewataka wanawake wanaommezea mate kumtumia ujumbe wa moja kwa moja.

"Jamani kama unajijua ni binti mzuri na unanifaa, tafadhali naomba unitongoze," Rayvanny aliandika.

Hata hivyo, mkali huyo wa kibao cha Zezeta, alisema baada ya tangazo hilo simu yake ilijaa jumbe za mahaba kutoka kwa wanawake waliokiri wanampenda.

Rayvanny alisambaza zaidi ya jumbe 50 alizopokea kwenye Insta Stories, na kufichua kuwa alikuwa amepokea zaidi ya jumbe 200 za mahaba kutoka kwa wanawake tofauti.

"Sikujua kwamba mnanipenda kiasi hiki. Hata mimi nawapenda sana nyote. Leo nimekuja kugundua kwamba kweli dunia imejaa wanawake warembo sana. Ila mwisho wa siku siwezi kuwa nao wote, nahitaji mwanamke mmoja tu.

"Nimepokea zaidi ya jumbe 200 za mahaba kutoka kwa wanawake tofauti kwa saa chache tu, na zingine zinamiminika. Sikutarajia hili hata kidogo. Nawapenda sana nyote na ikiwa unanipenda pia nitongozee," aliandika."



# AZAM FC, RUVU SHOOTING KUTOANA JASHO CHAMAZI

Na Saada Akida

WAKATI Azam FC ikiikaribisha Ruvu Shooting leo katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaopigwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, makocha wa timu hizo kila mmoja ameeleza dhamira yake ya kuibuka na pointi tatu katika mechi hiyo.

**Azam FC wanashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 4-3 katika mechi yao ya mwisho walicheza dhidi ya Mtibwa Sugar Uwanja wa Manungu, Morogoro wakati Ruvu Shooting wataingia uwanjani baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Tanzania Prisons, kwenye mchezo wa ligi hiyo uliopigwa katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.**

Hata hivyo, timu hizo zinashuka dimbani zikijivunia kufanya maandalizi mazuri kwa kila mmoja kuhitaji alama tatu muhimu ili kujiweka katika nafasi nzuri katika msimamo wa ligi hiyo, ambayo Yanga ipo kileleni baada ya kucheza mechi tisa.

Endapo Azam FC yenye alama 23 sawa na Yanga, lakini yenyewe ikicheza mechi 11, ikishinda leo itakaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo huku Ruvu Shooting ambayo nayo imecheza michezo sawa na wapinzani wao hao lakini ikiwa na pointi 11 katika nafasi ya 12, ikipata alama tatu inaweza kupanda hadi nafasi ya 10.

Akizungumzia mchezo huo, Kaimu Kocha Mkuu wa Azam FC, Kali Ongala, alisema wamejipanga zaidi ili kufanikisha malengo yao ya kuendelea kuzoa pointi tatu katika ligi hiyo.

Alisema anazidi kuyafanyia kazi makosa ya safu yake ya ulinzi ili yasijirudie katika mchezo wao dhidi ya Ruvu Shooting baada ya mechi iliyopita kuwa mbele kwa mabao 3-0, lakini wakazembea na kujikuta yakisawazishwa kabla ya kupata la ushindi jioni.

"Tumejiandaa vizuri, wachezaji wako tayari kwa ajili ya kupata pointi tatu, mechi itakuwa ya ushindani mkubwa na tutacheza kwa nidhamu kubwa kutokana na ubora wa wapinzani wetu," alisema Kali.

Nahodha wa Azam FC, Sospeter Bajana, alisema wamejipanga vizuri kuelekea mchezo huo wa leo kwa ajili ya kupambania alama tatu.

"Mechi ni ngumu kwa sababu ya matokeo ya nyuma ya wapinzani wetu, lakini kwa upande wetu pia kwa sababu tunahitaji kupata pointi muhimu ili kufikia malengo yetu," alisema Bajana.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Ruvu Shooting, Rajab Mohamed, alisema kuelekea mechi hiyo wachezaji wao wanamorali kubwa ya ushindi.

"Tumejipanga vizuri kuelekea mchezo wetu wa kesho (leo), tunawaheshimu Azam FC kwani ina wachezaji wazuri, lakini tumejipanga kukabiliana na wapinzani wetu kupata matokeo chanya," alisema kocha huyo.

Mchezo mwingine utakaochezwa leo ni kati ya KMC FC dhidi ya Dodoma Jiji FC, ambao utapigwa katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

HUPITI...




Kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto' akimhadaa beki wa Kagera Sugar, David Luhende, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza juzi na kumalizika kwa Yanga kushinda bao 1-0. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# KMKM yatangaza vichapo Ligi Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM, baada ya kufanya vibaya michezo sita katika ligi hiyo msimu huu, wamesema sasa wamerejea kuhakikisha wanashinda michezo iliyosalia kabla ya kwenda katika usajili wa dirisha dogo.

KMKM imepaa hadi nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikitokea nafasi ya tano baada ya kushinda mchezo wake wa jana kwa mabao 3-0 dhidi ya vinara wa ligi hiyo, timu ya Malindi SC.

Hadi sasa KMKM imeshinda jumla ya michezo sita, sare nne na kafungwa michezo miwili kati ya 12 iliyocheza, jambo ambalo inaona ni matokeo mabaya kwa upande wao.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha wa KMKM, Ame Msimu, alisema wamerejea katika kasi waliyoanza nayo mwanzoni mwa ligi baada ya kufanya vibaya katika mizunguko iliyopita.

Alisema kufanya vibaya kwa timu kwa kipindi kifupi ni kawaida katika mpira hasa katika ligi yenye ushindani kwa kuwa kila timu inahitaji kupata alama tatu kila inaposhuka dimbani.

"Hatukufanya vizuri mechi sita, ni michezo mingi ikilinganishwa na ukubwa wa timu yetu, lakini sasa tunaendelea na mipango yetu ili timu ifanye vizuri michezo iliyobaki," alisema.

Aidha, alisema ameyafanyia kazi mapungufu mengi aliyoyaona katika michezo iliyopita ikiwamo suala la kuongeza umakini kwa safu ya ulinzi na ushambuliaji.

Hata hivyo, alisema wanaendelea kujipanga kuhakikisha mchezo wao wa 13 dhidi ya Black Sailor utakaochezwa Novemba 20, mwaka huu wanatapata ushindi.

**Hatukufanya vizuri mechi sita, ni michezo mingi ikilinganishwa na ukubwa wa timu yetu, lakini sasa tunaendelea na mipango yetu ili timu ifanye vizuri michezo iliyobaki.**

# *JKT Tanzania kileleni Championship*

Na Adam Fungamwango

MAAFANDE wa JKT Tanzania kwa mara ya kwanza wamekaa kileleni mwa Ligi ya Championship ikiiengua Fountain Gate, baada ya kuwasasambua maafande wenzao wa Trasit Camp mabao 4-0 katika mechi iliyochezwa Jumamosi katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Wakati JKT Tanzania ikitoa kipigo hicho, timu ya Fountain Gate iliyokuwa ikiongoza ligi hiyo kusaka timu za kucheza Ligi Kuu msimu ujao, ilikubali kipigo cha mabao 2-1 Jumapili kwenye uwanja huo wa Uhuru, dhidi ya Pan African.

Matokeo ya mechi hizo mbili yameonekana kubadilisha msimamo wa ligi hiyo kwenye raundi ya tisa, kwani JKT Tanzania sasa inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 22, huku Fountain Gate ikishushwa kwenye nafasi ya pili kwa kubaki na pointi zake 21.

Timu ya Mbuni ambayo iliongoza kwa kipindi kirefu kwenye msimamo wa ligi hadi raundi ya saba, juzi ilipata kipigo kingine cha bao 1-0 dhidi ya Mbeya Kwanza, mechi ikichezwa Uwanja wa Majimaji Songea, hivyo kushuka tena hadi nafasi ya tano ikiwa na pointi zake 18.

Matokeo ya mechi zingine za ligi hiyo ni Biashara United kuichapa Kitayosce mabao 2-0 ikiwa nyumbani, Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara, Kengold ikaidungua African Sports bao 1-0 kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, huku Pamba ikiadhibu Green Warriors mabao 3-2 Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BELLINGHAM NA MAZUNGUMZO

MTENDAJI Mkuu wa Borussia Dortmund, Hans-Joachim Watzke, amesema klabu hiyo itafanya mazungumzo na kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19, ambaye amekuwa akihusishwa na timu kadhaa kubwa za Ulaya, kuhusu mustakabali wake baada ya Kombe la Dunia la 2022. ***(Bild, via Mail)***

### TIELEMANS ATAKIWA BARCA

BARCELONA ambao wanajua itakuwa vigumu kumsajili kiungo wa kati wa Ujerumani, Ilkay Gundogan, mwenye umri wa miaka 32, kutoka Manchester City Januari, pia wanamtazama kiungo wa kati wa Leicester City na Ubelgiji, Youri Tielemans, 25. ***(AS Mundo Deportivo)***

### XAVI HANA TATIZO

BARCELONA ilishindwa kutinga hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini rais wa klabu hiyo ya Nou Camp, Joan Laporta, amesema hajatilia shaka nafasi ya Xavi kama kocha. ***(Sport)***

### HAZARD AWINDWA VILLA

KOCHA wa Aston Villa, Unai Emery, anataka kusajili wachezaji wawili kutoka Real Madrid - winga wa Ubelgiji, Eden Hazard mwenye umri wa miaka 31, na mlinzi wa Hispania, Nacho Fernandez, 32. ***(El Nacional)***

### ZIYECH AWANIWA MILAN

AC Milan wanalenga kukubaliana na Chelsea kumsajili winga wao wa Morocco, Hakim Ziyech, mwenye umri wa miaka 29 katika dirisha la Januari. ***(Gazzetta dello Sport, Via Football Italia)***

### LEAO EURO MIL 100

AC Milan haitazingatia ofa za chini ya euro 100 kwa fowadi wa Ureno, Rafael Leao Januari huku wakihangaika kupiga hatua katika mazungumzo ya kuafiki kuongeza mkataba na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Calciomercato - Via Italy)***

### PINTO AMSHANGAA SOUTHGATE

MKURUGENZI wa AS Roma, Tiago Pinto "hawezi kukubali" hoja ya kocha wa England, Gareth Southgate ya kumuacha mshambuliaji Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 25 kwenye kikosi chake kwa ajili ya Kombe la Dunia la 2022. ***(DAZN, Via Football Italia)***

### RUDIGER NA BARCA

MLINZI wa Ujerumani, Antonio Rudiger, ambaye aliondoka Chelsea na kujiunga na Real Madrid msimu wa majira ya joto, amesema Barcelona walijaribu kumsajili, lakini kuhamia Nou Camp haikuwezekana kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(AS)***

### VERRATTI KUONGEZA MKATABA

KIUNGO wa kati wa Italia, Marco Verratti mwenye umri wa miaka 30, anakaribia kusaini mkataba wa nyongeza hadi 2026 na mabingwa wa Ufaransa, Paris St-Germain. ***(Mundo Deportivo)***

### DZEKO ATAKA KUBAKI

MKATABA wa mshambuliaji wa Bosnia, Edin Dzeko na Inter Milan unamalizika msimu ujao wa majira ya joto na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 amesema anataka kusalia na timu hiyo ya Serie A. ***(Calciomercato - Via Italy)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO ATEMA NYONGO UNITED, AMCHANA KOCHA

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester United, Cristiano Ronaldo, amesema anahisi kusalitiwa na Manchester United na kwamba analazimishwa kuondoka katika klabu hiyo.

**Mchezaji huyo raia wa Ureno sasa amevunja ukimya katika mahojiano na Piers Morgan kwenye kipindi cha runinga cha TalkTV.**

Klabu ya Manchester United imeombwa kutoa tamko ili kujibu madai hayo ya Ronaldo.

United ambayo iliichapa Fulham mabao 2-1 Jumapili, iko katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu England chini ya Kocha Erik ten Hag katika msimu wake wa kwanza.

Alipoulizwa iwapo uongozi wa United ulikuwa unajaribu kumfukuza katika klabu hiyo, Ronaldo alisema: "Ndiyo, si tu kocha (Erik ten Hag), lakini watu wengine wawili au watatu katika klabu. Ninahisi kusalitiwa."

Na alipoulizwa tena kama viongozi wakuu wa klabu walikuwa wakijaribu kumtimua, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, alisema: "Sijali. Watu wanapaswa kusikiliza ukweli.

> Nahisi kusalitiwa na kama watu wengine hawanitaki hapa, siwezi kumheshimu Ten Hag kwa...

"Ndio, nilihisi kusalitiwa na nilihisi kama watu wengine hawanitaki hapa, si mwaka huu tu bali mwaka jana pia."

Ronaldo hajachezeshwa tangu United ikipigwa mabao 3-1 dhidi ya Aston Villa Novemba 6, mwaka huu.

Aliondolewa kwenye mechi ya ligi dhidi ya Chelsea mwezi uliopita na Ten Hag baada ya kukataa kuingia kama mchezaji wa akiba dhidi ya Tottenham Hotspur.

"Siwezi kumheshimu Ten Hag kwa sababu haonyeshi kuniheshimu," alisema Ronaldo akimwambia Morgan. "Ikiwa huniheshimu, na mimi sitakuheshimu."

Mahojiano hayo yataonyeshwa kwa siku mbili usiku wa Jumatano na Alhamisi.

"Nadhani mashabiki wanapaswa kujua ukweli. Naitakia mema klabu hii. Hii ndiyo sababu nilikuja Manchester United. "Tangu (kocha wa zamani) Sir Alex (Ferguson) alipoondoka, sijaona mabadiliko yoyote katika klabu. Hakuna kilichobadilika.

"Ninaipenda Manchester United, ninawapenda mashabiki, daima wapo upande wangu. Lakini kama wanataka kufanya hivyo tofauti... inabidi wabadilishe mambo mengi."

Ronaldo amesema mtazamo wake kuhusu klabu hiyo unafanana na Ferguson, ambaye alikuwa muhimu katika kurejea kwake Old Trafford kutoka Juventus ilipoonekana huenda akajiunga na Manchester City.

"Anajua zaidi ya mtu yeyote kwamba klabu haiko kwenye njia inayostahili kuwa," aliongeza Ronaldo. "Anajua. Kila mtu anajua. Watu ambao hawaoni hilo ... ni kwa sababu hawataki kuona; wao ni vipofu."

**KUHUSU RANGNICK**

Ole Gunnar Solskjaer alikuwa kocha wa United wakati Mreno huyo aliporejea klabuni hapo kabla nafasi yake kuchukuliwa na Ralf Rangnick na kisha kocha wa sasa Ten Hag.

Kuhusu Rangnick, Ronaldo alisema: "Kamwe hakuwahi kumjua. Utawezaje kuwa bosi wa Manchester United? Sijawahi hata kumsikia."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,051,2

JACKPOT MECHI WIKI HII
TAREHE: 15, 16 NA 17 NOVEMBA 2022
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 15/11/22 | 22:45 | Hartlepool vs Solihull Moors | 2.81 | 3.35 | 2.32 |
| 02. 15/11/22 | 22:45 | Buxton FC vs Scarborough Athletic | 2.28 | 3.26 | 2.82 |
| 03. 16/11/22 | 04:00 | Atletico Huila vs Chico | 2.91 | 2.77 | 2.53 |
| 04. 16/11/22 | 20:00 | Rimini vs Vicenza | 2.37 | 3.50 | 2.75 |
| 05. 16/11/22 | 21:00 | Cyprus vs Bulgaria | 3.14 | 3.19 | 2.34 |
| 06. 16/11/22 | 22:00 | ADO Den Haag vs Roda Kerkrade | 2.46 | 3.49 | 2.56 |
| 07. 16/11/22 | 22:30 | Mexico vs Sweden | 2.20 | 3.23 | 3.38 |
| 08. 16/11/22 | 22:30 | Foggia vs Crotone | 3.00 | 3.30 | 2.31 |
| 09. 17/11/22 | 05:00 | Nicaragua vs EL Salvador | 3.07 | 3.37 | 2.28 |
| 10. 17/11/22 | 19:00 | Teplice vs Zbrojovka Brno | 2.43 | 3.17 | 2.68 |
| 11. 17/11/22 | 22:45 | Ireland vs Norway | 2.37 | 3.43 | 2.88 |
| 12. 17/11/22 | 23:00 | Jong AZ Alkmaar vs Jong Ajax | 2.70 | 3.75 | 2.32 |
| 13. 17/11/22 | 23:30 | Penafiel vs Moreirense | 3.09 | 3.09 | 2.36 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# POCHETTINO: NATAKA TIMU YA LIGI YA MABINGWA

**LONDON,** England

ALIYEKUWA Kocha wa Paris Saint-Germain, Mauricio Pochettino, anataka kazi yake inayofuata ya ukocha iwe katika klabu yenye uwezo wa kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya uzoefu wake wa kufanya kazi na Kylian Mbappe, Lionel Messi na Neymar.

Pochettino aliondoka PSG Julai, baada ya kushinda taji la Ligue 1 msimu uliopita huku wakitolewa Ligi ya Mabingwa Ulaya na kushindwa kuchukua taji hilo mwaka uliofuata.

Pochettino ambaye amewahi kuinoa Tottenham Hotspur, alishindwa kuifikisha timu katika hatua ya robo fainali licha ya kuwa na kikosi chenye nyota wengi wenye uwezo na kuangushwa na Real Madrid katika mechi ya hatua ya 16-bora.

Pochettino amekuwa hana kazi tangu aondoke PSG licha ya kuwa na ofa nyingi na sasa ameeleza ni nini hasa anachotafuta katika mradi mpya, na alisema kuwa kuhusu kuzungumza miradi katika soka ni vigumu sana.

"Baada ya kuwa katika klabu na Mbappe, Messi, Neymar, ni kawaida kwamba ningetafuta kudumisha kiwango hicho. Klabu ambayo inatoa nafasi ya kulenga makubwa zaidi, kama kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya itakuwa bora," alisema.

Kuhusu Messi, ambaye ana uwezekano wa kushinda Kombe la Dunia akiwa na Argentina huko Qatar 2022 baadaye mwezi huu, Pochettino anahisi kuwa Argentina wana uwezo wa kutwaa taji hilo msimu huu.



## Rooney atetea kuitwa Maguire, Trent

**LONDON,** England

WAYNE Rooney ameunga mkono hadharani uteuzi wa kikosi cha England chini ya kocha Gareth Southgate kuelekea Kombe la Dunia, akikiri kwamba hajali kujumuishwa kwa nyota wasio na kiwango Harry Maguire na Trent Alexander-Arnold.

Rooney, mfungaji bora wa muda wote wa Manchester United, England, amejaribu kutuliza ghadhabu iliyotokana na baadhi ya wachezaji wanaotiliwa shaka na Southgate, hasa nahodha wa United, Maguire na Alexander-Arnold wa Liverpool.

Southgate amekosolewa kwa kuchagua wachezaji kulingana na mafanikio ya zamani badala ya kiwango cha sasa.

Akiandika katika gazeti la Sunday Times, mshambuliaji huyo alisema kuna mijadala 'iliyotiwa chumvi' iliyozunguka kambi ya England.

"Kumekuwa na mijadala mingi, lakini Trent anakupa kitu tofauti, hofu kuhusu udhaifu wake wa kiulinzi imetiwa chumvi. Ndio, ameanzishwa mara chache msimu huu, lakini nadhani hiyo inaakisi zaidi Liverpool kama timu kuliko yeye binafsi," Rooney alisema.

Maguire ameichezea Man United mechi nne pekee za Ligi Kuu msimu huu.

07,683/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/11/22 | 18:00 | Fleetwood Town vs Bolton Wanderers | 3.05 | 3.35 | 2.24 |
| 02. 19/11/22 | 18:00 | Burton Albion vs Plymouth Argyle | 2.65 | 3.40 | 2.50 |
| 03. 19/11/22 | 18:00 | Port Vale vs Charlton Athletic | 2.33 | 3.35 | 2.90 |
| 04. 19/11/22 | 18:00 | Cambridge United vs Accrington Stanley | 2.40 | 3.35 | 2.80 |
| 05. 19/11/22 | 18:00 | Colchester United vs Doncaster Rovers | 2.27 | 3.25 | 3.10 |
| 06. 19/11/22 | 18:00 | Grimsby Town vs Stevenage FC | 3.00 | 3.25 | 2.32 |
| 07. 19/11/22 | 18:00 | Cove Rangers FC vs Greenock Morton FC | 2.55 | 3.35 | 2.60 |
| 08. 19/11/22 | 18:00 | Inverness Caledonian Thistle FC vs Ayr United FC | 2.90 | 3.45 | 2.31 |
| 09. 19/11/22 | 18:00 | Queen of The South FC vs Montrose FC | 2.48 | 3.40 | 2.70 |
| 10. 19/11/22 | 18:00 | Albion Rovers FC vs Stranraer FC | 2.38 | 3.40 | 2.80 |
| 11. 19/11/22 | 18:00 | Annan Athletic FC vs Elgin City FC | 2.31 | 3.40 | 2.90 |
| 12. 19/11/22 | 18:15 | SD Ponferradina vs Real Oviedo | 2.55 | 3.05 | 2.85 |
| 13. 19/11/22 | 20:30 | Sporting Gijon vs CD Leganes | 2.28 | 3.05 | 3.30 |
| 14. 19/11/22 | 22:00 | MVV Maastricht vs Almere City FC | 2.60 | 3.60 | 2.45 |
| 15. 20/11/22 | 19:00 | Sakaryaspor vs Bandirmaspor | 2.80 | 3.30 | 2.45 |
| 16. 20/11/22 | 19:00 | Qatar vs Ecuador | 3.30 | 3.10 | 2.26 |
| 17. 20/11/22 | 21:00 | Racing Santander vs Burgos CF | 2.30 | 2.95 | 3.40 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE- 15/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2106 | Aizawl FC vs Tiddim Road Athlectic Club | 2.14 | 3.26 | 3.07 |
| 14:00 | 4746 | Consadole Sapporo vs Kawasaki Frontale | 3.91 | 3.86 | 1.71 |
| 16:00 | 1779 | KMC vs Dodoma FC | 2.00 | 2.92 | 3.89 |
| 16:30 | 1981 | US Monastir vs Avenir Rjich | 1.83 | 2.81 | 5.04 |
| 16:30 | 3321 | Africain vs Olympique de Beja | 1.62 | 3.12 | 6.23 |
| 16:30 | 3779 | Churchill Brothers vs Rajasthan United | 1.97 | 3.30 | 3.45 |
| 16:30 | 5654 | CS Chebba vs CS Sfaxien | 3.16 | 2.58 | 2.53 |
| 17:00 | 1561 | ES EL Ghozlane vs USM EL Harrach | 2.00 | 3.06 | 3.65 |
| 17:00 | 1670 | AS Khroub vs CA Batna | 1.91 | 3.30 | 3.64 |
| 17:00 | 1827 | WA Boufarik vs Ben Aknoun | 1.81 | 3.40 | 4.50 |
| 17:00 | 3390 | GC Mascara vs Skaf Khemis Miliana | 2.05 | 2.93 | 3.71 |
| 17:00 | 3752 | RC Kouba vs SC Mecheria | 2.31 | 3.15 | 2.86 |
| 17:00 | 4038 | Hamra Annaba vs USM Annaba | 2.44 | 3.03 | 2.78 |
| 17:00 | 4059 | Ib Khemis El Khechna vs MO Constantine | 2.26 | 3.06 | 3.01 |
| 17:00 | 4256 | US Chaouia vs NRB Teleghma | 2.04 | 3.10 | 3.49 |
| 17:00 | 4754 | MC Saida vs ZR Temouchent | 3.00 | 2.76 | 2.47 |
| 17:00 | 4881 | Ol. Medea vs WA Tlemcen | 1.94 | 3.25 | 3.60 |
| 17:00 | 5265 | JSM Skikda vs Irb Ouargla | 2.63 | 2.88 | 2.68 |
| 17:00 | 5666 | ASM Oran vs MCB Oued Sly | 2.32 | 2.92 | 3.07 |
| 17:00 | 5978 | RC Relizane vs ES Mostaganem | 4.76 | 3.31 | 1.70 |
| 18:10 | 1696 | Ohud Medina vs Al Faisaly (KSA) | 4.37 | 3.06 | 1.84 |
| 19:00 | 5303 | Hilal Al-Quds vs Shabab Alsamu | 1.39 | 4.56 | 6.22 |
| 19:00 | 5786 | Azam vs Ruvu Shooting | 1.46 | 4.20 | 6.80 |
| 19:15 | 2400 | Romania W vs Czech Republic W | 4.86 | 3.69 | 1.60 |
| 19:40 | 3996 | AL Hazm vs Al Jabalain | 1.86 | 3.31 | 3.85 |
| 21:15 | 4388 | Brazil W vs Canada W | 1.89 | 3.41 | 3.60 |
| 21:30 | 1725 | Sangiuliano City Nova vs Juventus U23 | 2.12 | 3.16 | 3.21 |
| 21:30 | 3383 | FC Otelul Galati vs FCM Baia Mare | 1.59 | 3.68 | 5.04 |
| 21:30 | 5048 | Atletico Pulpileno vs UD Caravaca | 1.70 | 3.45 | 5.20 |
| 22:00 | 4994 | FUS Rabat vs RS Berkane | 2.13 | 2.77 | 3.70 |
| 22:45 | 1566 | Southport vs Kings Lynn | 3.15 | 3.40 | 2.05 |
| 22:45 | 1758 | Braintree vs Farnborough Town | 2.38 | 3.26 | 2.68 |
| 22:45 | 1966 | Derby vs Torquay | 1.09 | 8.28 | 19.72 |
| 22:45 | 2244 | Bracknell Town vs Yate Town | 1.50 | 4.46 | 4.75 |
| 22:45 | 2784 | Buxton FC vs Scarborough Athletic | 2.43 | 3.26 | 2.62 |
| 22:45 | 2857 | Cambridge Utd vs Curzon | 1.39 | 4.63 | 6.70 |
| 22:45 | 3077 | Folkestone Invicta vs Aveley FC | 2.29 | 3.65 | 2.58 |
| 22:45 | 3354 | Chippenham Town vs Havant and Waterlooville | 3.40 | 3.45 | 1.94 |
| 22:45 | 3398 | Dunfermline vs Celtic Glasgow B | 1.60 | 4.10 | 4.30 |
| 22:45 | 3409 | Nantwich Town vs Gainsborough | 3.32 | 3.37 | 1.99 |
| 22:45 | 3637 | Cheshunt vs Ebbsfleet | 7.99 | 5.07 | 1.29 |
| 22:45 | 4191 | Gillingham vs AFC Fylde | 1.85 | 3.35 | 4.04 |
| 22:45 | 4296 | AFC Wimbledon vs Weymouth | 1.28 | 5.33 | 8.49 |
| 22:45 | 4423 | Oxford City vs Dover | 1.83 | 3.51 | 3.71 |
| 22:45 | 4631 | Billericay Town vs AFC Hornchurch | 3.01 | 3.79 | 1.98 |
| 22:45 | 5226 | Hereford United vs Peterborough Sports | 2.04 | 3.40 | 3.16 |
| 22:45 | 5472 | Hendon vs Merthyr Town | 2.41 | 3.46 | 2.53 |
| 22:45 | 5499 | Alvechurch vs Mickleover Sports | 2.27 | 3.44 | 2.71 |
| 22:45 | 5503 | Hartlepool vs Solihull Moors | 2.81 | 3.35 | 2.32 |
| 23:00 | 2778 | Marsa FC vs Melita FC | 2.92 | 3.50 | 2.12 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MAYANGA AVURUNGWA MTIBWA KUPIGWA NYINGI

**Na Hadija Mngwai**

KIPIGO cha mabao tisa katika mechi mbili zilizoongozana, kimemvuruga Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Salum Mayanga, ambaye ameeleza sasa anaingia 'msituni' kutafuta dawa ya safu yake ya ulinzi.

**Mtibwa Sugar imejikuta ikipoteza michezo miwili mfululizo dhidi ya Simba ambayo iliwachakaza mabao 5-0 na dhidi ya Azam FC iliyoitandika 4-0 na kuifanya kuloa mabao tisa.**

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, alisema kikosi chao kilifanya makosa katika michezo miwili iliyopita jambo linalomuumiza kichwa kocha mkuu hivyo kuanza kutafuta tiba baada ya kugundua madhaifu ya nyota wake.

"Kwa kweli hatukufanya vizuri katika michezo yetu miwili iliyopita, tumefungwa mabao mengi, matano dhidi ya Simba na manne dhidi ya Azam FC, kuna uzembe ulifanyika kwa mabeki. Mwalimu Mayanga ameshabaini mapungufu, hivyo anaangalia jinsi ya kumaliza tatizo hilo.

"Ligi ni ngumu na ina ushindani wa hali ya juu, tunaendelea kujiimarisha ili kufanya vizuri michezo inayofuata," alisema Kifaru.

Akizungumzia mechi inayofuata dhidi ya Coastal Union kesho, Jumatano, alisema: "Tunajua tunakibarua kigumu, lakini kocha amekipanga kikosi chake kuhakikisha kinafanikiwa kushinda mchezo huo tutakaocheza katika Uwanja wetu wa nyumbani wa Manungu.

"Kikosi kipo vizuri, hakuna majeruhi ya kutisha yaliyokuwapo ni ya kawaida, hivyo tunaendelea na mazoezi ili kufanya vizuri".

Mtibwa Sugar ipo nafasi ya saba kwenye msimamo wa ligi hiyo baada ya kushuka dimbani mara 11 na kujikusanyia pointi 15 huku Coastal Union ambayo watacheza nayo kesho, ikiwa na alama 12 katika nafasi ya 11 baada ya kucheza mechi tisa hadi sasa.

UTAMBULISHO...



Balozi wa Kampuni ya Mo Green International inayojishughulisha na usambazaji wa pembejeo za kilimo, Burton Mwemba 'Mwijaku', akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana wakati wa hafla ya kutambulisha Bendi ya Town Classic inayomilikiwa na kampuni hiyo. Katikati ni meneja wa bendi hiyo, Andrew Sekidia na Ofisa Uhusiano wa kampuni hiyo, Kessa Mwambeleko. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Nabi na kiwango kibovu

INATOKA UKURASA 32

chocheza leo, kitu kikubwa ilikuwa ni kupata pointi tatu, kiwango tunaweza kukionyesha vizuri siku ya Alhamisi," alisema.

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Mexime, yeye amewapongeza Yanga kwa kuvumilia mashambulizi yao, akiongeza kuwa waliwashika kila idara, lakini tatizo lilikuwa ni bahati tu.

"Nilishaongea Simba na Yanga wana wachezaji ambao wanatembea na matokeo mkononi na miguuni mwao, na ndicho kilichotokea. Nilisema hivyo nina maana kuwa wachezaji wa timu hizo wanaweza kukuadhibu kwa kufanya kosa moja tu kwani wao wanachohitaji zaidi ni ushindi na wana wachezaji wengi wanaoweza kuamua mechi.

Nafikiri wao wamepata nafasi moja tu na ndiyo hiyo wameitumia, lakini sisi ndiyo tumeichukua hii mechi, hadi penalti tumepata hatukuwa na bahati tumeipoteza, yote kwa yote nawapongeza Yanga kwa kuweza kuvumilia mashambulizi tuliyokuwa tunawapelekea langoni mwao, kuishika timu kama Yanga ambayo haijapoteza mechi," alisema Mexime.

## *Mgunda awavalia njuga Kibu, Kyombo*

INATOKA UKURASA 32

kupata ushindi katika mchezo huo ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Simba wanashuka dimbani kesho kuwakaribisha Namungo FC katika Uwanja wa Benjamin Mkapa majira ya saa 1:00 usiku, ikihitaji ushindi ili kuendelea kujiweka katika mbio za ubingwa.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Simba ambayo ina alama 21 baada ya mechi 10, inashika nafasi ya tatu nyuma ya Azam FC na vinara Yanga zenye pointi 23 kila moja.

Hata hivyo, Azam ambayo leo itaikaribisha Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, yenyewe imecheza mechi 11 huku Yanga ikiwa imeshuka dimbani mara tisa tu hadi sasa.

# Michezo

Jumanne Novemba 15, 2022

Nipashe




Ronaldo atema nyongo United UKURASA 29

# Mgunda awavalia njuga Kibu, Kyombo

●●● Asema hakuna namna lazima safu ya ushambuliaji Simba sasa kieleweke baada...

**Na Saada Akida**

KAIMU Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amekiri kuwapo kwa kazi ya kufanya katika safu yake ya ushambuliaji kutokana na kupoteza nafasi nyingi za mabao wanazotengeneza katika michezo iliyopita.

**Safu ya ushambuliaji ya Simba inayoongozwa na Moses Phiri, Kibu Denis na Habib Kyombo, imekuwa butu katika michezo miwili iliyopita ambapo ilishindwa kuipa timu ushindi dhidi ya Singida Big Stars baada ya kutoka sare ya bao 1-1 huku Jumamosi ikipata ushindi mwembamba wa bao 1-0 dhidi ya Ihefu FC shukrani kwa Pape Sakho aliyeipa pointi tatu.**

Akizungumza na Nipashe jana, Mgunda alisema amerudi uwanjani kwa kuwafungia kazi washambuliaji wake Kibu, Kyombo na Phiri ambaye ni kinara wa mabao ndani ya Simba akiwa amefumania nyavu mara tano kwenye ligi hiyo.

Mgunda alisema ameona mapungufu ya kikosi chake hususan safu ya ushambuliaji kushindwa kuzibadili nafasi wanazotengeneza kuwa mabao na kuishia kuzipoteza jambo ambalo linawagharimu kuibuka na alama tatu.

Alisema ligi imekuwa na ushindani mkubwa, hivyo wamerudi uwanjani kufanya kazi madhaifu yao na kuboresha yaliyo bora kuwa bora zaidi kuelekea mchezo wao wa kesho dhidi ya Namungo FC utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Ni kweli tumekuwa tunatengeneza nafasi nyingi na tunatumia chache, hili nimeanza kulifanyia kazi kwa kuhakikisha makosa haya hayajirudii kwenye michezo ijayo, ligi imekuwa ngumu, wachezaji wanatakiwa kuwa makini ili kufikia malengo," alisema Mgunda.

Alisema mbali na ligi kuwa ngumu, pia ratiba imebana kutokana na mechi kuwa karibu karibu, lakini wachezaji wanapambana kuhakikisha wanafuata maelekezo anaowapa mazoezini ili kupata matokeo chanya.

"Kikubwa ni mshikamano baina yetu na mashabiki, wachezaji wanapambana kuendelea kupata matokeo mazuri katika mechi zetu zijazo, tutaendelea kujituma kwa ajili ya mechi zijazo," alisema Mgunda.

Alisema mechi ijayo (kesho) dhidi ya Namungo FC, si nyepesi kwa kuwa wapinzani wao hao ni wazuri, lakini wanajipanga

INAENDELEA UK. 31



KYOMBO

# Nabi na kiwango kibovu Yanga SC

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amekiri timu yake haikucheza vizuri kwenye mechi ya juzi dhidi ya Kagera Sugar katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza licha ya kushinda bao 1-0, lakini alitarajia kukutana na changamoto hiyo kutokana na mazingira mengi kutokuwa rafiki.

Akizungumza baada ya mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Nabi alisema uchovu wa wachezaji wake kutokana na safari, mvua iliyonyesha Mwanza na mazingira ya uwanja, alitarajia kuwaona wachezaji wake kutocheza vizuri, hivyo amewataka radhi wanachama na mashabiki wa Yanga, akisema kuwa huenda kwenye mechi ya Alhamisi dhidi ya Singida Big Stars, kiwango ambacho wamekizoea kitaonekana.

"Ni kweli kiwango hakikuwa kizuri, lakini tulitarajia hilo, na ndiyo maana tulibadilisha hata mfumo wa uchezaji, tulianza na mabeki watatu na mastraika wawili ili tucheze mpira wa moja kwa moja na hii inatokana mazingira ya uwanja, mvua na safari, tumefika hapa kila mchezaji anashindwa hata kukimbia. Hata hivyo sisi tunataka kuwa bingwa, ukitaka kuwa hivyo unapaswa kucheza kwenye mazingira yote, si timu nyingi zinaweza kupata ushindi kwenye mazingira kama haya," alisema Nabi.

Hata hivyo, alisema hawatolalamika kwa sasa kwa sababu wameshasema vya kutosha, lakini wao wanaangalia mechi inayokuja

"Hatutalalamika, tunaliacha tumeshasema vya kutosha, sisi tunaangalia mechi ya Alhamisi. Nawaomba msamaha mashabiki wa Yanga kwa kiwango kibovu tuli-

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >